

Kiswahili

kwa

Shule za Rwanda

Kidato cha Kwanza

Mwongozo wa Mwalimu

© 2020 Bodi ya Elimu Rwanda

Haki zote zimehifadhiwa.

Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Elimu Rwanda.

Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Elimu Rwanda wakati yaliyomo yamenukuliwa.

DIBAJI

Mwalimu mpendwa,

Bodi ya Elimu Rwanda inayo heshima kwa kutoa mwongozo wa mwalimu kwa kidato cha kwanza katika ngazi ya chini ya elimu ya sekondari.

Mwongozo huu ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira.

Ili kwenda sambamba na juhudzi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa, namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenyenye mchakato wa kujifunza ambao unamwezesha mwanafunzi kuendeleza mawazo yake na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yaye ya binafsi au katika makundi. Wanafunzi, kwa msaada wa wakufunzi, watapata stadi za lugha zinazofaa zitakazowawezesha kutumia yale waliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, wataonyesha tofauti siyo tu katika maisha yao binafsi bali pia hata kwa taifa .

Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji iliyositisiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka kwa yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mwalimu.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzhishwa kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, ili kutumia kitabu hiki kwa ufanisi, jukumu lako kama mkufunzi litakuwa :

- Kuandaa masomo yako na vifaa vya ufundishaji vinavyofaa,

- Kuandaa majadiliano katika makundi ya ushirikiano ya wanafunzi ukizingatia umuhimu wa ushauri kuwa kujifunza hufanyika kwa ufanisi wakati mwanafunzi afanyapo kazi kwa kushirikiana na watu wanaomzidi maarifa na uzoefu;
- Kushirikisha wanafunzi kwa kupitia kazi za ujifunzaji kama: njia ya uchunguzi, makundi ya mijadala, utafiti, mazoezi ya utafiti na kazi za kibinagsi;
- Kutoa fursa ya usimamizi kwa wanafunzi kwa kuendeleza uwezo wao, kwa kuwapa ushindani tofauti na kutoa majukumu yanayoongeza tafakuri tunduizi, utatuvi wa matatazo, ubunifu na uvumbuzi, mawasiliano na ushirikiano;
- Kutoa msaada na kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kwa kutathmini mchango wa wanafunzi katika mazoezi ya darasani;
- Kuwaongoza wanafunzi ili waweze kuoanisha matokeo ya utafiti;
- Kutilia maanani tathmini ya kazi binafsi na kazi za makundi zilizofanyika darasani kwa kutumia mchakato na mbinu za tathmini zinazoegemea katika uwezo wa wanafunzi,
- Kuutumia mwongozo kutakusaidia katika kazi yako ya kufundisha kwani yaliyomo katika mwongozo huu wa mwalimu yanaeleweka kiasi kwamba unaweza kutumiwa kwa urahisi.

Ingawa mwongozo huu wa mwalimu una majibu kwa kila kazi zote zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi, unaombwa kupitia kila swali na kazi kabla ya kutathmini.

Napenda, kwa moyo wote, kutoa shukrani zangu kwa watu wote walioshiriki kutoa mchango wao wa kuboresha mwongozo huu wa mwalimu, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda (REB/CTRL) walioandaa mchakato wa kazi hii tokea ilipoanzishwa.

Pongezi maalum ziwaendee walimu wa ngazi tofauti kwa msaada wao wa kuendeleza na kukamilisha zoezi hili.

Maoni au mchango wowote wa mawazo unakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo mengine yatakayofuata baadaye.

Dkt. Irénée NDAYAMBAJE

Mkurugenzi Mkuu, Bodi ya Elimu Rwanda

SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki cha mwongozo wa mkufunzi. Kitabu hiki kisingeliwezekana bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki; jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu za kwanza ni kwa wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda walioshiriki katika kuandaa na kuandika kitabu hiki. Pia napenda kutoa shukrani kwa walimu wa ngazi zote kwa juhudi zao katika ufanikishaji wa kazi hii ya thamani.

Aidha, natoa shukrani kwa uongozi wa shule mbalimbali nchini Rwanda kwa kuwaruhusu walimu kushiriki katika kukiandaa na hata kukikamilisha kitabu hiki.

Joan MURUNGI

Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana (CTLR)

YALIYOMO

Mada Kuu: Kuelewa mazungumzo na kujieleza kimazungumzo	1
Mada Ndogo: Maamkizi na utambulisho	1
Somo la Kwanza	
Maana ya maamkizi	4
Somo la Pili	
Aina mbalimbali za maamkizi	11
Somo la Tatu	
Matumizi ya nafsi na viwakilishi vya nafsi katika maamkizi	16
Mada Kuu: Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali	21
Mada Ndogo: Msamiati wa mazingira ya shule	21
Somo la Kwanza	
Mazungumzo shulenii	23
Somo la Pili	
Mazungumzo kati ya wanafunzi	30
Somo la Tatu	
Viongozi wetu shulenii.....	38
Somo la Nne	
Shule yangu	45
Somo la Tano	
Usafi shulenii	53
Mada Kuu: Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali	62
Mada Ndogo: Msamiati katika mazingira ya nyumbani	62
Somo la Kwanza	
Aina za nyumba, watu wanaoishi humo na ujenzi wa nyumba (vifaa).....	65
Somo la Pili	
Vifaa mbalimbali vinavyopatikana nyumbani	70
Somo la Tatu	
Mifugo wanaopatikana nyumbani na vivumishi vya ngeli ya A – WA.	76

Somo la Nne	
Majina yanayohusishwa na watu na uhusiano wao kijamii pamoja na vivumishi vya ngeli ya A-WA	81
Somo la Tano	
Uhusiano wa kifamilia pamoja na vivumishi vya ngeli ya A-WA	86
Mada Kuu: Msamiati wa Mazingira Mbalimbali	91
Mada Ndogo: Msamiati wa Mazingira ya Utawala	91
Somo la Kwanza	
Nchi yangu.....	94
Somo la Pili	
Ofisi ya tarafa yangu.....	106
Somo la Tatu	
Utawala Bora	115
Mada Kuu: Msamiati wa mazingira mbalimbali	124
Mada Ndogo: Msamiati wa mazingira ya sokoni.....	124
Somo la Kwanza	
Mnunuzi na muuzaji	126
Somo la Pili	
Biasara mbalimbali	134
Somo la Tatu	
Mazingira ya Sokoni	143
Mada Kuu: Matumizi ya msamiati kuhusu usafi wa mwili	151
Somo la 1	
Maana ya Usafi wa Mwili	155
Somo la pili	
Msamiati wa Mwili na Mazingira.....	160
Somo la 3	
Usafi wa Mwili na Mazingira	164

Ramani ya Yaliyomo

	Mada 1: Kuelewa Mazungumzo na Kujieleza Kimzungumzo	Mada 2: Msamiati katika Mazingira ya Shule	Mada 3: Msamiati katika Mazingira ya Nyumbani	Mada 4: Msamiati katika Mazingira ya Utawala	Mada 5: Msamiati katika Mazingira ya Sokoni	Mada 6: Msamiati katika Mazingira ya Usafi wa Mwili
Idadi ya Vipindi	8	10	11	10	11	12
Mpangilio wa Darasa	-Darasa zima -Makundi -Mwanafunzi binafsi	-Darasa zima -Makundi -Mwanafunzi binafsi	-Darasa zima -Makundi -Mwanafunzi binafsi	-Darasa zima -Makundi -Mwanafunzi binafsi	-Darasa zima -Makundi -Mwanafunzi binafsi	-Darasa zima -Makundi -Afisa wa afya -Mludumu wa afya -Mshauri
Vifaa	-Vinaso sauti. -Vifaa ya vifaa -Vifaa ya shule -Vifaa vile vitabu, madaftari, penseli, kitit cha mwalimu, meza, kalamu, kifutio, kabati la vitabu, rula, kifutio, ubao, chaki na saa -Kitabu cha mwanafunzi -Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyowezza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum	-Vinaso sauti. -Picha -Vitabu. -Redio na simu. -Vifaa au zana kwa wanafunzi wasiojiweza au walio wazito kuelewa.	Ramani ya Rwanda inayonyesha mpango mkuu wa mazingira Picha au michoro ya nyumba za jadi na za kisasa Michoro ya vifaa tofauti ndani ya nyumba Picha za mifugo tofauti Kitabu cha mwanafunzi Vinaso sauti	Ramani ya Rwanda inayonyesha mpango mkuu wa mazingira Picha au michoro ya nyumba za jadi na za kisasa Michoro ya vifaa tofauti ndani ya nyumba Picha za mifugo tofauti Kitabu cha mwanafunzi Vinaso sauti	-Bidhraa tofauti zipatikanazo Sokoni -Pesa -Picha au michoro ya watu na bidhaa sokoni -Kitabu cha mwanafunzi -Vinaso sauti	-Skeletoni -Picha au michoro ya mwili wa binadamu -Mwanafunzi fulani -Kitabu cha mwanafunzi -Vinaso sauti

<p>- Kubaini aina za salamu mbalimbali zinazotumiwa katika Kiswahili kufuatana na nyakati mbalimbali (asubuhii, mchana, jioni)</p> <p>- Kurudia maneno yanayotumivu katika kujitambulisha au kumtambulisha mtu mwagine.</p> <p>- Kutaja na kurudia maneno maalumu yanayotumivu katika kuragana</p> <p>- Kuonyesha kwa usahihii matamshi sahihi ya seauti za Kiswahili.</p> <p>- Kuainisha na kueleza nafsi za Kiswahili na matumizi yake.</p>	<p>- Kubainisha na kuainisha vifaa tofauti vitumiwayyo nyumbani.</p> <p>- Kukumbuka mabadiiliko yanayojoitekeza katika umoja na wingi wa majina ya ngelei ya A-WA pamoa na vivumishi vyake.</p> <p>- Kubairisha na kuainisha aina za nyumba na vifaa vinavyoziengen.</p> <p>- Kubusisha watu mbalimbali katika uhusiano wa familia kwa watu wa nyumbani</p> <p>- Kubraia majina ya mifugo mbalimbali iliopo nyumbani</p> <p>-Kuelzea umuhimu wa usafi nyumbani.</p> <p>- Kuorodhesha majina ya mifugo wa nyumbani</p>	<p>-Kuonyesha mahali Rwanda lipo kweneye ramani ya dunia pamoa na ramani ya Afrika.</p> <p>-Kutaja nchi zinazopakana na Rwanda kwa kuzingatia pande nne za dunia.</p> <p>-Kutaja nembo mbalimbali za nchi na serikali na viongozi wakuu wa kiserikali.</p> <p>-Kutaja siku za wili na miezi ya mwaka pamoa na kuosoma tarehe.</p> <p>-Kutaja na kubainisha maeneo ya kuitawala nchini Rwanda kama vile mtaa, tarafa, jumbo na wilaya.</p> <p>-Kubani matumizi sahihi ya umoja na wingi wa majina ya Ngelei ya U-/ na I-ZI pamoa na matumizi ya vivumishi vinavyoambatana.</p>	<p>-Kuonesha umahiri wa namna ya kuiliza bei ya bidhaa mbalimbali.</p> <p>-Kubaini makundi na majina ya bidhaa mbalimbali zilizopo sokoni.</p> <p>-Kutoa mfano wa maneno yetumiwayo katika hesabu ambayo yanabeba sauti za kipekee za Kiswahili na kuzingatia utamkaji sahihi wake k.m.[th] na [dh].</p> <p>-Kuonyesha ujuzi wa kuhesabu toka moja hadi elfu kumi.</p> <p>-Kukumbuka vipimo vitumiwayo katika upimaji wa viti tofauti.</p>	<p>-Aya na maisha bora -Usafi wa mwili na fikra</p> <p>-Mazingira bora ya mwili na hali inayotuzunguka -Matumizi bora ya pesa</p> <p>-Elimu kwa pamoa -Usawa wa kijinsia</p> <p>-Utamaduni wa kiusanifishaji</p> <p>-Masomo ya ujinsia na uzazi</p>
---	---	---	--	---

<p>-Stadi za utafiti</p> <p>-Ubunifu na ugunduzi</p> <p>-Ujifunzaji wa muda mrefu</p> <p>-Ushirikiano na stadi za maisha</p> <p>-Mawasiliano katika lugha rasmi</p> <p>-Tafakuri tандузи.</p> <p>-Uslughishajji na tандузи.</p> <p>-Usuluhishajji wa muda mrefu</p> <p>-Ushirikiano na stadi za maisha</p> <p>-Mawasiliano katika lugha rasmi</p> <p>Stadi za utafiti</p> <p>Ubunifu na ugunduzi Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha</p> <p>Ujifunzaji wa muda mrefu</p> <p>Ushirikiano na stadi za maisha</p> <p>Mawasiliano katika lugha rasmi</p> <p>Usuluhishajji wa muda mrefu</p> <p>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha</p> <p>Ujifunzaji wa muda mrefu</p> <p>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha</p> <p>Ujifunzaji wa muda mrefu</p>	<p>Tafakuri tандузи Usuluhishajji wa matatizo</p> <p>Mawasiliano katika lugha rasmi</p> <p>Stadi za utafiti</p> <p>Ubunifu na ugunduzi Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha</p> <p>Ujifunzaji wa muda mrefu</p> <p>Ushirikiano na stadi za maisha</p> <p>Mawasiliano katika lugha rasmi</p> <p>Usuluhishajji wa muda mrefu</p> <p>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha</p> <p>Ujifunzaji wa muda mrefu</p> <p>Ushirikiano na stadi za maisha</p> <p>Mawasiliano katika lugha rasmi</p> <p>Usuluhishajji wa muda mrefu</p> <p>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha</p> <p>Ujifunzaji wa muda mrefu</p> <p>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha</p> <p>Ujifunzaji wa muda mrefu</p>	<p>Tafakuri tандузи Usuluhishajji wa matatizo</p> <p>Mawasiliano katika lugha rasmi</p> <p>Stadi za utafiti</p> <p>Ubunifu na ugunduzi Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha</p> <p>Ujifunzaji wa muda mrefu</p> <p>Ushirikiano na stadi za maisha</p> <p>Mawasiliano katika lugha rasmi</p> <p>Usuluhishajji wa muda mrefu</p> <p>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha</p> <p>Ujifunzaji wa muda mrefu</p> <p>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha</p> <p>Ujifunzaji wa muda mrefu</p> <p>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha</p> <p>Ujifunzaji wa muda mrefu</p>
<p>-Kutofautisha salamu mbalimbali kulingana na mazingira pamoja na rika na kuweza kuzitumia kwa usahili.</p> <p>-Kuchagua orodha ya watu mbalimbali wanaosalimilwa kwa kutumia neno “Shikamoo.”</p>	<p>Kuwapanga watu wa ryumbani kutohaka na uhusiano uliopo katiyao.</p> <p>-Kutungu sentensi fupi kwa kuzingatia matumizi rasmi ya majina ya ngeli. Ya A-WA pamoa na vivumishi vyake.</p> <p>-Kulinganisha na kutofautisha shule moja na nyinge kwa kuzingatia mazingira na shughuli zifanyikazo.</p> <p>-Kugundua uhusiano wake na watu wengine wapatikanao shulenii au dasarani.</p>	<p>-Kujadiliana na mnunuzi au muuzaaji bei ya bidhaa mbalimbali (mawasiliano katya mteja na muuzaaji).</p> <p>-Kutumia pande nne za dunia kuelezea kitu, malali, au mtu yupo upande upi.</p> <p>-Kupanglia siku za wiki, mlezi ya mwaka kwa kuzingatia majina yake na kipi kinaanza mwanzo hadi kile cha mwisho (jumattatu, Jumanne...)</p>
<p>Stadi/ Ujuzi</p>	<p>Kutumia msamati husika kwa usahili katika maamkizia au salamu mbalimbali, kuagana na kuigiza katika mawasiliano.</p>	<p>-Kutumia msamati wa sehemu za mwili wa binadamu kwa kutunga sentensi sahihi katika mawasiliano.</p> <p>-Kulinganisha na kutofautisha sehemu muhimu za mwili wa mtu na</p>

	<p>- Kugundua mabadiliko Yapi yanayoitokeza katika maneno ya salamu kama vile sijambo, hujambo, hajambo yanapokuwa katika wingi.</p> <p>- Kuziweka nafsi za Kiswahili katika makundi yake yaani; nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu katika umoja na wingi na kuzitumia kwa usahihii katika salamu na utambulisho.</p>	<p>-Kutumia msamati sahihi kuhusu vifaa vitumiwavyo darasani katika mawasiliano rahisi.</p> <p>-Kutumia vyema maelekezo aliyopewa na mwalimu katika kusikiliza na kusoma kwa ufasana kitfungu cha habari kinachohusika.</p> <p>Kutunga sentensi ifupi kwa kuzingatia wakati uliopo.</p>	<p>- Kuiweka vifaa nya nyumbani katika makundi na kubainisha majina yake. -Kuchunguza dhima au kazi ya kila aira ya mifugo iliyo po nyumbani.</p> <p>- Kuiwegawayna nyumbaa katika sehemu zake muhimu -</p> <p>Kuchambua sifa za vyumba vya nyumba ya kisasa.</p>	<p>- Kutumia ujuzi wa kupanga ratiba au kueleza utokeaji wa matukio mbalimbali.</p> <p>-Kuiyawanya nchi ya Rwanda kwa kuzingatia maeneo yake ya kiutawala (tarafa, wilaya, mkoau jimbaji).</p> <p>- Kutorautisha na kutumia mizani au vipimo kulingana na kitu kinachohusika na upimaji (K.m. kilo moja ya mchele, mita, ita moja ya maji au mafuta, n.k.)</p>	<p>-Kutumia ujuzi wa kuhesabu nambari, pesa katika kufanya ununzu au uuzaaji wa bidhaa (kulipa pesa au kururidha salio).</p> <p>-Kutofautisha na kutumia mizani au vipimo kulingana na kitu kinachohusika na upimaji (K.m. kilo moja ya mchele, mita, ita moja ya maji au mafuta, n.k.)</p>	<p>-Kutumia ujuzi wa kuhesabu nambari, pesa katika kufanya ununzu au uuzaaji wa bidhaa (kulipa pesa au kururidha salio).</p> <p>-Kutofautisha na kutumia mizani au vipimo kulingana na kitu kinachohusika na upimaji (K.m. kilo moja ya mchele, mita, ita moja ya maji au mafuta, n.k.)</p>
	<p>- Kuonyesha adabu na heshima kwa watu mbalimbali wanaomzunguza katika mazingira tofauti.</p> <p>- Kuonyesha uttamaduni wa kusalimiana, kuaga na kuagana, na kuititia salamu kwa usahihii.</p> <p>- Kuonyesha shauku ya kufahamiana na watu mbalimbali wamzungukao</p>	<p>-Kujivunia au kuionea shule yake fahari.</p> <p>-Kuheshimu vifaa vya shule kwa kujiepusha na uharibiu wowote dhidi ya vifaa hivyo.</p> <p>-Kuimarisha usafi katika mazingira mbalimbali.</p> <p>-Kujengwa mahusiano mema na watu wengine wote walipo shulenii na nje ya shule.</p>	<p>-Kujivunia au kuionea shule yake fahari.</p> <p>-Kuheshimu vifaa vya shule kwa kujiepusha na uharibiu wowote dhidi ya vifaa hivyo.</p> <p>-Kuimarisha usafi katika mazingira mbalimbali.</p> <p>-Kujengwa mahusiano mema na watu wengine wote walipo shulenii na nje ya shule.</p>	<p>- Kuboresha afya kwa kuimarisha usafi wa mazingira.</p> <p>- Kuwaheshimu watu kulingana na uhusiano uliopo katii yao.</p> <p>- Kupambana na umasikini kwa njia ya mifugo na ufundi</p>	<p>-Kujivunia nchi yake na kujependa kwa kuimarisha uzalendo na usalama wa nchi hiyo.</p> <p>-Kuheshimu nembo za taifa na viongozi wa nchi.</p> <p>-Kushirikitiana na Wanyarwanda wote pamoa na rai a wa nchi zinazozunguka Rwanda katika harakan za kupigana na umaskini na kugombanii haki za kibinadamu.</p> <p>-Kuimarisha usafi katika mazingira mbalimbali.</p> <p>-Kujengwa mahusiano mema na watu wengine wote walipo shulenii na nje ya shule.</p>	<p>-Kuimarisha mtindo wa huduma bora katika kazi yevote na hasa biashara.</p> <p>-Kutokata tamaka au kutokasirika ovyo wakati wa mazungumzo au wakati wa kujadilia bei.</p> <p>Kujengwa umaskini katika masuala yanayohusika na pesa.</p> <p>-Kuheshimu na kufurahia tofauti zilizomo katika lugha na tamaduni nyingine kama Kiswahili.</p> <p>-Kumheshimu ntu yeote wakati wa mazungumzo au majadiliano.</p>
	<p>Maadili na Mwenendo Mwemenda</p>					

UTANGULIZI

Nafasi ya Kiswahili katika jamii na katika mfumo wa elimu

Lugha ya Kiswahili imepewa hadhi kubwa kwa kuteuliwa kuwa mojawapo katika lugha rasmi za Jumuiya ya Afrika. Nchini Kenya na katika nchi ya Tanzania, Kiswahili ni lugha ya taifa na pia lugha rasmi. Nchi za Uganda na Burundi nazo hazijaachwa nyuma kwani lugha ya Kiswahili imeanza kumea mizizi huko na kufunzwa kikamilifu.

Nchi nyingine kama Amerika, Ujerumani na mataifa mengi ya Ulaya yameanza kufunza lugha ya Kiswahili katika vyuo vikuu. Wanaelewa kuwa Kiswahili ndiyo lugha inayoweza kuunganisha nchi za ng'ambo na Afrika. Lugha hii huwafaa sana watalii wanaozuru Afrika.

Mipango imefanywa ili kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inawekwa katika programu za tarakilishi na kwenye mtandao duniani kote. Ni wazi kuwa Kiswahili kinapiga hatua kwa kasi sana ili kuweza kwenda na wakati.

Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini Rwanda

Somo la Kiswahili limekuwa likifundishwa katika viwango vya elimu vya sekondari nchini Rwanda. Kwa sasa, somo hili linatathminiwa kitaifa.

Lugha ya Kiswahili imepewa nguvu zaidi hasa tukizingatia kuwa wanafunzi wengi hulichukua somo hili katika sekondari na vyuo vikuu na kupata mafunzo katika fasihi na isimu, na kufuzu katika somo hili. Tukitilia maanani mambo haya yote, tutaona kuwa wizara ya elimu imeipa lugha ya Kiswahili heshima inayostahili na kuhakikisha kuwa lugha hii inakuzwa.

a) Ufahamu

Ufahamu ni kipengele muhimu katika lugha ya Kiswahili. Kuwaruhusu wanafunzi kusoma kwa sauti huku wakipokezana kwa zamu ni muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu wa Kiswahili anashauriwa awe ameteua kifungu kabla ya kipindi kuwadia. Auchambue msamiati mpya na kuupigia mstari ama kuuandika kwenye daftari la kumbukumbu. Angalau kila mwanafunzi apate fursa ya kusoma sentensi kadhaa. Mwalimu ayakosoe makosa yoyote ya matamshi.

b) Sarufi

Sarufi ni mpangilio maalum wa maneno kwa ufasaha kulingana na kanuni zake au kupanga na kutumia maneno vizuri kulingana na mipango au taratibu zilizokubaliwa kuwa ni sahihi. Sehemu muhimu katika sarufi ni ngeli. Mtu yejote asiyejua na kuzitawala ngeli kamwe hawezi kusema kuwa anaielewa lugha ya Kiswahili. Atakuwa akituhadaa. Sarufi pia hujumlisha sehemu muhimu kama vile matamshi, majina, vielezi, vitenzi, viambishi, uakifishaji, nyakati, vivumishi, mnyambuliko wa vitenzi na nyakati.

Mwalimu atumie mbinu mbalimbali katika kuwafunza wanafunzi sarufi. Mwalimu atafute nyenzo zinazofaa na rahisi kupata. Mwalimu asitafute nyenzo ambazo

zitagharimu kiasi kikubwa cha pesa. Mwalimu aunde vifaa vyake ili kuepuka matumizi ya pesa kwa minajili ya kuvinunua.

Mwalimu awatathmini wanafunzi wake ili kutambua kama yale yote waliyojifunza wameelewa. Endapo watatokea wanafunzi ambao hawajaelewa basi mwalimu achukue jukumu la kuwasaidia wanafunzi wake mmoja mmoja kibinagsi kutegemea matatizo yao.

c) Msamiati

Katika kufunza msamiati, ni jambo la busara endapo mwalimu atatumia vifaa halisi katika kueleza maana na matumizi ya msamiati. Endapo vifaa vingine ni vigumu kuvipata basi mwalimu anaweza kutumia picha au aandae chati nzuri ili kulifanya funzo hili kueleweka kwa urahisi na pia kulifanya kuwa la kusisimua zaidi. Aidha, mwalimu anaweza kuunda au kubuni kwa mfano matumizi ya katoni kuunda mfano wa tarakilishi pale ambapo si rahisi kuipata na kuileta darasani ili kuizungumzia.

Mwalimu anaweza kufunza msamiati kwa njia ya ufahamu. Hapa itambidi mwalimu awaongoze wanafunzi kupata maana kutokana na habari yenye. Katika funzo la msamiati, ni bora mwalimu awaambie wanafunzi watunge sentensi wakitumia msamiati waliojifunza.

d) Kusikiliza na kuzungumza

Kusikiliza na kuzungumza ni kipengele muhimu sana katika kujifunza lugha yoyote ile. Ni wazi kuwa mtu ambaye hajapata kusikia neno lolote, yaani alizaliwa kiziwi, kamwe hawezi kuongea. Ataongea akisema nini? Binadamu ye yeyote alijifunza kuongea kuititia kwa kuwasikiliza watu wengine wakiongea na maneno ya kwanza aliyoazungumza ni yale aliyoasikia.

Ni sharti mwalimu akuze stadi hii muhimu ya kujifunza lugha. Wanafunzi wanaweza kujifunza funzo la kusikiliza na kuzungumza kwa kuigiza mchezo wa kuigiza. Kila mwanafunzi apewe sehemu yake ya kuigiza. Mwalimu ajitayarische kwa kutunga (endapo ana uwezo) au kuteua mchezo wa kuigiza unaofaa kwa kuzingatia maudhui na kiwango cha wanafunzi. Somo hili huwajenga wanafunzi kuwa na uwezo wa kuongea mbele ya wengine kwa ufasaha bila matatizo yoyote.

Hali kadhalika, wanafunzi wanaweza kujadiliana na wenzao kuhusu methali. Wanaweza kuendeleza methali sawasawa kisha waeleze maana ya methali hiyo na hatimaye mwanafunzi mmoja atoe kisa kifupi ambacho kinaunga mkono methali hiyo.

Tathmini katika funzo hili huwa ni maswali ambayo humhitaji mwanafunzi ayajibu kwa kuongea ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wamepata fursa ya kuongea na kuwasikiliza wengine wakiongea, itakuwa bora endapo mwalimu ataandaa mara kwa mara vipindi kabambe vya michezo ya kuigiza, mafumbo, vitendawili, hadithi na hotuba. Aidha, wanafunzi wapewe fursa ya kusikiliza vipindi vya redio na hata inapowezekana, kutazama runinga na kanda za video.

e) Kusoma na kuandika

Wanafunzi katika kiwango hiki wanapaswa kuwa wanajua kusoma kwa ufasaha. Wanaposoma, mwalimu anapaswa kuwa macho kwa sababu wanafunzi wengine huenda wakawa na mbinu mbaya ya usomaji. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi hawasogezi kitabu karibu sana na macho na pia hawatumii vidole kuelekeza macho. Hio si mbinu nzuri na ni sharti mwalimu aikatae.

Mwalimu anapaswa kusoma taarifa ambayo anawatarajia wanafunzi wasome. Achambue maneno magumu ambayo yametumika na kuelewa maana. Awambie wanafunzi wasome mmoja mmoja kwa sauti huku akisikiliza kwa makini ili kukosoa makosa yote ya matamshi. Ni bora zaidi mwalimu ayaandike maneno magumu ubaoni. Awaelekeze wanafunzi wapate maana ya maneno magumu kutokana na makala waliyoyasoma.

Katika kuandika, mwalimu asisitize kuhusu hati nadhifu inayosomeka kwa urahisi. Kila herufi iandikwe vizuri. Mwalimu aziandike herufi ubaoni na kuwaonyesha wanafunzi jinsi zinavyoandikwa. Mwalimu azungumzie kuhusu uakifishaji bora. Mwalimu awape zoezi la kuandika na kuhakikisha kuwa wanafunzi wamefuata maagizo.

Mwalimu anaweza kuandaa funzo la imla ambapo anapaswa kuteua sentensi nzuri zenye maneno ambayo huwatatiza wanafunzi wake. Kisha ayaandike ubaoni na kuwaongoza wanafunzi kuyasoma kwa ufasaha. Mwalimu ayafute kisha awambie wanafunzi wayaandike jinsi anavyoyasoma. Njia hii itamwezesha mwalimu kuelewa iwapo wanafunzi wake wameelewa au la. Vile vile mwalimu anaweza kuyasoma maneno (kwa matamshi safi) na kuwaagiza wanafunzi wayaandike.

Tathmini

Hii ndio sehemu muhimu sana kwa sababu hiki ndicho kigezo kinachomwezesha mwanafunzi na mwalimu kutambua kama malengo ya funzo lake yalitimia.

Mwalimu huwatathmini wanafunzi wake ili:

- (a) Kumwezesha mwalimu kuelewa hatua walizopiga wanafunzi.
- (b) Kumtia mwanafunzi moyo wa kuendelea kujifunza.
- (c) Kumsaidia mwalimu kuelewa maendeleo yake katika kufunza.
- (d) Kumwezesha mwalimu kuelewa kama ametimiza malengo yake vizuri ili aweze kurudia funzo inapobidi.
- (e) Kumwezesha mwalimu kutambua kama malengo ya funzo lake yalifaulu na kwa kiasi gani.

Aina za tathmini

1. Kuandika muhtasari wa yale waliyoyasoma.
2. Kutahini usahihi wa sentensi zilizoandikwa kwenye madaftari.
3. Kuhakiki matamshi kwa kusoma sentensi au vifungu mbalimbali.
4. Kutunga sentensi zilizoendelezwu vizuri.
5. Kuambatanisha maelezo na maneno kwa usahihi.

6. Mazoezi na marudio ya mtihani wa wiki.
7. Maswali ya chemshabongo darasani ambayo humwezesha mwanafunzi kuelewa aliyoyasoma hapo awali.
8. Mitihani ya kila mwisho wa muhula.

Ni muhimu mwalimu asahihishe kazi za wanafunzi. Aelewe matatizo ambayo yanawakabili wanafunzi ili awafunze upya sehemu yenye matatizo. Mwalimu asisitize kuhusu kufanya masahihisho.

Mwalimu awatambue wanafunzi wenye matatizo na kuwapa msaada maalum. Mwalimu atumie mbinu mbalimbali ili kumwezesha mwanafunzi kuelewa vyema. Mwalimu awe makini sana anaposhughulikia wanafunzi dhaifu ili wasikate tamaa. Daima awatie motisha.

Nyenko za kufunzia

Nyenko ni muhimu katika somo lolote likiwamo Kiswahili. Mwalimu anatarajiwa kuwa mbunifu na kutumia nyenko ambazo zinapatikana kwa urahisi. Ni muhimu mwalimu kuhakikisha kuwa hamna gharama inayoweza kuepukika katika funzo lolote lile. Ni vyema mwalimu abuni baadhi ya nyenko zake.

Mwalimu yejote ni lazima aende na wakati. Wakati huu ambapo teknolojia imekua sana hasa katika mawasiliano, ni muhimu mwalimu atumie vifaa vya kisasa. Kwa mfano, ni muhimu mwalimu kutumia vifaa halisi kama rununu na kutumia picha za baadhi ya vyombo ambavyo ama havipatikani katika mazingira ya shulenii au mwalimu hawezikuvibeba na kwenda navyo darasani kama vile tarakilishi, runinga, kipepesi, n.k.

Ni vyema kwa mwalimu kuyafahamu mazingira ya mwanafunzi wake. Anapofunza kuhusu baruameme, baruapepe, mtandao, wavuti n.k., somo hili litakuwa rahisi kwa wanafunzi wa mjini na kuwaelezea wanafunzi hao ni rahisi sana. Wanafunzi wale ambao hawajawahi kuona wala kusikia mambo hayo, kwao huenda ikawa ni kioja. Hapo mwalimu anatakiwa awe na nyenko za kutosha ili kuwafaa wanafunzi wake. Vifaa vingine vinapatikana kwa urahisi na mwalimu anaweza kuwaambia wanafunzi wake walete baadhi ya vifaa hivyo.

Mwalimu asichukulie funzo lolote kuwa rahisi. Utashangaa kugundua kwamba unapofunza kuhusu mimea, wanafunzi wengi hasa wa mijini hawajapata kuiona mimea mingi. Ni bora kwa mwalimu kutumia picha au mimea yenyewe kama inaweza kupatikana.

Mwisho kabisa, ni vyema kwa mwalimu kuelewa kuwa kufaulu au kutofaulu kwa funzo lolote kunamtegemea mwalimu. Ukiwaona wanafunzi wako wakilipenda somo la Kiswahili ujue kuwa aliyefaulu ni wewe. Ukiwaona wanafunzi wakilalamika kuwa lugha ya Kiswahili ni ngumu na inayosinya basi ujue tatizo ni wewe. Ni jukumu la mwalimu yejote aliyehitimu kuona kuwa wanafunzi wake watakuwa wakilitarajia somo lake na kutaka asitoke darasani. Hapo utakuwa umefaulu. Wewe ndiwe unayewafanya wanafunzi wakuchukie na wewe ndiwe unayeweza kuwafanya wanafunzi wakupende.

Namna ya kuwashughulikia wanafunzi wa aina mbalimbali

Mwalimu anapaswa kwenda darasani akilifahamu jambo moja kuwa wanafunzi wote wanaweza kufunzwa na kuelewa. Mwalimu ajiepushe kabisa na tabia ya kuwapa wanafunzi wengine majina kuwa ni wajinga. Wanafunzi wote wameletwa shulenii kuondoa ujinga. Unapomwita mwanafunzi mjinga uelewe kuwa wewe ndiwe uliyeshindwa kuondoa ujinga huo.

Jinsi wanafunzi walivyotoka katika mazingira tofauti ndivyo wanavyotofautiana na ndivyo walivyo tofauti katika kuelewa somo au funzo lolote. Utawapata wanafunzi wenyewe akili tambuzi kiasi kwamba wakiambiwa kitu huelewa haraka ajabu. Wakipewa zoezi wao hulifanya haraka.

Mwalimu anapaswa kuwa macho na kuwashughulikia vizuri kwa sababu wanaweza kupotoka kwa urahisi. Wanapomaliza zoezi huishia kupiga kelele na kuwasumbua wenzao. Mwalimu anapaswa kuwaandalia mazoezi ya kutosha ili wakimaliza waendelee na mengine.

Mwalimu anapaswa kuwashughulikia barabara wanafunzi wanaochukua muda kuelewa. Akishawapa wengine zoezi achukue muda huo kuwasaidia wanafunzi dhaifu. Ahakikishe kuwa japo watachukua muda kuelewa mwishowe watawafikia wale wanaoelewa haraka.

Mwalimu hupata sifa chungu nzima anapowasadidhia wanafunzi dhaifu kuwa bora. Kufaulu kwa darasa lolote kunategemea wanafunzi wote. Ni bora kwa mwalimu yejote kujikwamua katika kutoa sababu kuwa wanafunzi wake ni dhaifu. Swali bado litamrudia, "Umefanya nini kuondoa udhaifu wao. Umepewa jukumu. Mustakabali wa wanafunzi unakutegemea wewe. Itakuwa ni fahari kubwa utakapowaona wanafunzi wako wakiwa wamefanikiwa vizuri. Wanafunzi pia watamwonea fahari mwalimu wao.

Mwalimu atenge muda wake ili kuwashughulikia wanafunzi wenyewe matatizo mbalimbali hasa wale ambao si wepesi wa kuelewa. Hali kadhalika mwalimu anapaswa kuchukua tahadhari ili asiwakere wanafunzi wengine. *Kwa mfano:* katika kusimulia hadithi anapaswa kutoa hadithi ambazo hazitawadunisha wanafunzi wenyewe upungufu fulani.

Mwalimu ahakikishe kuwa katika mafunzo yake ameshughulikia usawa wa jinsia. Pasiwe na ubaguzi wa aina yoyote.

Ratiba ya mafunzo

Ratiba ni muhimu kwa mwalimu yejote aliyehitimu. Ni sharti mwalimu awe na mwongozo na taratibu za kufuata ili asisahau mambo muhimu.

Mwalimu aandae ratiba kutokana na silabasi ambayo ndiyo mwongozo unaotoa mwelekeo. Mwalimu avitumie vitabu bora vilivyoidhinishwa na wizara ya elimu. Ufuatao ni mfano wa ratiba ya mafunzo katika somo la Kiswahili.

WIKI	KIPINDI	MADA KUU	MADA NDOGO	MALENGO	NYENZO	ASILIA	MAONI
I	I	KUELEWA MAZUNGUMZO NA KUJIELEZA KIMAZUNGUMZO	Maamkizi na Kujitambulisha i) Maana ya Maamkizi	- Kufahamu maana ya maamkizi - Kuonyesha adabu na heshima kwa watu mbalimbali wanaomzunguka mwanafunzi katika mazingira tofauti -Kuonyesha shauku ya kufahamiana na watu mbalimbali.	-Michoro ya watu tofauti wakiamkiana -Vinasauti. -Redio na simu zenyewe uzezo wa kuhifadhi mazungumzo	Kitabu cha wanafunzi ukurasa wa 2-10	
	2		ii) Aina mbalimbali za Maamkizi	-Kubaini aina za salamu mbalimbali zinazotumiwa katika Kiswahili kufuatana na rika, mazingira na nyakati mbalimbali(a subuhimchana,jioni) -Kutofautisha salamu mbalimbali kulingana na mazingira pamoja na rika na kuweza kuzitumia kwa usahihi -Kutumia msamati husika kwa usahihi katika maamkizi, kuagana na kuigiza katika mawasiliano	Michoro ya watu tofauti wakiamkiana- Vinasauti. -Redio na simu zenyewe uzezo wa kuhifadhi mazungumzo.	Kitabu cha wanafunzi ukurasa wa 15-27	
2	3		iii) Matumizi ya nafsi na maamkizi: Viwakilishi vya nafsi	-Kutambua nafsi za Kiswahili -Kutunga sentensi zenye maamkizi pamoja na viwakilishi vya nafsi -Kuandika umoja na wingi wa sentensi zenye maamkizi katika umoja na wingi	Michoro ya watu tofauti wakiamkiana -Vinasauti. -Redio	Kitabu cha wanafunzi ukurasa wa 28-33	

Mpangilio wa funzo

Huu ni utaratibu anaouandaa mwalimu ili kuliendesha vyema funzo lake kuanzia mwanzo hadi tamati. Utaratibu huo humwezesha mwalimu kufuata hatua baada ya nyingine na kuweza kupata picha ya funzo lake mapema kabla. Humwezesha mwalimu kushughulikia maswala yote muhimu katika funzo hili. Kufikia mwisho wa funzo, mwalimu huweza kutathmini ili kuelewa kama funzo lake limefaulu.

Ufuatao ni mfano wa mpangilio wa funzo.

ANDALIO LA SOMO

Jina la shule: BWIZA

Jina la Mwalimu : GASIMBA ERIC

Muhula	Tarehe	Somo	Kidato	Mada	Idadi ya masomo	Muda	Idadi ya wanafunzi
wa kwanza	07/02/2016	Kiswahili	cha kwanza	ya 2	I kwa 2	Dakika 40	46

Aina ya wanafunzi wenyewe mahitaji maalum ya kielimu pamoja na idadi yao: I

1. Mwanafunzi mwenye matatizo ya kusikia.

Mada Kuu:	Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali
Mada Ndogo:	Msamiati wa mazingira ya shule
Uwezo unaohitajiwa katika mada:	Mwishoni mwa mada hii, mwanafunzi atakuwa na uwezo wa kusikiliza kwa makini, kusoma vifungu , na kutumia msamiati muhimu katika mazingira ya shule.
Kichwa cha somo	Mazungumzo shulenii
Uwezo uhitajiwao katika somo	Kufikia mwishoni mwa somo hili, mwanafunzi atawez: <ul style="list-style-type: none"> • Kusoma vyema, kwa sauti na bila kusitasita. • Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati maalum wa shulenii. • Kuigiza mazungumzo kwa kuzingatia msamiati wa shulenii.
Mpangilio wa darasa	Mandhari: Somo linatoka darasani ambamo wanafunzi wataigiza mazungumzo.
Malengo ya kujifunza (Ni lazima yazingatie mahitaji ya wanafunzi wote)	Maarifa na ufahamu: <ul style="list-style-type: none"> • Kujua matamshi bora ya sauti za Kiswahili (irabu na konsonanti) • Kujua msamiati wa shulenii. Stadi: <ul style="list-style-type: none"> • Kuwa na uwezo wa kutunga sentensi sahihi. • Kutokuwa na uoga wa kuongea mbele ya watu hasa wakati wa maigizo. Maadili na mwenendo mwema: <ul style="list-style-type: none"> • Kuonyesha adabu na uadilifu wakati wa majadiliano na maigizo.
Zana au vifaa	Kitabu cha Mwanafunzi, redio, rekoda, ubao, chaki, michoro, wanafunzi wenyeewe.
Marejeo	Kitabu cha Kiswahili, 2016

Muda na kila hatua	Mbinu za kufundishia na kujifunzia Kwa njia ya maigizo katika makundi au kati ya wanafunzi watatu watatu, wanafunzi watasoma na kuigiza mazungumzo shulenii.		
	Wajibu wa mwalimu	Wajibu wa mwanafunzi	
Utangulizi Dakika 5	<ul style="list-style-type: none"> Mwalimu awaamkie wanafunzi kisha awaulize maswali ya dodoso kuhusu kile wanachokiona katika michoro iliyo ndani ya vitabu vyao. Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili washiriki katika mjadala.. 	<ul style="list-style-type: none"> Wanafunzi wajibu salamu za Mwalimu na baadaye wayajibu maswali yake. Wanafunzi wajipange katika makundi kushiriki mjadala.. 	<p>Maarifa:</p> <ul style="list-style-type: none"> - Amani na maadili. - Ujuzi wa matamshi ya sauti zinazopatikana katika kifungu husika. <p>Stadi:</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kusoma kwa usahihi mazungumzo au salamu katika Kiswahili. • Kuigiza mazungumzo au salamu mbalimbali. • Kuzungumza hadharani bila uoga wala wasiwasi.
Somo lenyewe Dakika 30	<ul style="list-style-type: none"> Mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma kifungu kilicho katika vitabu vyao. Kwa kuwa ni mara ya kwanza ya wanafunzi kujifunza lugha hii, mwalimu awasomee kwa sauti na kutumia matamshi sahihi kama mfano wa kuigwa. Kuwaongoza wanafunzi kusoma kwa sauti na kusahihisha matamshi yasiyo sahihi. Kuandika msamati unaoomba matamshi sahihi. Kuwaongoza wanafunzi kuigiza mazungumzo hayo kati ya watu wawili. 	<ul style="list-style-type: none"> Wanafunzi wanatega sikio jinsi mwalimu anavyowasomea na kumfuata kwa makini. Mmoja kwa mmoja au kundi kwa kundi, wanafunzi wasome kifungu husika wakimwiga mwalimu jinsi alivyotamka sauti za Kiswahili. Kutamka maneno maalum yaliyochaguliwa na wanafunzi wenye, mwalimu au yale yaliyonekana kuleta matatizo ya kimatamshi wakati wa kusoma. Kuigiza darasani mazungumzo husika. 	<p>Maadili na mwenendo mwema:</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mwanafunzi kujenga tabia ya adabu mahali popote hasa anapokutana na wengine. <p>Masuala mtambuka yanayoshughulikiwa:</p> <p>• Usawa wa kijinsia</p> <ul style="list-style-type: none"> - Mwanafunzi kushirikiana na wenzake katika uigizaji wa mazungumzo bila ubaguzi wa kijinsia.

Hitimisho Dakika 5	<p>Mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa muhtasari wa msamiati utumikao shulenii</p> <p>Mwalimu awape wanafunzi zoezi la kusoma na kujaza mapengo kwa kuandika.</p> <p>Mwalimu awape wanafunzi kazi ya ziada ili isahibishwe katika somo litakalofuata.</p>	<p>Kusoma msamiati unaotumiwa shulenii mionganii mwa wanafunzi.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Wanafunzi wanashiriki katika zoezi lililotolewa. • Kuandika katika daftari kazi iliyotolewa na mwalimu. 	<ul style="list-style-type: none"> • Elimu isiyo na ubaguzi Katika makundi, wanafunzi wenyewe ulemavu fulani au matatizo mengine ya kimaisha ni lazima nao wapewe haki zao za kushirikishwa sawa sawa na wenzao.
Tathmini ya mwalimu	<p>Kutokana na jinsi wanafunzi walivyoshiriki katika somo hili, mwalimu ataamua mahali atakaposisitiza wakati wa mafundisho kulingana na matatizo mbalimbali yaliyojitekeza kwa wanafunzi fulani.</p>		

MADA KUU: KUELEWA MAZUNGUMZO NA KUJIELEZA KIMAZUNGUMZO

Mada Ndogo: Maamkizi na utambulisho

Idadi ya vipindi: 8

Ujuzi upatikanao katika mada:

Kusalimiana na kuitikia salamu kwa kuzingatia wakati na rika mbalimbali za watu.

Kujitambulisha na kumtambulisha mtu mwingine.

Kutumia kwa ufasaha vipengele fulani vya kisarufi kuhusu umoja na wingi katika salamu pamoja na nafsi za Kiswahili.

Uhusiano wake na masomo mengine:

Somo la stadi za jamii kuhusu mwenendo mwema shulenii pamoja na adabu.

Vifaa vya kujifunzia:

- Vinasa sauti.
- Picha za watu wa umri mbalimbali wakisalimiana.
- Kujitambulisha na kuagana katika mazingira mbalimbali.
- Vitabu vya wanafunzi.
- Redio na simu zenye uwezo wa kuhifadhi mazungumzo.
- Vifaa au zana kwa wanafunzi wasiojiweza au wasioelewa kwa haraka.

Vigezo vya tathmini au upimaji:

- Kusalimiana na watu mbalimbali katika nyakati na mazingira tofauti.
- Kujitambulisha na kumtambulisha mwenzake.
- Kusikiliza maamkizi na kuzungumza kwa ufasaha.
- Kuaga au kuitikia pale mtu anapoagwa katika mazingira mbalimbali.

Maelezo kwa mwalimu

Mwalimu aeleze kuwa; maamkizi ni njia ya kujuliana hali. Watu wote hujuliana hali, wakubwa kwa wadogo. Mwalimu asisitize mifano iliyopo kwenye michoro ilio katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 2-3 na kutoa mifano katika hali mbalimbali kutokana na mazingira mengine. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la kuamkiana na kuuliza maswali ya dodoso.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote; waoga, walemvu na wengine kwani maamkizi ni sehemu muhimu ya maisha ya mwanadamu. Awambie kuwa kutabasamu, kuonyesha uaminifu na hata kukumbatiana ni kati ya njia ambazo hutumika katika maamkizi.

Mwalimu pia afafanue umuhimu wa umri na maamkizi. Kwa nini wadogo ndio hutumia ‘shikamoo’ tu? Pia, aeleze hali mbalimbali na nyakati zinavyoathiri aina za maamkizi ambazo hutumika.

Mwalimu afafanue msamiati unaohusiana na maamkizi na maneno yote yaliyotumika katika somo na kuhakikisha wanafunzi wanaelewa somo na wanalfurahia.

- a) Mwalimu atumie mifano ya utamaduni katika jamii mbalimbali wanamotoka wanafunzi.
- b) Mwalimu ataje tamaduni za mataifa jirani.
- c) Mwalimu atumie hadithi na maigizo ikiwezekana. Mfano; (kuamkiana na mwanafunzi mmoja pale darasani) katika umoja na wingi wa salamu.

Mwalimu pia awakumbushe wanafunzi kuhusu alfabeti na irabu za Kiswahili kabla ya kukabili somo la matamshi na tahajia.

Masuala mtambuka

- Amani na maadili.
- Umoja na uwiano wa kijamii.
- Usawa na heshima kijinsia.
- Udumishaji wa utamaduni.
- Elimu.

- Kuepuka mambo ambayo yanaweza kusababisha mafarakano kati ya watu.
- Mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa.

Ujuzi wa jumla

- Stadi za utafiti.
- Ubunifu na ugunduzi.
- Ujifunzaji wa muda mrefu.
- Ushirikiano na stadi za maisha.
- Mawasiliano kwa lugha rasmi.
- Tafakuri tanduizi.
- Usuluhishaji wa matatizo.

Maana ya maamkizi

Muda: Kipindi I

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha mazungumzo yanayohusu maamkizi.
- Kueleza maana ya maamkizi na kuyafahamu.
- Kuamkiana kwa lugha ya Kiswahili.

b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe.
- Vinasa sauti.
- Michoro au picha katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 2
- Vitabu hasa vya wanafunzi, ukurasa 2
- Wafanyakazi shulenii.

c) Maandalizi ya somo

Kipindi hiki kinahusu maisha ya watu ya kila siku na utamaduni wao. Mwalimu ahakikishe kuwa kipindi kimesisimua. Pia, ahakikishe anakosoa salamu za vijana ambazo haziendi pamoja na utamaduni na hadhi ya jamii pana. Kuwaweka wanafunzi katika vikundi baada ya kuwaamkia na wao kuitikia ili waigize nje kutafaa sana. Pia mwalimu anaweza kuwaauliza wanafunzi maswali ili wayajibu na kueleza salamu za mwalimu wa zamu na mwalimu mkuu katika gwaride. Wanafunzi waigize maamkizi yanayowahusu wote na kwa hivyo mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi anashiriki hata wale wenye taathira mbalimbali. Ishara za viungo vya mwili ni muhimu sana katika kufanikisha somo hili.

d) Utaratibu wa somo

Hatua ya 1: Utangulizi

- Mwalimu awaamkie wanafunzi.
- Wanafunzi waitikie maamkizi ya mwalimu.

- Mwalimu awaulize wanafunzi wazungumzie maamkizi ya mwalimu mkuu kwenye gwaride.
- Mwalimu awapange wanafunzi kwenye makundi ili kuigiza maamkizi.
- Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufasiri michoro au pitcha na kuigiza mazungumzo yaliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi uk 2-8*.

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali kama vile: Mnaona nini? Wahusika wanafanya nini? Kisha wanafunzi waeleze wanachokiona.

Mwalimu aulize maswali ya dodosi. Ayajibu maswali ya wanafunzi na kuyakosoa maelezo yao ama salamu potoshi.

Hatua ya 2: Maigizo ya maamkizi mbalimbali

Mwalimu awaongoze wanafunzi kuigiza maamkizi yaliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi ukurasa 7-8*. Wanafunzi wazingatie maadili na utamaduni wa kushirikiana na kufana katika jamii. Hatimaye mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu zoezi kuhusu maamkizi. Mwalimu atoe zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu. Mwalimu asahihishe na kuwakosoa wanafunzi.

Hatua ya 3: Msamiati wa maamkizi

Mwalimu atumie fursa hii kuelezea; maana ya utamaduni unaondamana na maamkizi, maana na nyakati za kufanya hivyo kama sehemu ya kurahisisha msamiati.

Mifano:

- | | |
|------------|---|
| • Makiwa | – Tunayo: Huambiwa mtu aliyefiwa. |
| • Shikamoo | – nakushika miguu: Mdogo humwambia mkubwa kuonyesha heshima. |
| • Hujambo | – huna jambo?; kujulia hali. |
| • Sijambo | – sina jambo. |
| • Kwaheri | – kuagana. |
| • Buriani | – (huzuni) mtu anayeaga kwa muda mrefu na hakuna tumaini la kuonana karibuni. |

Mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga sentensi sahihi kudhahirisha iwapo wanaelewa maana ya maamkizi na baadhi ya njia za kuamkiana. Hatimaye, mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi katika madaftari yao kisha asahihishe na kuwaelekeza.

Hatua ya 4: Ufahamu

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma mifano ya maamkizi yaliyo mwanzoni mwa somo. Mwalimu atilie maanani kufahamu na kuelewa utamaduni unaoenda na maamkizi. Mfano; umri, nyakati, hali n.k. Pia atilie maanani haja ya wanafunzi ya kuelewa utaratibu wa kuamkiana.

Hatua ya 5: Sarufi

Mwalimu awaeleze wanafunzi kuwa lugha ya Kiswahili ina nafsi tatu:

Nafsi ya kwanza: Mimi

Nafsi ya pili: Wewe

Nafsi ya tatu: Yeye

Mwalimu awaongoze wanafunzi kufahamu kuwa nafsi huzungumzia mtu anayefanya kitendo.

ninakuamkia - Mimi + Wewe

unaniemkia - Wewe + Mimi

ananiemkia - Yeye + Mimi

Mwalimu awaongoze wanafunzi kutambua umoja na wingi wa nafsi na kuonyesha mabadiliko yanayotokea.

Mimi - Sisi : ninakuamkia - tunawaamkia

Wewe - Nyinyi : unaniemkia - mnatuamkia

Yeye - Wao : ananiemkia - wanatuamkia

Tazama:

ni – tu

u – m

a – wa

Mwalimu awahimize wanafunzi kuamkiana kama watu binafsi kisha katika kikundi. Hatimaye, awaongoze katika zoezi na kulikosoa. Awape wanafunzi mwongozo mwafaka. Abuni zoezi la ziada kwa wanafunzi wanyonge. Kwa mfano; kurudia igizo la kuamkiana.

Hatua ya 6: Tahajia na matamshi bora

Mwalimu aitumie nafasi hii kufundisha matamshi bora ya salamu za Kiswahili na uandishi kwa kutumia hati nzuri. Kwa mfano, kuandika maneno yenye sauti ambatano kama vile:

Shikamoo na sabalheri. Pia anaweza kutumia fursa hii kurudia msamiati wa maamkizi na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa kabisa.

Hatua ya 7: Hitimisho

Hi ni sehemu inayohitimisha maana ya mwalimu kuoanisha nafsi na maamkizi kwani huenda pamoja.

Mifano:

Hujambo Msafiri? (wewe)

Mimi sijambo Mutoni.

Msafiri: Mzazi mzima? (yeye)

Mutoni: Ni mzima.

Mwalimu abuni mazingira zaidi ya kuamkiana kama zoezi la ziada kwa wanafunzi hasa wanyonge. Kwa mfano: kuigiza maamkizi kati ya mwalimu na wanafunzi (mwanafunzi).

E. Zoezi la ziada

Ili kuwasaidia wanafunzi wa kiwango cha chini, mwalimu abuni njia ya kuwawezesha kuelewa maamkizi. Mfano ni kutazama upya michoro au picha, kuwaamkia wenzao

na pia wanaweza kufanya kuwa wahusika katika igizo la maamkizi wenyewe kisha mwalimu awaulize waeleze kile walichokifanya nao wajibu.

F. Tathmini

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili hadi watano ili waigize maamkizi. Kupitia hayo, atathmini iwapo wamefahamu maigizo au la. Pia, atathmini matumizi ya nafsi ya kwanza kwa kuwahimiza kuanza mazungumzo yao na:

Ninakuamkia – Mimi

Anakuamkia – Yeye

Unaniamkia – Wewe

Njia ya maswali na majibu pia itumiwe kabla ya kuwaambia wanafunzi wafanye zoezi la ziada ama maswali ya marudio kwa wanafunzi wenyе kiwango cha juu.

MAJIBU

Zoezi la 1, ukurasa 5

Mwalimu awape wanafunzi mwongozo wa kuigiza maamkizi mbalimbali.

Zoezi la 2, ukurasa 5

Majibu ni kama vile:

- Kuonyesha adabu njema
- Kuonyesha heshima
- Ni utamaduni
- Kuonyesha ujirani na uhusiano mwema
- Kuonyesha kwamba una mkabala mzuri na watu
- Ni ishara ya malezi mema
- Ni ishara ya uadilifu.

Zoezi la 1, ukurasa 6

1. Sijambo.
2. Marahaba.
3. Ya kuonana.
4. Njema/Nzuri
5. Asante.

Zoezi la 2, ukurasa 7

Mwalimu atathmini kazi za wanafunzi.

Zoezi, ukurasa 8

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

Zoezi la 1, ukurasa 10

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi wake. Kwa mfano:

1. Mimi sijambo - Sisi hatujambo
2. Kwaheri - kwaherini

Zoezi la 2, ukurasa 10 -11

- | | | | |
|--------------|--------------|--------------|-----------------|
| 1. Hatujambo | 2. Hawajambo | 3. Kwaherini | 4. M hali gani? |
| 5. Karibuni | | | |

Zoezi la 1, ukurasa 13

Mifano:

1. Njia, onja, kunja, vunja
2. Pweka, pwaguzi, kupwa, pwani
3. Nzi, kwanza, tanza, chenza
4. Swaga, sweta, guswa, poswa.
5. Mbolea, mbu, kumbukumbu, shamba.

Mwalimu atathmini majibu mengine ya wanafunzi.

Zoezi la 2, ukurasa 14

Mwalimu awape wanafunzi mwongozo wa kutumia kamusi ya Kiswahili ili kupata maana ya msamati mpya.

Zoezi la ziada, ukurasa 14

1. Salamu 2. Kwaheri 3. Shikamoo 4. Hujambo 5. Akheri

Aina mbalimbali za maamkizi

Muda: Vipindi 2

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, wanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi na ufasaha msamiati wa maamkizi.
- Kuamkiana kwa kutumia nafsi za lugha ya Kiswahili.

b) Vifaa vya kujifunzia

- Vinasa sauti
- Michoro na picha
- Watu binafsi (wanafunzi wenyewe)
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 15
- Magazeti
- Redio

c) Maandalizi ya somo

Kipindi hiki kinazungumzia aina ya maamkizi ambayo yanapatikana katika lugha ya Kiswahili. Ni muhimu kuwashirikisha wanafunzi ipasavyo hasa katika michoro au picha na maelezo katika utangulizi wa somo hili. Uigizaji na kuwasikiliza watu katika mazingira ya wanafunzi wakiamkiana ni muhimu sana. Ikiwa kuna wanafunzi wenge taathira ya kutoona, kutosikia na mengine, uigizaji ni muhimu kushirikishwa kupitia vitendo.

d) Utaratibu wa somo

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu aanze somo kwa kuauliza wanafunzi maswali ili kuwakumbusha somo lilopita. Wanafunzi nao wamjibu mwalimu. Kisha awaulize kuhusu picha na michoro

iliyo katika *Kitabu cha Wanafunzi*, ukurasa 15-17 nao wajibu. Mwalimu awaongoze kutambua kwamba maamkizi hayana vikwazo vya kijinsia, kidini, kitamaduni na kikabilo. Vikwazo hivyo viepukwe na wanafunzi wote washirikishwe katika somo hili. Wanafunzi wasome maelezo yaliyo chini ya picha na kujibu maamkizi.

Mifano: Habari — njema/nzuri

Shikamoo — Marahaba

Mwalimu afafanue ugumu wowote ambao wanafunzi wake wanakabiliana nao. Awapange katika makundi ili kuulizana na kujibizana kama hatua ya kumudu zoezi la kuamkiana.

Hatua ya 2: Aina mbalimbali za maamkizi

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma kwa sauti mifano ya msamiati wa maamkizi kwa njia ya kubadilishana. Kisha, awaelekeze kusoma kimya kimya ili kufanya msamiati huo na uzame ndani ya akili zao. Baadaye, awaongoze kuunakili msamiati huo katika madaftari yao. Wanakili maamkizi na majibu yake. Kisha mwalimu awapange wanafunzi katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili ili kuigiza aina mbalimbali za maamkizi. Mwalimu asahihishe matamshi na mawazo hasi kuhusu utamaduni wa kuamkiana.

Hatua ya 3: Msamiati wa maamkizi mbalimbali

Sehemu hii ni muhimu sana. Mwalimu aitumie kufafanua msamiati wa maamkizi na matumizi yake. Mfano ni: Kwa nini ni mdogo huamkia mkubwa kwa; ‘shikamoo tu?’ Mbona hatuwezi kujibu: ‘jambo?’ kwa, ‘sijambo?’ n.k.

Mwalimu awahimize wanafunzi kutunga sentensi sahihi kwa kutumia nafsi za Kiswahili.

Mifano: Mimi sijambo.

Wewe ni mzima?

Yeye hajambo?

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu zoezi la msamiati. Asahihishe na kuwapa wanafunzi mwelekeo mwafaka. Mwalimu abuni zoezi la ziada kwa wanafunzi wa

kiwango cha chini. Wanafunzi wa kiwango cha juu wanaweza kuongozwa kufanya maswali ya marudio.

Hatua ya 4: Mazungumzo yenyе maamkizi

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma kwa makini msamiati wa maamkizi katika mazungumzo. Wanafunzi wajibu maswali ya dodosa ya mwalimu na mwalimu afafanue masuala magumu ili kuhakikisha ya kwamba wanafunzi wanaelewa barabara. Hatimaye mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi na kujibu kwa usahihii.

Hatua ya 5: Sarufi

Mwalimu atumie nafasi hii kuwahimiza wanafunzi kutumia nafsi za Kiswahili katika sentensi sahihi na rahisi pale inapowezekana kwa kutumia msamiati wa maamkizi. Msisitizo uwe katika umoja na wingi wa nafsi tatu za lugha ya Kiswahili. Mwalimu atumie wakati huu kufafanua viambishi vya umoja na wingi wa nafsi hizi. Mifano:

Viwakilishi vya nafsi - umoja	Viwakilishi vya nafsi - wingi	Viambishi vya umoja	Viambishi vya wingi
mimi	sisi	ni	tu
wewe	nyinyi	u	m
yeye	wao	a	wa

Hatimaye mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga sentensi sahihi kwa kutumia nafsi za Kiswahili katika umoja na wingi. Mwalimu awakosoe wanapokosea. Mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi kuhusu nafsi za Kiswahili. Mifano:

Umoja	Wingi
Mimi ninaimba.	Sisi tunaimba.
Wewe unaimba.	Nyinyi mnaimba.
Yeye anaimba.	Wao wanaimba.

Hatua ya 6: Tahajia na matamshi bora

Mwalimu atumie sehemu hii kufundisha zaidi msamiati wa maamkizi na maneno ya adabu yanayoandamana na msamiati wa maamkizi. Mifano ya maneno ya adabu ni: pole, tafadhali, karibu, samahani, niwie radhi n.k. Salamu na utu huenda pamoja. Mwalimu atumie fursa hii kufundisha maadili ya upole na heshima kwa watu wote bila ubaguzi. Hatimaye mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi la kutamka na kuandika kwa hati nadhifu.

Hatua ya 7: Hitimisho

Hiit ni tamati ya somo la pili. Mwalimu aulize maswali na kupima majibu ya wanafunzi ili kutathmini iwapo dhana zote muhimu zimeeleweka. Dhana hizo ni:

- Maana ya maamkizi
- Aina za maamkizi
- Nafsi za lugha ya Kiswahili katika umoja na wingi

E. Mazoezi ya ziada

Hili linawalenga wanafunzi wa kiwango cha chini ili wazame kwenye somo na kuwafikia wenzao. Mwalimu atumie vifaa dhahiri kama vile kuwatumia wanafunzi wenyewe kushiriki katika zoezi la kuamkiana. Pia mwalimu atumie imla na maswali ya kushtukiza.

F. Tathmini

- Mwalimu atumie maswali ya kushtukiza
- Mwalimu atumie imla
- Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuigiza zoezi la kuamkiana tena na mazungumzo.

MAJIBU

Zoezi la I, ukurasa 20

1. Tunayo
2. Pole
3. Hongera
4. Buriani dawa
5. Shikamoo

Zoezi la 2, ukurasa 20 - 21

1. Vyema / salama 2. Karibu 3. Asante 4. Salmini 5. Ya
kuonana

Zoezi la makundi, ukurasa 22

Mwalimu awape wanafunzi mwongozo wa kuigiza maamkizi mbalimbali.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 22

1. Daktari 2. Shikamoo 3. Anaugua 4. Pole 5. Kuonyesha upole

Zoezi la ziada, ukurasa 22

Mwalimu awape wanafunzi mwongozo wa kuigiza maamkizi mbalimbali.

Zoezi la I, ukurasa 25-26

1. a) Mimi – sisi
b) Wewe – nyinyi
c) Yeye – wao
2. Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi.

Somo la 3

Matumizi ya nafsi na viwakilishi vya nafsi katika maamkizi

Muda: Vipindi 2

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa makini, ufasaha na usahihi: silabi, maneno na sentensi.
- Kutaja msamiati wa maamkizi katika umoja na wingi.
- Kutumia nafsi za Kiswahili katika umoja na wingi kikamilifu.

b) Vifaa vya kujifunzia

- Vinasa sauti
- Mabango
- Michoro na picha
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 27
- Magazeti

c) Maandalizi ya somo

Hili ni somo la mwisho katika mfululizo wa maamkizi na nafsi za Kiswahili. Ni wakati muhimu wa kutathmini iwapo malengo yaliafikiwa ama la na iwapo somo limeeleweka barabara. Mwalimu awape wanafunzi maswali ya marudio kwa wingi na pia kuauliza maswali ya dodosi ili kutathmini uelewa wao. Mwalimu ashirikishe vifaa vingi na wanafunzi wote bila kubagua jinsia, dini ama tabaka pamoja na taathira za kuona, kusikia ama kutumia viungo fulani vya mwili.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufasiri michoro na pia kunakili mifano na maelezo muhimu katika madaftari yao. Pia awaongoze wanafunzi kuigiza wahusika mbalimbali katika mazingira ya maamkizi katika umoja na wingi.

d) Utaratibu wa somo

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuwaauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali yake. Mwalimu asisimue wanafunzi wake kwa kutumia picha na michoro iliyo katika *Kitabu cha Wanafunzi*, ukurasa 23. Wanafunzi waeleze wanachokiona na kujibu. Mwalimu anukuu maelezo yao ubaoni. Mwalimu awaongoze kuandika kwenye madaftari yao mifano mwafaka. Katika hatua hii, ni muhimu kuwashirikisha wanafunzi wote walioko darasani hata walemavu. Wale wenye taathira ya kuona mbali waketi katika madawati ya mbele kabisa. Mwalimu afafanue vigezo vya kugeuza maamkizi katika umoja na wingi na mabadiliko yanayotokea.

Mfano:

Jambo	–	Jambo
Hujambo	–	Hamjambo
Sijambo	–	Hatujambo

Hatua ya 2: Kusikiliza na kuzungumza

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa mara nyingine kwenye michoro na picha pamoja na vifungu vya maamkizi vilivyo katika ufunguzi wa somo hili. Mwalimu aulize maswali ya kufuatisha ili wanafunzi watoe maelezo ya kina. Mwalimu awapange wanafunzi kwenye makundi; mmoja awaamkie na wenzake wajibu kwa wingi. Hali hii inaweza kurudiwa zaidi ya mara moja hadi wanafunzi wote wafahamu namna maamkizi katika umoja na wingi yanavyobadilika. Hatimaye wanafunzi wafanye igizo la kuamkiana na kunakili majibu kwenye madaftari yao.

Hatua ya 3: Msamiati wa viwakilishi vya nafsi

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la msamiati. Wanafunzi wanaweza kupangwa katika makundi na kuulizwa kujibu katika makundi yao. Baadhi wataje msamiati wa maamkizi kwenye umoja na wenzao wakijibu kwa wingi. Hili ni zoezi muhimu katika kumudu umoja na wingi wa maamkizi. Pia ni zoezi zuri la kutumia nafsi za kiswahili katika umoja na wingi. Mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika mifano katika madaftari yao. Mwalimu akosoe kazi ya wanafunzi na kuwapa mwongozo ufaao.

Hatua ya 4: Ufahamu

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma tena mifano ya maamkizi katika umoja na wingi kabla ya kuwaongoza kufanya zoezi. Mwalimu ajibu maswali ya wanafunzi na pia

kuhimiza mbinu bora za kusoma ufahamu. Mwalimu atumie mbinu kama vile:

- Kusoma kwa sauti
- Kusoma kwa zamu
- Kusoma kimya kimya

Mwalimu akosoe majibu ya wanafunzi. Ashirikishe wanafunzi wote bila kubagua.

Hatua ya 5: Sarufi

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali na kuwataka wajieleze kwa kutumia nafsi za lugha ya Kiswahili katika umoja na wingi. Mwalimu awahimize wanafunzi kutunga sentensi rahisi naye akadirie usahihi wake na kutoa mwongozo bora. Hatimaye mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya mazoezi yote ya sarufi. Mwalimu asahihishe na kutoa ushauri kwa wanafunzi. Mwalimu atumie mazoezi ya ziada kuwakuzwanafunzi wenyewe kiwango cha chini.

Hatua ya 6: Tahajia na matamshi bora

Mwalimu atumie fursa hii kutathmini kuimari kwa kiwango cha matamshi na mwandiko wa wanafunzi wake. Mwalimu awaongoze wanafunzi wake kunakili msamiati muhimu kwenye madaftari yao kwa kushiriki zoezi la imla mbali na yaliyopendekezwa kwenye *Kitabu cha Wanafunzi*.

Hatua ya 7: Hitimisho

Hili ni somo la mwisho kwenye somo hili linalohusu msamiati wa maamkizi na nafsi za Kiswahili. Mwalimu ahitimishe somo kwa kuuliza maswali kadhaa na kutaka wanafunzi wake kujibu kulingana na alivyouliza. Mwalimu athibitishe iwapo wanaweza kutaja msamiati wa maamkizi na maneno ya adabu katika umoja na wingi. Atumie maswali ya kutathmini malengo ya kujifunza.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya mazoezi na hata kazi ya ziada ili kumudu somo hili barabara. Wale wa kiwango cha juu, wahimizwe kufanya maswali ya marudio.

E. Mazoezi ya ziada

Mazoezi haya yanalenga kuwasaidia wanafunzi ambao ni wa kiwango cha chini. Mwalimu atumie mazoezi mengi yaliyopendekezwa na waandishi kuhakikisha zoezi hili linafaalu. **Kwa mfano:** Kutunga sentensi sahihi zenye viwakilishi vya nafsi katika umoja na wingi.

F.Tathmini

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti tofauti kwa kurejelea mabango, michoro na picha pamoja na wanafunzi wenyewe na kutathmini majibu yao. Awaongoze kujua umuhimu wa kushirikiana, kupendana na kuthaminiana huku wakionyesha adabu, heshima na upendo kwa wenzao. Mbinu kama imla inaweza kutumiwa na mwalimu kuwatathmini wanafunzi.

MAJIBU

Zoezi la 1, ukurasa 28

1. Unanikumbuka
2. Yeye
3. Nyinyi
4. Wao
5. Sisi

Zoezi la 2, ukurasa 29

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Kwa mfano:

- | | |
|---------------------|-----------------------|
| 1. Mimi ninalima. | - Sisi tunalima. |
| 2. Wewe ni mkulima. | - Nyinyi ni wakulima. |
| 2. Yeye ni dereva. | - Wao ni madereva. |

Zoezi la ziada, ukurasa 29

1. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.
2. Sijambo
3. a) Ndio
b) Ndio
c) (Sisi, Nyinyi, Wao)
4. Yetu
5. Sisi - Mimi
Nyinyi - Wewe
Wao - Yeye

Zoezi la 1, ukurasa 30-31

1. Yeye 2. sisi 3. wao 4. wewe 5. nyinyi

Zoezi la 2, ukurasa 31

1. Sisi 2. wao 3. nyinyi 4. wewe 5. mimi

Zoezi la mjadala, ukurasa 31

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika namna ya kushiriki katika mjadala husika.

Zoezi la imla, ukurasa 32

Mwalimu awasomee wanafunzi maneno yafuatayo ili wayaandike katika madaftari yao:

1. Karne
2. Katiba
3. Bilauri
4. Bendera
5. Pakua

Maswali ya marudio, ukurasa 32 - 33

1 a) U mzima? b) U hali gani? c) Hujambo? d) Hajambo?

2. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

3. a) Majaliwa b) Buriani dawa c) Nawe pia d) Binuru

4. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. Kwa mfano:

Shikamoo/ naomba/ samahani/ pole/ mzima

5. Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi.

6. a) tu b) u c) m d) a e) wa

MADA KUU: MATUMIZIYA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI

Mada Ndogo: Msamiati wa mazingira ya shule

Idadi ya vipindi: 10

Ujuzi upatikanao katika mada hii:

- Kusikiliza kwa makini
- Kusoma vifungu vya habari na kutumia msamiati muhimu katika mazingira ya shule kwa kuzingatia wakati uliopo

Uhusiano wake na masomo mengine:

- *Jiografia* kwa kuonyesha ramani ya mazingira ya shule.
- *Historia* kwa kuhakikisha maelezo ya wakati wa kuanzishwa kwa shule.
- *Mafunzo ya jumla* kwa kuzungumzia umoja na mshikamano unaopaswa kumudu shulenii kati ya wanafunzi na walimu na vilevile nyumbani kati ya wazazi na watoto.

Vifaa vya kujifunzia:

- Vinasa sauti
- Ramani ya Rwanda inayoonyesha mazingira
- Michoro ya vifaa tofauti ndani ya darasa
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 36
- Picha ya mwalimu mbele ya wanafunzi darasani
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum kwa kuwa ni vigumu kwao kuelewa.

Kigezo cha tathmini na upimaji:

- Uwezo wa kutamka bila kusita jina la shule na mazingira yake pamoja na kutaja mojawapo ya vifaa vinavyopatikana shulenii au darasani.

Maelezo kwa mwalimu:

a) Utangulizi wa mada

Mada hii inashughulikia msamiati wa mazingira ya shule. Kwa hivyo, majina ya vifaa mbalimbali, majina ya viongozi na watu wengine wapatikanao katika mazingira ya shule, vitendo tofauti vinavyohusu mazingira ya shule, majina ya kazi zinazofanywa na watu mbalimbali waliosomea katika shule, yamezungumziwa katika mada hii. Mbali na hayo, mada hii imegusia pia matumizi ya wakati uliopo, tungo yakinishi na tungo kanushi.

Dhana muhimu zinazojitokeza katika mada hii ni pamoja na *vifaa mbalimbali* vya *darasani, ratiba ya siku na wiki, usafi shulenii, adabu shulenii, sarufi, sentensi, viongozi shulenii, wakati uliopo, tungo yakinishi na tungo kanushi*.

b) Masuala mtambuka

- Amani na maadili
- Usawa wa kijinsia
- Elimu ya pamoja
- Mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo
- Utamaduni wa kiusanifishaji
- Masomo ya ujinsia na uzazi

c) Ujuzi wa jumla

- Usuluhishaji wa matatizo
- Mawasiliano kwa lugha rasmi
- Stadi za utafiti
- Ubunifu na ugunduzi
- Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha
- Ujifunzaji wa muda mrefu

Somo la Kwanza

Mazungumzo shuleni

Muda: Vipindi 2

a) **Malengo ya somo**

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha mazungumzo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi.
- Kutaja majina ya vifaa mbalimbali vипатиканавоуо дарасанi.
- Kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati wa mazingira ya shule.

b) **Vifaa vya kujifunzia**

- Vinasa sauti
- Michoro ya vifaa tofauti ndani ya darasa
- Vifaa vya shule kama vile vitabu, madaftari, penseli, kitit cha mwalimu, meza, kalamu, kifutio, kabati la vitabu, rula, kifutio, ubao, chaki na saa
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 37
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu

c) **Maandalizi ya somo**

Hili ni somo la kwanza katika msamiati wa mazingira ya shule na linahusu mazungumzo shuleni kati ya wanafunzi na mwalimu. Kwa kuwa wanafunzi hawa hawajakuwa na msamiati mwingi katika Kiswahili, ni vizuri mwalimu aweze kutumia sehemu za mwili kama nyenzo muhimu kumwelekeza mwanafunzi kutambua maana ya kile kinachozungumziwa. Kwa hivyo, atumie uso, mikono na sehemu nyingine za mwili ili kutoa maelezo ya kuwarahisishia wanafunzi uelewa. Mwalimu ahakikishe pia kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi

hasa wale wa kiwango cha chini katika ujifunzaji. Vilevile, ni vyema mwalimu azingatie wakati unaofaa wa kuonyesha vifaa hivyo hadharani ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwu katika muda unaotakikana. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu atumie vifaa hivyo kwa kuwaomba wao wenyewe kuvigusa huku wakitaja majina ya vifaa hivyo. Katika somo hili, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli inayohusika darasani.

d) **Utaratibu wa somo**

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu awaamkle wanafunzi wake na kuwaauliza maswali kuhusu somo lililopita na wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awachangamshe wanafunzi wake kwa kuwaauliza maswali kuhusu picha na michoro iliyoko katika *Kitabu cha Wanafunzi*, ukurasa 37.

Kwa mfano:

- Mnaona nini kwenye picha hizi?

Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile: "*Mimi ninaona meza.*" Ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kupata ujuzi kuhusu ubunifu na ugunduzi, tafakuri tanduizi kwa kusisitiza uchunguzi wa picha ili wanafunzi watambue usawa wa kijinsia kutokana na picha za wanafunzi zinazoonyesha wasichana na wavulana wote wakiwa darasani. Vilevile, masuala ya elimu ya pamoja yasisitizwe pale ambapo miongoni mwa wanafunzi kuna wale wenyе ulemavu na ambao wanajifunza pamoja na wengine. Kwa hivyo, wanafunzi watazame picha walizoonyeshwa na mwalimu wao na kujibu maswali waliyoulizwa. Kwa mfano: *Mimi ninaona kabati, mimi ninaona kiti*, na kadhalika.

Hatua ya 2: Kusoma na ufahamu - Mazungumzo kati ya wanafunzi na mwalimu

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha mazungumzo kinachohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Hivyo basi, wanafunzi wasome kwa kimya pamoja na kuandika msamiati huo mpya kwenye madaftari yao. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wamesoma kwa kimya kama inavyotakikana, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu cha mazungumzo mara tu wanafunzi wanapomaliza kusoma. Kwa mfano, anaweza kuwaauliza swali lifuatalo: *Ni watu gani wanaozungumza katika kifungu hiki?* Wanafunzi kwa upande wao, wajibu

maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hicho. Kwa mfano: *Mazungumzo yanafanyika kati ya wanafunzi na mwalimu*. Baada ya kupata picha ya uelewa wa jumla wa wanafunzi kuhusu kifungu kinachoohusika, mwalimu awaulize wanafunzi kusoma kwa sauti mazungumzo hayo kati ya mwalimu na wanafunzi mmoja baada ya mwingine. Katika hatua hii, ni lazima mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

Hatua ya 3 : Ujifunzaji wa msamiati wa mazingira ya shulen

Mwalimu awaambie wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujadiliana kwanza kuhusu maana za msamiati mpya waliokutana nao. Wanafunzi wajadiliane kuhusu maana za msamiati huo kwa kuzingatia matumizi yake katika kifungu cha mazungumzo kinachoohusika. Watumie kamusi pale panapohitajika. Kwa hivyo, mwalimu azunguke darasani kutoa maelekezo pale yanapohitajika. Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu zoezi la kwanza la msamiati na kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa zoezi hilo. Hivyo basi, wanafunzi, katika makundi yao ya wanafunzi watatu watatu, wajadiliane kuhusu zoezi hilo la msamiati huku mwalimu akizunguka darasani kuelekeza wale wanaotatizika. Baada ya kujibu maswali yaliyotolewa kuhusu zoezi hili, mwalimu ashirikishe wanafunzi wote kujibu maswali hayo. Kwa hivyo, mwalimu achukue fursa kwa kutumia vifaa alivyovileta kuhusiana na mazingira ya shule ili kurahisisha uelewa wa wanafunzi.

Kuhusu zoezi la pili la msamiati, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujipanga katika makundi ya wanafunzi wawili ili wajadiliane kuhusu maana za msamiati unaotakiwa kujazwa katika mapengo yaliyoachwa. Ni vyema mwalimu awaambie wanafunzi warejelee matumizi ya msamiati husika katika kifungu cha mazungumzo walichokisoma. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kujibu maswali ya mazoezi hayo. Wakati wa kujibu mazoezi haya, mwalimu arejelee pia mifano mingine inayoweza kusaidia wanafunzi kupata stadi za utafiti, utawala binafsi na stadi za maisha. Kwa mfano, anaweza kuwachochea wanafunzi kuchunguza na kufikiri kuhusu umuhimu wa vifaa vilivyopo na namna ya kutunza vifaa hivyo vyta shule, mienendo mizuri inayomtambulisha mwanafunzi mwenye adabu kwa kuzingatia maana za baadhi ya maneno yaliyopendekezwa kama vile: *adabu, kutunza, samahani, na kadhalika*.

Hatua ya 4 : Ratiba ya mwanafunzi ya siku na wiki nzima

Katika sehemu hii, mwalimu awaombe wanafunzi kujipanga katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili kujadiliana kuhusu kile kinachoendelea katika picha zilizo katika vitabu vyao. Baadaye, kila kundi lisome sentensi zilizotolewa na kuzihusisha na picha hizo huku wakielekezwa na mwalimu wao. Kwa kuzingatia maelezo ya picha

hizo, mwalimu awaelekeze wanafunzi hawa kujadiliana kuhusu ratiba yao kuanzia wanapoamka hadi wanapofika shulen. Katika zoezi hili, mwalimu achague mwanafunzi mmoja katika kila kikundi na kumwomba aeleezee wenzake ratiba yake kama njia ya kuwasaidia kupata ujuzi kuhusu namna ya kuwasiliana katika lugha rasmi.

Hatua ya 5: Kusikiliza na kuzungumza - Maigizo

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi katika kifungu cha mazungumzo kinachohusika. Baadaye, mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watano watano ambapo mwanafunzi wa kwanza atachukua nafasi ya Mutoni, wa pili achukue nafasi ya Musafiri, wa tatu naye nafasi ya mwalimu na wanafunzi wengine wawili watajumuika nao katika nafasi ya wanafunzi. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi hawa kujitokeza mbele ya darasa na kuigiza mazungumzo kati ya mwalimu na wanafunzi. Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi mara tu yanapojitokeza ili kuwazo esha wanafunzi wake kutamka kwa usahihi herufi, silabi, maneno na sentensi za Kiswahili.

Hatua ya 6: Ufahamu

Katika hatua hii ya ufahamu, mwalimu awaelekeze tena wanafunzi kusoma kwa makini na kwa kimya kifungu cha mazungumzo kati ya mwalimu na wanafunzi huku wakijibu maswali yaliyotolewa kama maswali ya ufahamu. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitoa maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

Hatua ya 7: Hitimisho

Katika hatua hii ya mwisho wa somo hili, mwalimu ahitimishe somo kwa kuuliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza ili kutambua ikiwa wanaweza kutaja vifaa mbalimbali vinavyopatikana katika mazingira ya darasani na maswali mengine yanayolenga kutathmini malengo ya ujifunzaji. Ili kusaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi wake katika namna ya kujibu zoezi la tatu la msamiati na kuwaomba walifanye kama kazi mradi; yaani kazi ya nje ya darasa. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza somo la pili la mada hii ya msamiati wa mazingira ya shule.

Mazoezi ya ziada

Ili kuwasaidia wanafunzi wa kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaelekeze wanafunzi hao dhaifu kutazama darasa lao na kutunga sentensi zao kwa kutumia vifaa vilivyopo humo. Mwalimu awape mfano wa sentensi na kuwaelekeza

kuhusu kile wanachotakiwa kufanya.

Swali: *Tazama darasa lako, kisha, tunga sentensi tano kwa kuanza na “**Mimi ninaona ...**”*

Kwa mfano: *Mimi ninaona ubao katika darasa langu.*

e) **Tathmini**

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kurejelea vifaa alivyovileta darasani na picha zilizotumiwa kujifunzia somo hili ili kutathmini ikiwa wanafunzi wameelewa. Vilevile, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kwa kuchunguza ikiwa wanafunzi wametambua umuhimu wa kutunza vifaa vyao vya shule na kuheshimu watu wengine wanaojitokeza katika mazingira ya shule. Kunyosha mkono kila wakati mwanafunzi anapotaka kuuliza au kujibu swali, kutumia ipasavyo neno *samahani* ni baadhi ya matendo ya kuonyesha mienendo ya kuwa na adabu shulenii au darasani.

Zoezi la ufhamu, ukurasa 39

1. Musafiri amefanya **zoezi** la Kiswahili.
2. Swali la kwanza ni **gumu** kwa Musafiri.
3. Swali la kwanza ni **rahisi** kwa Mutoni.
4. Mwalimu huwapa wanafunzi **kazi ya nyumbani** kila siku.
5. Mutoni na Musafiri wanaenda haraka kwa sababu **kengele** inalia.
6. Wanafunzi **hawajambo**.
7. Daftari la Mutoni **limeharibika**.
8. Mutoni **amenyeshewa** na mvua.
9. Wanafunzi wanaweka vitabu na madaftari katika madawati yao. Sasa ni wakati wa kufanya **jaribio**.
10. Kila mwanafunzi anachagua **jibu** sahihi.

Zoezi la 1, ukurasa 39 - 40

Mwalimu ahakikishe wanafunzi wote wanashirikishwa katika usomaji wa sentensi zilizo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 40-41.

Zoezi la 2, ukurasa 40

1. Kiswahili ni somo **muhimu** kwa wanafunzi.
2. Mwalimu anauliza swali **gumu** kwa wanafunzi.

3. Mwalimu anaandika **ubaoni**.
4. **Kiti** cha mwalimu kiko mbele ya darasa.
5. Wanafunzi wanaweka vitabu katika **madawati** yao.
6. Mimi **ninatunza** vizuri vifaa nya shule; vitabu, madafrari na kalamu.
7. Mutesi ameharibu daftari lake. Mwalimu atampatia **adhabu**.
8. Sisi tumeshinda **somo** la Kiswahili.
9. **Samahani !** Mwalimu. Ninaomba ruhusa ya kuenda haja.
10. Mwalimu **anatupenda** sana kwa sababu tunasoma vizuri.

Zoezi la 3, ukurasa 41

1 E

2 F

3 A

4 B

5 K

6 C

7 I

8 D

9 H

10 J

11 G

Zoezi, ukurasa 43

Mwalimu amshirikishe kila mwanafunzi katika kueleza shughuli zao kuanzia kuamka asubuhi hadi kufika darasani na kurudi nyumbani jioni.

Zifuatazo ni baadhi ya shughuli zinazoweza kuzungumziwa na wanafunzi:

- Kuamka
- Kuoga, kupiga mswaki, kupiga sulu viatu

- Kupata kifungua kinywa au chai kwa mkate
- Kuvaasare
- Kuchukua vitabu na madaftari
- Kuanza safari kuelekea shuleni au kuingia darasani
- Kufika shuleni na kufanya marudio au mazoezi
- Kuanza masomo

Zoezi la ufahamu, ukurasa 44-45

1. Shule ya Bwiza
2. Kidato cha kwanza
3. Gasimba husali, kisha huenda bafuni kokuga. Baadaye yeye hupiga meno mswaki, huchana nywele na kuvaasare yake.
4. Mamake Gasimba
5. Gasimba huanza kusoma vitabu vyake.
6. Mkuu wa shule
7. Alhamisi jioni wao hufanya mazoezi ya kuogelea. Ijumaa jioni wao hushiriki katika mjadala.
8. Yeye humsaidia mamake kufanya kazi za nyumbani.
9. Gasimba hehudhuria ibada kanisani. Baadaye yeye hupumzika kisha hujitayarisha kwa ajili ya kwenda shule Jumamatu.
10. a) Chakula cha kwanza cha asubuhi kabla ya kuanza shughuli zozote za siku.
b) Mavazi yanayofanana ambayo huvaliwa na kundi la watu kama vile wanafunzi.
c) Mazungumzo ya kutoa hoja za kupinga au kutetea mada fulani.
d) Mchezo wa mpira wa miguu.

Mazungumzo kati ya wanafunzi

Muda: Vipindi 2

a) **Malengo ya somo**

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha mazungumzo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi.
- Kutaja majina ya masomo na kutambua vitendo mbalimbali kuhusiana na mazingira ya shule.
- Kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati wa mazingira ya shule.
- Kubainisha kiambishi cha wakati uliopo.
- Tingo yakinishi.

b) **Vifaa vya kujifunzia**

- Vinasa sauti
- Michoro ya vifaa tofauti ndani ya darasa
- Vifaa vya shule kama vile: mpira wa kucheza kandanda, mpira wa kikapu na mpira wa mikono
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 46
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu.

c) **Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu mazungumzo kati ya wanafunzi na lina vipindi viwili. Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kujifunzia somo hili kama vilivyobainishwa hapo juu. Katika kulipitia somo zima, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wake wanatoka nje ya darasa lao na kutumia uwanja wa michezo ili kupata uelewa zaidi kuhusu michezo ya aina mbalimbali na kufahamu mambo mengine muhimu yanayozungumziwa katika

kifungu walichokisoma. Vilevile, ni vyema mwalimu azingatie kwamba wakati uliopo ndio wakati msingi ambao unatakiwa kutumiwa kama kirejeleo cha kutambua nyakati nyingine zinazotumiwa katika mawasiliano. Kwa hivyo, mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ipasavyo katika ujifunzaji wa viambishi yya wakati uliopo kwa kuzingatia nafsi tofauti za Kiswahili. Mwalimu awaelekeze kwanza wanafunzi katika ujifunzaji wa wakati ulipo katika tungo yakinishi ili baadaye, katika somo jingine, waweze kuendelea na wakati ulipo katika tungo kanushi bila kuchanganya viambishi vilivyopo. Hali hii ndiyo itasaidia pia wanafunzi kutambua kwa njia rahisi sifa za wakati uliopo katika tungo yakinishi na kuzitofautisha na zile za tungo kanushi. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

d) **Utaratibu wa somo**

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kusahihisha zoezi walilopewa kama kazi mradi. Baadaye, aendelee na somo kwa kuchangamsha wanafunzi wake kwa kuauliza maswali kuhusu picha na michoro iliyoko katika *Kitabu cha Wanafunzi*, ukurasa 46. Kwa mfano: ‘*Mnaona nini kwenye picha hizi?*’ Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu swali waliloulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama; “*mimi ninaona...*” Baadaye, mwalimu aendelee na somo kwa kuauliza kile kinachofanywa na wanafunzi wanaojitokeza katika picha husika. Kwa mfano, anaweza kuuliza: “*Wanafunzi wanafanya nini katika picha hii?*” Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao. Kwa mfano: ‘*Wanafunzi wanacheza.*’ Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha picha zilizopo huku wanafunzi nao wakifiki na kubaini kinachoendelea katika picha hizo. Kwa hivyo, nafasi ya msichana katika michezo tofauti, masuala ya elimu ya pamoja kuititia michoro ya walemvu wanaoshirikishwa katika michezo ya aina tofauti itumiwe kama njia nzuri ya kufikia ujuzi huo ainasafu.

Hatua ya 2: Kusoma na ufhamu

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha mazungumzo kinachohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Wanafunzi nao wasome kwa kimya huku wakiandika msamiati huo mpya. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu cha mazungumzo walichokisoma ili

kuhakikisha ikiwa wamesoma na kuelewa. Kwa mfano, anaweza kuuliza swali lifuatalo: ‘*Mazungumzo haya yanafanyika kati ya nani?*’ Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale walioyasoma katika kifungu hicho. Kwa mfano: ‘*Mazungumzo yanafanyika kati ya wanafunzi.*’ Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu kilichopo, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa sauti kifungu hicho cha mazungumzo kwa kuhakikisha kuwa wanasoma kwa namna inayofaa. Kwa hivyo, mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

Hatua ya 3: Ujifunzaji wa msamiati

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba watafute maana za msamiati mpya kufuatana na jinsi ulivytumiwa katika kifungu cha mazungumzo walichokisoma. Mwalimu awaombe wanafunzi kutumia kamusi pale wanapohitaji na azunguke darasani kuelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi hiyo. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma sentensi walizopewa na kujadiliana kuhusu maana za msamiati uliopigiwa mistari huku wakitunga sentensi zao wenyewe. Ni vyema mwalimu azunguke pia darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe kusahihisha kwa pamoja zoezi hilo la msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliopo na ambao ulikuwa mpya kwao, mwalimu achukue fursa hii kwa kuuliza ikiwa kuna msamiati ambao hawajaelewa ili maana yake ijadiliwe kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika kifungu cha mazungumzo kilichopo. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio unaomwonyesha ikiwa wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, usuluhisho wa matatizo na mawasiliano katika lugha rasmi. Kwa hivyo, kupitia mifano ya sentensi zilizotolewa, mwalimu awaelekeze wanafunzi kupata maana yake ili waweze kutunga sentensi zao wenyewe.

Hatua ya 4: Ujifunzaji wa sarufi (wakati uliopo)

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma sentensi zilizopo kwa kutilia mkazo nafsi, viambishi vyake na kiambishi cha wakati ***na*** ili waweze kutunga sentensi zenye kulenga mawasiliano katika lugha rasmi. Katika zoezi la kwanza la sarufi, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika matumizi sahihi ya vitenzi vilivyopendekezwa yaani; ***cheza na soma.*** Kutokana na majibu yalijotolewa na wanafunzi kwa kutumia vitenzi hivi, mwalimu awaombe wanafunzi wake kutafakari kuhusu muundo wa vitenzi katika wakati uliopo, tungo yakinishi. Kwa hivyo, awaelekeze wanafunzi kutambua viambishi

nafsi, kiambishi cha wakati uliopo ‘na’ na sehemu ya kitenzi inayorudiwarudiwa yaani; soma na cheza, huku akitoa mifano mingine ya vitenzi.

Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufanya zoezi la pili la sarufi ambapo wanafunzi wanahitajika kukamilisha tungo walizopewa kwa kutumia nafsi inayofaa baada ya kutambua kiambishi nafsi kilichotumiwa katika tungo hizo. Wanafunzi wazingatie maelekezo waliyopewa na mwalimu wao na kufanya zoezi hilo na kulisahihisha kwa pamoja mara tu wanapomaliza. Mwalimu achunguze ikiwa wanafunzi wote wameelewa ili awaombe kuendelea na zoezi la tatu la sehemu hii ya sarufi.

Zoezi la tatu la sarufi linafanywa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili. Kwa hivyo, wanafunzi waelekezwe kuhusu jinsi watakavyojadiliana katika makundi yao na kutambua sifa za umaja na wingi wa tungo. Mkazo utiliwe kuhusu jinsi ya kubadilisha nafsi kutoka nafsi za umaja hadi nafsi za wingi, kubadilisha viambishi nafsi kutoka viambishi vya umaja hadi viambishi vya wingi au kinyume cha hayo. Katika hatua hii, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wote wameshirikishwa kusahihisha mazoezi yaliyopo kwa kuwachochea kupata ujuzi ainasafu kama vile tafakuri tanduizi ambapo anaweza kuwaomba wanafunzi wengine kuchunguza majibu yanayotolewa na wenzao, suluhisho la matatizo ambapo anawaomba wanafunzi kutoa suluhisho la matatizo ya wenzao, mawasiliano katika lugha rasmi kwa kuwaelekeza wanafunzi kusahihisha makosa yao na ya wenzao na stadi za utafiti ambapo anaomba wanafunzi kutambua makosa ya wenzao na kuyasahihisha.

Hatua ya 5: Kusikiliza na kuzungumza

Hatua hii ya tano inahusu kusikiliza na kuzungumza. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi kifungu cha mazungumzo kinachohusika. Baada ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wameshazoea kusoma kama inavyotakikana, mwalimu awaombe wanafunzi kufunga vitabu vyao. Mwalimu aendelee kwa kuwasomea wanafuni maneno na vifungu vya maneno vifuatavyo ili waviandike katika madaftari yao.

unaumwa, unadanganya, njoo hapa, anaomba ruhusa, anapiga kelele, pole sana, twende kujunga na wenzetu, mnapenda somo la Kiswahili, pia.

Katika zoezi hili la imla, mwalimu azingatie kwamba maneno yaliyopo yana utata kwa wanafunzi pale ambapo baadhi yake yana silabi ambazo wanafunzi hawajazizoea katika lugha yao ya mama kama vile mfuatano wa irabu mbili ambazo zinajitokeza

katika silabi tofauti na matumizi ya sauti *I* na *r* ambazo ni fonimu tofauti katika lugha ya Kiswahili. Hali hii ichochee wanafunzi kutafiti kuhusu maneno mengine yenye na sifa hizo katika lugha ya Kiswahili kama njia ya ujifunzaji wa kudumu kwa wanafunzi pale wanapoweza kutumia maneno hayo katika mawasiliano yao na watu wengine bila tatizo lolote.

Hatua ya 6: Ufahamu

Katika hatua hii ya ufahamu, mwalimu awaombe tena wanafunzi kusoma kwa makini na kwa kimya kifungu cha mazungumzo kati ya wanafunzi na mwalimu huku wakijibu maswali yaliyotolewa kama maswali ya ufahamu. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitoa maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

Hatua ya 7: Hitimisho

Katika hatua hii ya mwisho wa somo hili, mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyofunza. Maswali hayo yaegemei hasa katika kuchunguza ikiwa wanaweza kutaja majina ya masomo wanayojifunza na kutumia msamiati waliojifunza, kutambua viambishi nafsi na kiambishi cha wakati uliopo katika tungo yakinishi. Ili kusaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi wake katika namna ya kujibu zoezi la nne la sehemu ya sarufi na kuwaomba walifanye kama kazi mradi; yaani kazi ya nje ya darasa. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza kwa somo la tatu la mada hii ya ‘msamiati wa mazingira ya shule’.

e) **Mazoezi ya ziada**

Mwalimu atoe zoezi la ziada ambalo linalenga kuwaboresha wanafunzi wa kiwango cha chini wasioweza kuelewa haraka kama wenzao.

1. Soma tena kifungu cha mazungumzo kati ya Kalisa, Mutoni na Birasa, kisha andika nafsi na vitenzi viliyyotumiwa katika wakati uliopo. Piga mstari chini ya nafsi, kiambishi nafsi na kiambishi wakati uliopo.

Kwa mfano: Mimi ninapenda mchezo wa kandanda.

2.Tunga sentensi zako katika nafsi zote sita (umoja na wingi) kwa kutumia vitenzi katika wakati uliopo. Piga mstari chini ya kila nafsi, kiambishi nafsi na kiambishi cha wakati uliopo.

Kwa mfano: Sisi tunakimbia haraka.

f) **Tathmini**

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kuchunguza ikiwa wanaweza kurejelea majina ya masomo wanayojifunza, vitendo mbalimbali vinavyohusiana na mazingira ya shule na hata vifaa vingine alivyovileta darasani pamoja na kueleza kile kinachoendelea katika picha zilizotumiwa kujifunzia somo hili ili kutathmini ikiwa wanafunzi wameelewa. Vilevile, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kwa kuchunguza ikiwa wanafunzi wametambua umuhimu wa kutumia maneno ya adabu na heshima kama vile: *pole, kuomba ruhusa, n.k.* Maswali mengine yalenge kutathmini kiwango cha uelewa wa wanafunzi kuhusu utambuzi wa nafsi za umoja na wingi, viambishi nafsi na kiambishi cha wakati uliopo, tungo yakinishi.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 48

1. Kalisa anapenda mchezo wa kandanda.
2. Mutoni anapenda mchezo wa voliboli.
3. Birasa anapenda mchezo wa voliboli.
4. Hapana. Birasa anapenda mchezo wa voliboli.
5. Wanafunzi wanaopenda mchezo wa voliboli ni Mutoni na Birasa.
6. Muhire hupiga kelele darasani.
7. Mwalimu wa zamu amesimama karibu na uwanja wa kuchezza kandanda.
8. Birasa anataka kuomba ruhusa ya kupumzika bwenini.
9. Birasa anatoka zahanatini.
10. Birasa anaumwa. Ameumia kwenye mkono wake.

Zoezi, ukurasa 48 - 49

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi.

Zoezi la I, ukurasa 49

- I. Mwalimu atathmini sentensi zitakazotungwa na wanafunzi, kwa mfano:

Mimi ninacheza mpira. - Sisi tunacheza mipira.

- | | | |
|----------------------|---|-------------------------|
| Wewe unacheza mpira. | - | Nyinyi mnacheza mipira. |
| Yeye anacheza mpira. | - | Wao wanacheza mipira. |

2. Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi, kwa mfano:

Umoja				Wingi			
Nafsi	Kiambishi nafsi	Kiambishi cha wakati	Kitenzi	Nafsi	Kiambishi nafsi	Kiambishi cha wakati	Kitenzi
Mimi	ni	na	cheza/ soma	Sisi	tu	na	cheza/ soma
Wewe	u	na	cheza/ soma	nyinyi	m	na	cheza/ soma
Yeye	a	na	cheza/ soma	wao	wa	na	cheza/ soma

Zoezi la 2, ukurasa 50

1. **Mimi** ninakimbia.
2. **Wao** wanafundisha.
3. **Wewe** unatunza mazingira yako.
4. **Yeye** anaenda sokoni.
5. **Nyinyi** mnatumia pesa zenu vizuri.
6. **Sisi** tunafurahia usawa wa kijinsia.
7. **Wao** wanalala mabwenini.
8. **Mimi** ninaingga darasani.
9. **Yeye** anachunguza nidhamu.
10. **Sisi** tunajali maslahi ya wanafunzi walemavu.

Zoezi la 3, ukurasa 50 - 51

1. Nyinyi mnacheza kandanda.
2. Wao wanakuja madarasani.
3. Mimi ninaandika barua.

4. Sisi tunaketi kwenye viti.
5. Wewe unachoma jani.
6. Yeye anatembea njiani.
7. Nyinyi mnaandika kwenye mbao.
8. Yeye anazungumza Kiswahili.
9. Sisi tunasimama mbele ya madarasa.
10. Wao wanaimba nyimbo za taifa la Rwanda.

Zoezi la kuigiza, ukurasa 5 I

Mwalimu awape wanafunzi mwongozo wa kuigiza mazungumzo kati ya wanafunzi.

Zoezi la imla, ukurasa 5 I

Mwalimu awasomee wanafunzi maneno yafuatayo:

Darasa	Shulenii
Mwalimu	Kalamu
Ubao	Bwalo
Daftari	Chaki
Mwanafunzi	Kandanda

Somo la Tatu

Viongozi wetu shuleni

Muda: Vipindi 2

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha mazungumzo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi.
- Kutaja majina ya viongozi mbalimbali wapatikanao shuleni.
- Kudhihirisha mahusiano baina ya watu wapatikanao shuleni.
- Kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati wa mazingira ya shule.

b) Vifaa vyta kujifunzia

- Vinasa sauti
- Michoro ya mazingira tofauti ya shule kama vile ofisi ya walimu na viongozi wengine.
- Vifaa vyta shule kama vile vitabu, kalamu, kifutio, ubao, chaki, n.k.
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 52
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu.

c) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu msamiati wa mazingira ya shule kwa kuwekea mkazo majina ya viongozi na watu wengine wapatikanao katika mazingira ya shule. Tofauti na masomo yaliyotangulia ambayo yamejikita katika mtindo wa kimazungumzo, somo hili linahusu kifungu cha habari kilichoandikwa kinathari. Kwa hivyo, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wake wanajizoeza maandishi ya aina hii kuitia mazoezi yaliyoandaliwa hasa zoezi la kusoma kwa utambuzi wa herufi, silabi, sentensi na hata matumizi

ya alama mbalimbali za uakifishaji zilizopo. Ili kurahisisha uelewa wa wanafunzi, mwalimu awapeleke wanafunzi wake katika mazingira ambapo wao wenyewe wanaweza kutambua na kuonyesha sehemu mbalimbali za shule yao kama vile; ofisi mbalimbali, bwalo, vidato tofauti, mabweni, viwanja vilivyopo n.k. Hivyo basi, baada ya kusoma na kupata maelezo kuhusu mambo yaliyozungumziwa katika somo hili, ni vyema wanafunzi watoke nje ya darasa lao ili kujifunzia katika mazingira halisi ya shule yao ambapo mwanafunzi anawaonyesha wenzake sehemu hizo za shule zilizotajwa. Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi wake. Aidha, ni lazima mwalimu azingatie wakati unaofaa wa kuonyesha vifaa hivyo hadharani ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona ni lazima pia mwalimu atumie vifaa hivyo kwa kuwaomba wao wenyewe kuvigusa huku wakitaja majina ya vifaa hivyo. Katika somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi kulingana na maelekezo yaliyotolewa katika kila zoezi linalohusika.

d) **Utaratibu wa somo**

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita nao wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu wao. Baadaye, mwalimu achukue fursa hii kuwaomba wanafunzi wasahihishe zoezi walilopewa kama kazi mradi ili aweze kuendelea na somo jipya. Kisha, mwalimu awachangamshe wanafunzi wake kwa kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu picha na michoro iliyopo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 52. Kwa mfano: ‘*Mnaona nini kwenye picha hizi?*’ Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu maswali yaliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile: “*Mimi ninaona...*” Kwa mfano: ‘*Mimi ninaona ofisi ya mkuu wa shule*’ Katika hatua hii, ni lazima mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kupata ujuzi kuhusu tafakuri tандuizi kuititia picha za wanafunzi zinazoonyesha viongozi mbalimbali wapatikanao shuleni na hata wajibu wao huku akiwasaidia kuwasiliana katika lugha rasmi. Wanafunzi watazame picha hizo walizoonyeshwa na mwalimu wao na kujibu maswali yaliyoulizwa huku wakielekezwa kutambua nafasi ya uongozi bora shuleni na wajibu wao katika ujifunzaji na mienendo mizuri inayotakikana shuleni.

Hatua ya 2: Kusoma na ufahamu

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu kinachohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaopata. Hivyo basi, wanafunzi wasome kwa kimya pamoja na kuandika msamiati huo mpya. Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wote

wamesoma kwa kimya kama walivyoambiwa, mwalimu aulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu cha habari kilichosomwa. Kwa mfano, anaweza kuuliza swali lifuatalo: ‘*Kiranja wa darasa ni nani?*’ Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale walivoyasoma katika kifungu hicho. Kwa mfano: ‘*Kiranja wa darasa ni Kayitare.*’ Baada ya kupata picha ya uelewa wa jumla wa wanafunzi kuhusu kifungu cha habari kinachohusika, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa sauti kifungu hicho. Wanafunzi wasome kwa sauti kama walivyoambiwa na mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa kwa lengo la kutambua herufi, silabi na sentensi. Vilevile, ni lazima mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanasoma kwa kuzingatia matumizi ya alama za uakifishaji zilizopo katika kifungu cha habari walichopewa.

Hatua ya 3: Ujifunzaji wa msamiati wa viongozi wa shulenii

Mwalimu atoe maelekezo kuhusu namna ya kutafuta maana za msamiati mpya ambao uliorodheshwa na wanafunzi wakati wao wa kusoma kifungu cha habari kilichopo. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujadiliana kuhusu msamiati huo. Wanafunzi wazingatie matumizi ya msamiati huo katika kifungu kilichopo na wajadiliane kuhusu msamiati huo huku wakinumia kamusi pale panapohitajika. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi na kuwaelekeza pale wanapotatizika. Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza la msamiati kwa kuwafafanulia kile kinachotakiwa kutimizwa katika zoezi hilo. Mwalimu awaombe wanafunzi kuchunguza michoro iliyopo na kuihusisha na sentensi zilizopo huku akiwatolea mfano. Wanafunzi wajibu swali hilo kama walivyoelekezwa na mwalimu na kulisahihisha mara moja wanapolimaliza. Katika zoezi la pili, mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kukamilisha mapengo yaliyoachwa katika sentensi walizotolewa kwa kutumia maneno yaliyopo. Wanafunzi wafanye zoezi hilo kulingana na maelekezo ya mwalimu wao na kusahihisha kwa pamoja baada ya kulimaliza. Ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba kila msamiati unaotumiwa umeeleweka ipasavyo kwa wanafunzi wote kwa kuomba wanafunzi kuisoma sentensi moja moja na kuielewa ipasavyo. Kwa hivyo, achukue fursa kwa kutumia mifano katika hali ya mazingira ya shule ili kurahisisha uelewa wa wanafunzi. Kwa mfano, anaweza kuwaomba watoke nje ili waweze kuona wenyewe ofisi za viongozi walipo shuleni na hata kutumia ishara za mwili katika kufafanua baadhi ya msamiati uliopo.

Isitoshe, ni lazima mwalimu azingatie kwamba wanafunzi wanastahili kurejelea matumizi ya msamiati husika katika kifungu cha habari walichokisoma ili kuelewa zaidi. Wakati wa kujibu mazoezi haya, mwalimu atumie mifano mingine inayoweza

kusaidia wanafunzi kupata ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, stadi za maisha kwa kurejelea umuhimu wa mambo yanayofanywa shulen i vile kuvaare sare, mienendo mizuri na wajibu wa wanafunzi na viongozi wao, na kadhalika. Vilevile, kupidia mahusiano baina ya watu wapatikanao shulen, mwalimu achukue fursa hii kuwasaidia wanafunzi kutafuta suluhisho la matatizo yanayowakumba. Kwa mfano, anaweza kurejelea umuhimu wa kulipa karo ya shule kupidia benki na kuleta hati ya malipo kwa muda unaotakikana na hasara inayoweza kumpata mwanafunzi wakati anapokaa na pesa hizo za shule bila kuzilipa kwani zinaweza kuibwa. Ujuzi kuhusu ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha nao unapatikana katika hatua hii pale ambapo mwalimu anarejelea vitendo vya kuheshimu viongozi wao shulen, mienendo inayotakikana katika mazingira mbalimbali ya shule kama vile bwaloni na mabwenini na umuhimu wa kuwa hodari katika mambo wanayoyafanya shulen na hata nje ya shule.

Hatua ya 4: Kusikiliza na kuzungumza

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma na kutamka kwa usahihi maneno ya ufahamu uliotolewa katika *Kitabu cha Wanafunzi, ukurasa 53-54* kwa utambuzi wa herufi na silabi. Mwalimu aweke mkazo juu ya matamshi ya irabu mbili zinazofuatana katika silabi tofauti kama vile: ‘wanaingia,’ silabi za konsonanti pekee *m* na sauti *tʃ* ambayo ina muundo ulio tofauti na ule uliopo katika lugha ya kwanza ya wanafunzi. Hivyo basi, wanafunzi wote wapewe muda wa kutosha ili watamke kwa usahihi maneno hayo na vifungu vya maneno vilivyotolewa huku mwalimu akirekebisha pale ambapo wanafanya makosa. Ni vyema mwalimu atilie mkazo tofauti hizo na asaidie wanafunzi kutafakari kuhusu matamshi sahihi ya lugha ya Kiswahili ili waweze kutumia matamshi bora ambayo yanawasaidia pia kuwasiliana katika lugha rasmi na watu wengine.

Hatua ya 5: Ufahamu

Katika hatua hii ya ufahamu, mwalimu awaombe tena wanafunzi kusoma kwa makini na kwa kimya kifungu cha habari kilichopo huku wakijibu maswali yaliyotolewa katika sehemu ya ufahamu. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitoa maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

Hatua ya 6: Hitimisho

Katika hatua hii ya mwisho wa somo hili, mwalimu ahitimishe somo kwa kuuliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyofunza ili kuhakikisha kuwa wanaweza kutaja majina ya viongozi wao shulen. Maswali mengine yalenge mahusiano kati ya watu wapatikanao shulen na hata ujifunzaji wa mambo mbalimbali

yanayofanywa na wanafunzi na wajibu wa viongozi wao. Wanafunzi waelekezwe katika kuwatambua watu mbalimbali na kazi zao. Ili kusaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi wake katika namna ya kujibu zoezi la tatu la msamiati na kuwaomba walifanye kama kazi mradi. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza somo la nne la mada hii ya 'msamiati wa mazingira ya shule'.

Mazoezi ya ziada

Ili kuwasadia wanafunzi wa kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe wanafunzi hawa kutunga sentensi nne zinazoonyesha majina ya viongozi wao pamoja na wajibu wao. Mwalimu awape mfano wa sentensi na awaelezee kile wanachotakiwa kukifanya. Kwa mfano:

Swali: *Taja majina ya viongozi wako shuleni na kazi zao.*

Jibu: *"Mkuu wa shule anaongoza shule."*

e) **Tathmini**

Katika sehemu hii ya tathmini, mwalimu alenge kutambua ikiwa ujifunzaji umefanywa kwa namna ya kuridhisha. Kwa hivyo, apime uwezo wa wanafunzi kuititia maswali mbalimbali kuhusiana na utambuzi wa majina ya viongozi na wajibu wao, matumizi ya msamiati waliojifunza katika sentensi fupifupi na hata kutambua mahusiano ya watu wapatikanao shuleni ili kuchunguza mienendo mizuri inayotakikana kwa kila mmoja. Hivyo basi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutafakari na kukuza stadi zao za utafiti kuhusu mienendo inayomtambulisha mwanafunzi kulingana na mazingira alipo shuleni kama vile mabwenini, bwaloni, darasani, namna ya kuheshimu viongozi wake na wanafunzi wenzake kama vile kutopiga kelele wakati wanapoingia mabwenini, bwaloni, kuepuka tabia mbaya za ulafi bwaloni, kuheshimu kiranja wao na hata kuwajibika ipasavyo katika shughuli zao za ujifunzaji.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 53 - 54

1. Kwizera anasoma katika shule ya sekondari ya Gikondo.
2. Yeye anasoma katika kidato cha kwanza.
3. Kiranja wao ni Kayitare.
4. Kwizera anaelewa vizuri masomo ya Kiswahili, Kinyarwanda, Kiingereza, Hisabati, Jiografia, Historia na mengine.

5. Viongozi wao ni: mkuu wa shule, mwalimu wa mitaala (mwalimu wa taaluma), mwalimu wa nidhamu, mhasibu na mukutubi, mwalimu mshauri wa wasichana na mwalimu mshauri wa wavulana.
6. Mwishoni mwa kila muhula wanafunzi hufanya mtihani.
7. Katika mikutano na mkuu wa shule, kiranja wao huuliza maswali mazuri.
8. Hakutajwa.
9. Mkuu wa nidhamu huwaadhibu wanafunzi wanaofanya makosa.
10. Walimu washauri huingia bwaloni kuchunguza chakula cha wanafunzi na kuwashauri kuheshimiana wakati wa kula.

Zoezi la 1, ukurasa 54

Mwalimu awape wanafunzi mwongozo wa kueleza shughuli zao wakiwa shulenii. Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi.

Zoezi la 2, ukurasa 55

1. Huu ni **muhula** wa kwanza wa mwaka wa shule.
2. Tunafanya **mtihani** wa Kiswahili. Mwalimu wetu ametupa maswali rahisi.
3. Wanafunzi wote wa shule yangu wanavaa **sare**.
4. **Kiranja** wa darasa letu anaitwa Kagabo. Yeye anasimamia wanafunzi wenzake.
5. **Mkuu** wa shule yetu ni mzuri sana. Yeye anaongoza shule vizuri.
6. Mwalimu mshauri wa wasichana **anachunguza** nidhamu ya wasichana.
7. Mwalimu mshauri wa **wavulana** anapanga michezo shulenii.
8. Wanafunzi wanalala **mabwenini**.
9. Walimu washauri wanaingia **bwaloni** kuchunguza chakula chetu.
10. Wakati wa chakula cha **mchana** tunaenda bwaloni.

Zoezi la 3, ukurasa 55-56

- | | | | | | |
|-----|---|----|---|----|---|
| 1. | J | 2. | B | 3. | H |
| 4. | D | 5. | I | 6. | E |
| 7. | F | 8. | A | 9. | G |
| 10. | C | | | | |

Zoezi, ukurasa 57

1. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kushiriki mjadala kwa kuwagawa katika makundi.
2. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika matumizi sahihi ya kamusi ili kupata maana za maneno waliyopewa. Kwa mfano:
 - a) Mhariri: Mtu anayesoma, kusahihisha na kusanifu miswada ya maandishi kama vile vitabu au makala.
 - b) Malenga: Mtu ambaye ni bingwa wa kutunga mashairi na nyimbo.
 - c) Msasi: Mtu anayewinda wanyama pori.
 - d) Sogora: Fundi wa kupiga ngoma.
 - e) Mhandisi: Mtu mwenye elimu ya kutengeneza na kuhudumia mitambo, majengo na madaraja.

Zoezi la kutamka, ukurasa 57

Mwalimu awape wanafunzi mwelekeo wa namna ya kusoma sentensi zilizo katika kitabu chao. Mwalimu ayarekebishe makosa yoyote ya kimatamshi pindi tu yatakaposikika.

Shule yangu

Muda:Vipindi 2

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi.
- Kutaja baadhi ya kazi zinazofanywa na watu waliosoma.
- Kutumia msamati wa mazingira ya shule katika sentensi fupifupi.
- Kutambua na kutumia vivumishi vyta sifa katika sentensi fupifupi.
- Kulinganisha shule mbili kwa kutumia neno **kuliko na sawasawa**.

b) Vifaa vya kujifunzia

- Vinasa sauti
- Vifaa vya shule kama vile vitabu, kalamu, kifutio, ubao, chaki, n.k.
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 58
- Michoro ya watu tofauti waliosoma na kazi zao
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

c) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia somo hili kama vilivybainishwa hapo juu. Katika kuendeleza somo, mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kama vile picha mbalimbali za watu wanaofanya kazi tofauti ili kuwachochaea wanafunzi kuelewa na kufikiria kuhusu kazi mbalimbali zinazofanywa na watu waliosoma na kuwachochaea kujali kazi yoyote kwa kuifanya vizuri. Aidha,

ni lazima mwalimu azingatie wakati unaofaa wa kuonyesha vifaa hivyo hadharani ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Vilevile, ni vyema mwalimu azingatie hapo mwanzoni kwamba sarufi iliyotolewa katika somo hili ni mwendelezo wa wakati uliopo uliojitokeza katika somo la pili la mada hii. Hivyo basi, ni lazima arejelee mambo muhimu yaliyopatikana katika somo hilo kama vile nafsi, viambishi vya nafsi na kiambishi cha wakati ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wanakumbuka vizuri matumizi ya wakati uliopo katika tungo yakinishi. Hatimaye, mwalimu aendelee kufundisha wakati uliopo katika tungo kanushi huku akitilia mkazo tofauti zinazojitokeza kati ya tungo yakinishi na tungo kanushi. Katika somo hili, mwalimu ahakikishe pia kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi kulingana na maelekezo yaliyotolewa katika kila zoezi linalohusika.

d) **Utaratibu wa somo**

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita na wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu wao. Mwalimu achukue fursa hii kusahihisha kazi iliyotolewa kwa wanafunzi kama kazi mradi; yaani kazi ya nje ya darasa. Mwalimu awachangamshe wanafunzi wake kwa kuwauliza maswali mepesi kuhusu shule yao na wangependa kufanya kazi gani wakimaliza shule. Kwa mfano: ‘*Mimi ningependa kuwa rubani.*’ Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama “*Mimi ningependa kuwa...*” Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu. Kwa mfano: ‘*Mimi ningependa kuwa daktari.*’ Baadaye, mwalimu aendelee na somo kwa kuwauliza kile kinachofanywa na watu ambao wangetaka kuwa katika siku za usoni. Kwa mfano, anaweza kuuliza: “*Daktari anafanya kazi gani?*” Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao kwa kuelezea kile kinachofanywa na watu waliowataja. Kwa mfano: ‘*Daktari hutibu magonjwa.*’ Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu agusie maswali yanayoelekeza wanafunzi kutafakari kuhusu nafasi ya msichana katika kazi zinazofanywa na watu. Maswali mengine yaweza kudhihirisha nafasi ya walemaru na jinsi wanavyoweza kufanya kazi za aina tofauti kiasi kwamba nao wanawenza kuwa watu maarufu sana katika jamii.

Hatua ya 2: Kusoma na ufahamu

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu kinachohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Baada ya kusoma kwa kimya, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu hicho ili kuhakikisha kuwa

wamesoma na kuelewa. Kwa mfano, awaulize; *Mimi ninaitwa nani? Shule yangu ni shule gani?* Wanafunzi nao wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hicho. Kwa mfano: *Mimi ninaitwa Kamali. Shule yangu ni shule ya sekondari ya Mugano.* Hatimaye, mwalimu awaambie wanafunzi wasome kwa sauti kifungu cha habari kinachohusika. Wanafunzi wasome kwa sauti mmoja baada ya mwengine. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanasona kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi huku akisahihisha pale ambapo wanafunzi wanafanya makosa. Mwalimu achunguze pia ikiwa wanafunzi wanasona kwa kuzingatia matumizi ya alama mbalimbali za uakifishaji katika kifungu cha habari kilichopo.

Hatua ya 3: Ujifunzaji wa msamiati

Mwalimu awaelekeze wanafunzi ili watafute maana za msamiati mpya waliokutana nao. Kwa hivyo, awagawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili waweze kujadiliana kuhusu maana za msamiati huo kulingana na matumizi yake katika kifungu cha habari walichokisoma. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika na kuwaelekeza katika matumizi ya kamusi pale panapohitajika. Aidha, mwalimu awaombe wanafunzi kufanya zoezi la kwanza la msamiati kwa kuwafafanulia kile kinachotarajiwa katika zoezi hilo. Katika zoezi la pili, mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuhusisha maneno katika sehemu A na maelezo yaliyomo katika sehemu B. Wanafunzi wafanye zoezi hilo kama walivyoambiwa na mwalimu. Aidha, katika kusahihisha mazoezi yaliyopo, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi ili waweze kupata ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi kuititia mifano mbalimbali ya kazi zinazofanywa na watu waliosoma: wanawake kwa wanaume. Vilevile, mifano ya majina ya wanawake waliomaliza masomo na kufanya kazi mbalimbali, waimbaji maarufu na madaktari inaweza kutolewa na wanafunzi ili kudhihirisha ikiwa wameelewa vizuri kile kilichozungumziwa katika kifungu cha habari kuititia mazoezi ya msamiati yaliyopo.

Hatua ya 4: Matumizi ya lugha

Katika hatua hii, mwalimu alenge kuwasaidia wanafunzi kuwa na ujuzi unaowasaidia kuwasiliana katika lugha rasmi. Ili kufikia lengo lake, mwalimu awaambie wanafunzi wasome sentensi zinazohusika huku akiwekea mkazo matumizi ya ratiba ya siku na wiki nzima. Kuititia mifano uliotolewa, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufanya zoezi la kwanza katika sehemu hii ya matumizi ya lugha. Aidha, mwanafunzi aorodheshe majina ya siku za wiki kuanzia Jumatatu hadi siku ya mwisho ya wiki kwa kubainisha shughuli za kila siku kama zinavyozungumziwa katika sentensi fupifupi zilizopo. Katika kuimarisha ujuzi wa wanafunzi kuhusu tafakuri tanduizi na

mawasiliano katika lugha rasmi, mwalimu achukue fursa hii kuwaomba wanafunzi wake kuzungumzia masomo yao na siku ambapo wanajifunza masomo hayo.

Hatua ya 5: Kusikiliza na kuzungumza

Katika sehemu hii, mwalimu awaombe wanafunzi kutamka kwa utambuzi wa herufi na silabi zilizopo katika maneno yaliyopo kuhusiana na siku za wiki. Mbali na kuwazoesha wanafunzi kutamka kwa usahihi majina ya siku za wiki na kutaja shughuli mbalimbali ambazo hufanywa na wanafunzi shulenii na hata nje ya shule yao, mwalimu atilie mkazo matamshi ya sauti na silabi zenyenye kutatiza wanafunzi kama zinavyojitokeza katika maneno yaliyotolewa. Kwa mfano, baadhi ya maneno yana silabi zenyenye konsonanti peke yake kama n, m, irabu mbili mbili katika silabi tofauti, silabi zenyenye mfuatano wa konsonanti ambao hawajauzoea kama katika neno *daktari na alhamisi* au silabi zitakazojirudiarudia kama ilivyo katika neno *sawasawa*. Kwa hivyo, mwalimu azingatie kwamba wanafunzi wote wanatamka kwa usahihi maneno na vifungu vya maneno vilivyotolewa kwa utambuzi wa herufi, silabi katika maneno yaliyopo kwa ajili ya kuwapatia ujuzi kuhusu mawasiliano katika lugha rasmi. Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kuwaomba wajadiliane kuhusu ratiba zao nje ya darasa kuanzia Jumatatu hadi Jumapili. Halafu, mwalimu amchague mwanafunzi mmoja kutoka kila kundi ili ajitokeze mbele ya darasa na kuwaeleza wenzake kuhusu shughuli zake za wiki za nje ya darasa.

Hatua ya 6: Ujifunzaji wa sarufi (vivumishi vya sifa)

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi wake kusoma sentensi zilizopo na kuchunguza sifa za kila kifungu kilichopigiwa mistari. Ili kufanikisha ujifunzaji wa sarufi katika sehemu hii, mwalimu afafanue kwanza mfano, *kiti kizuri* katika zoezi la kwanza kwa kubainisha jinsi ambavyo kiambishi cha jina *ki kinafanana* na kiambishi *ki kinachojitokeza* katika kivumishi *kizuri* ili wanafunzi wapate ufahamu kuhusu uhusiano wa jina na kivumishi cha sifa. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika katika uchunguzi wao wa sifa za vifungu vilivyopigiwa mistari. Hatimaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote kwa kusahihisha zoezi hilo la kwanza huku wakijadiliana kutokana na majibu mbalimbali yanayotolewa na wanafunzi. Aidha, mwalimu awaambie wanafunzi wachunguze sifa za jina na zile za kivumishi cha sifa kupitia sentensi zilizopo ili waweze kufanya zoezi la pili la sehemu ya sarufi. Wanafunzi nao wazingatie maelekezo ya mwalimu ili wayajibu maswali yaliyotolewa katika zoezi la pili la sehemu hii. Wanafunzi wasome kifungu cha habari kuhusu ‘shule yangu’ na kuandika vifungu vya maneno vyenye jina na kivumishi cha sifa kama wanavyopata katika mfano ‘madarasa mazuri’. Mwalimu

awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu ili waweze kulinganisha na kujadiliana kuhusu shule mbili wanazozifahamu kwa kubainisha sifa zake. Kwa hivyo, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wameweza kutumia ipasavyo maneno yanayotumiwa katika kulinganisha vitu viwili kama vile *kuliko* na *sawasawa*. Baadaye, mwalimu amchague mwanafunzi mmoja kutoka kila kundi na kumwambia aandike ubaoni mifano yake na kuwaomba wanafunzi wengine kutoa mchango wao na kurekebisha pale ambapo wamekosea.

Hatua ya 7: Ufahamu

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa makini kifungu cha habari kuhusu ‘*shule yangu*’ huku wakiyajibu maswali yaliyotolewa kama maswali ya ufahamu. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo.

Hatua ya 8: Hitimisho

Katika hatua hii ya kuhitimisha somo hili, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza ili kuhakikisha kwamba wanaweza kutambua na kutumia vivumishi vya sifa katika sentensi fupifupi. Isitoshe, mwalimu awaulize maswali mengine kwa kurejelea majina ya kazi zinazofanywa na watu waliokamilisha masomo, kulinganisha shule mbili kwa kutoa sifa zake huku wakitumia maneno kama *kuliko* na *sawasawa*, kurejelea ratiba yao kwa kubainisha shughuli zao za kila siku darasani na hata nje ya darasa. Ni vyema pia mwalimu ahitimishe somo hili kwa kuuliza maswali yanayodhamiria kuchunguza ikiwa wanafunzi wameelewa umuhimu wa kuwajibika kazini, kutodhalilisha na kujali aina yoyote ya kazi inayofanywa, kutodharau mtu kulingana na kazi anayoifanya, kupenda kazi, kujivunia kazi unayoifanya na kutembelea shule ambapo ulisomea kama njia nzuri ya kujivunia shule yako na kuwa mfano mzuri kwa wanafunzi waliopo. Ili kusaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu zoezi la msamiati na kuwaomba walifanye kama kazi mradi. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza somo la tano la mada hii ya ‘msamiati wa mazingira ya shule’.

e) **Mazoezi ya ziada**

Ili kuwasaidia wanafunzi wa kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe wanafunzi hawa kutunga sentensi nne zinazoonyesha majina ya viongozi wao pamoja na wajibu wao. Mwalimu awape mfano wa sentensi na awaelezee kile wanachotakiwa kukifanya. Kwa mfano:

“Mkuu wa shule anaongoza shule.”

Swali: *Taja majina ya viongozi wako shuleneni na kazi zao.*

f) Tathmini

Katika sehemu hii ya tathmini, mwalimu aulize maswali yanayolenga kutambua ikiwa ujifunzaji umefanywa kwa namna ya kuridhisha. Kwa hivyo, maswali hayo yapime uwezo wa wanafunzi wa kurejelea ratiba yao ya wiki kwa kubainisha masomo wanayojifunza na hata kazi nyingine wazifanyazo nje ya darasa. Vilevile, maswali mengine yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia vivumishi vya sifa huku wakitafakari kuhusu mienendo mizuri inayomtambulisha mtu aliyejifunza. Hivyo basi, mwalimu achunguze ikiwa wanafunzi wamepata pitcha ya stadi za maisha kupitia maswali mbalimbali yanayohusiana na kazi wanazopenda kufanya na zile wasizopenda kufanya baada ya kumaliza masomo yao.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 58 - 59

1. Mimi ninaitwa Kamali.
2. Mimi ninasoma katika shule ya sekondari ya Mugano.
3. Ndugu zangu ni Kagabo na Mutesi.
4. Wao wanasoma katika shule ya sekondari ya Mugano.
5. Mimi ninasoma katika kidato cha kwanza.
6. Hapana darasa lao ni dogo.
7. Munyana ni mwimbaji maarufu.
8. Kayitare anajenga maghorofa mrefu mjini Musanze.
9. Kalisa, Kayitare na Munyana walisoma katika shule ya sekondari ya Mugano.
10. Wasichana wanavaa marinda mrefu na wavulana wanavaa suruali na mashati mazuri.

Zoezi la I, ukurasa 59

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma sentensi zilizo kwenye *Kitabu cha Wanafunzi*, ukurasa 60 kwa usahihi. Mwalimu akosoe makosa ya kimatamshi.

Zoezi la 2, ukurasa 60

- | | |
|------|------|
| 1. C | 2. A |
| 3. H | 4. E |
| 5. B | 6. D |
| 7. F | 8. G |

Zoezi la 3, ukurasa 60 - 61

1. Nyumba hii ni **nzuri**. Nyumba hii ni safi sana.
2. Bagabo ni **fundi** wa uchoraji. Yeye anaweza kuchora picha za vitu vingi sana.
3. Mtoto huyu ni **mdogo** sana. Ana miaka mitatu.
4. Yeye alijenga nyumba **ndefu** sana. Nyumba yake inapendeza.
5. Kalisa ni mchoraji **maarufu** sana. Picha zake zinapendwa na watu wengi.
6. Mwanafunzi huyu ni **mwerevu** kabisa. Yeye anafaalu masomo yote.
7. Yeye ni **mwimbaji** mzuri sana. Anaimba nyimbo za Mungu.
8. Mtoto huyu ni mdogo **kuliko** Amina. Yeye hatembe i vizuri.
9. Kitabu hiki ni **sawasawa** na kitabu changu. Vitabu vyote vinazungumzia somo la Kiswahili.
10. Watoto **wabaya** hawapendi kufanya mazoezi yao. Wao wanapiga kelele darasani.

C. Kusikiliza na kuzungumza

I. Wanafunzi watamke kwa usahihi maneno yafuatayo:

- Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi, Ijumaa, Jumamosi, Jumapili.
- Bidii, sawasawa, ninaitwa, mimi ninajivunia, maarufu, daktari, wafuasi, hospitali, kuliko, mwimbaji.

2. Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wazungumzie shughuli wanazozifanya nje ya darasa kuanzia Jumatatu hadi Jumapili.

Baadhi ya shughuli za nje ya darasa zinaweza kuwa:

- **Jumatatu** tuna michezo mbalimbali.
- Jumanne tunasali katika jumuiya zetu.
- Jumatano tunasafisha mazingira yetu.
- Alhamisi tuna mkutano na Mkuu wa shule.
- Ijumaa tuna michezo mbalimbali.
- Jumamosi tunasafisha mazingira yetu.
- Jumapili tunaenda kanisani kuomba.

Zoezi la 1, ukurasa 63

Kwa mfano: Mwalimu wetu ana kiti kizuri.

Jibu: kiti kizuri: **ki** katika neno kiti ni sawasawa na **ki** katika neno kizuri

1. kitabu kibovu ki/ki
2. mtoto mzuri m/m
3. nyumba mbaya na nyumba nzuri n/m na n/n
4. mtu mzima na mtoto mchanga. m/m na m/m
5. mkono mchafu m/m
6. viatu vizuri vi/vi
7. mashati mazuri ma/ma
8. madirisha makubwa ma/ma
9. mlango mrefu m/m
10. kitabu kizuri. ki/ki

Zoezi la 2, ukurasa 63 - 64

a) Kwa mfano: madarasa mazuri

- viongozi wazuri
- wanafunzi wazuri
- maghorofa marefu
- marinda marefu
- mashati mazuri

b) *Kwa mfano: Shule ya sekondari ya Mtakatifu Yohana ni nzuri kuliko shule ya sekondari ya Kimisagara.*

- Wanafunzi wanaweza kulinganisha shule mbili kwa kutumia: zuri, baya, chafu, kubwa, dogo, n.k.

Usafi shuleni

Muda: Vipindi 2

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha mazungumzo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi.
- Kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati wa mazingira ya shule.
- Kutambua vitendo mbalimbali vinavyohusiana na usafi shuleni.
- Kubainisha na kutofautisha sifa za wakati uliopo; tungo kanushi.

b) Vifaa vya kujifunzia

- Vinasa sauti
- Michoro ya vifaa tofauti vilivyo ndani ya darasa
- Vifaa vinavyotumiwa katika shughuli za usafi shuleni kama vile ufagio, majembe, vifutio, n.k.
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 65
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu.

c) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia somo hili na azingatie kwamba sehemu kubwa ya ufunzaji inaweza kuegemezwa katika vitendo halisi vya kusafisha mazingira ya shule ili kurahisisha uelewa wa yale yanayozungumziwa katika somo zima. Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake waweze kutambua ubaya wa uchafu na athari zake kwa maisha ya watu pale ambapo usafi unaweza kulinganishwa na chanzo cha maisha mema. Hivyo basi, mbali na vifaa vinavyoweza kuonekana na kuguswa, mwalimu atumie pia michoro ili aweze kudhihirisha matunda ya kuzingatia usafi na athari mbaya za kukaa katika mazingira chafu. Kwa mfano, anaweza kuchora picha ya

mtoto aliye mgonjwa wa kipindupindu na ya mtoto mwenye afya nzuri.

Vilevile, ni lazima mwalimu azingatie kwamba somo hili ni mwendelezo wa masomo yaliyohusu matumizi ya wakati uliopo. Kwa hivyo, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua kwanza sifa za wakati uliopo; tungo yakinishi, ili waweze kuwa na msingi imara wa kujifunzia wakati uliopo; tungo kanushi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ipasavyo katika utambuzi wa viambishi nafsi na vya wakati uliopo ili wapate kuelewa vizuri yale yaliyomo katika sehemu ya sarufi ya somo hili. Ni vyema mwalimu akumbuke kuwatolea mifano ya viambishi tamati tofauti kama vile *a*, *u*, *e* na *i* na kuwaelezea jinsi viambishi hivyo hutumiwa katika tungo yakinishi na tungo kanushi za wakati uliopo. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe pia kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

d) Utaratibu wa somo

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuwaauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali wanayoulizwa kuhusu somo lililopita. Katika sehemu hii ya mwanzo, ni vyema mwalimu achukue fursa ya kusahihisha zoezi ambalo lilitolewa kwa wanafunzi kama kazi mradi ili kuhakikisha kuwa wote walielewa somo hilo. Baadaye, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne na kuwaomba wajadiliane kuhusu picha na michoro zilizopo katika *Kitabu cha Wanafunzi*, ukurasa 65 kwa kueleza kile wanachokiona. Ili kuwarahisishia kuelewa shughuli hii, mwalimu atumie mifano kuhusu baadhi ya yanayoonekana katika picha hizo. Kwa mfano, anaweza kuwaonyesha picha na kuwaambia: *Shule hii ni safi. Ina ua zuri.* Wanafunzi, kwa upande wao, wajadiliane katika makundi yao kisha wajitokeze mbele ya wenzao kwa kuwaelezea wenzao wanachokiona katika picha hizo. Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu aelekeze wanafunzi wake kuhusu ujuzi wa tafakuri tanduizi ambapo wanatofautisha picha ya shule chafu na picha ya shule safi. Vilevile, ubunifu na ugunduzi utiliwe mkazo kwa kuwachochea wanafunzi kufikiri na kugundua athari za uchafu na za usafi kuhusu maisha ya watu kuititia picha wanazozichunguza.

Hatua ya 2: Kusoma na ufahamu

Mwalimu aombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha habari kinachohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Wanafunzi nao wasome kwa kimya na kuandika msamiati huo mpya. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi

maswali mbalimbali kuhusu kifungu cha habari walichokisoma ili kuhakikisha kuwa wamesoma na kuelewa. Kwa mfano, anaweza kuuliza swali lifuatalo: *Ni shule gani zinazozungumziwa katika kifungu hiki?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hicho. Kwa mfano: *Shule zinazozungumziwa ni shule ya Sekondari ya Bwiza na Shule ya Sekondari ya Kimira.* Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu kilichopo, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa sauti kifungu hicho cha habari na kuhakikisha ikiwa wanasoma kwa namna inayofaa. Mwalimu asahihishe makosa pale yanapojitokeza.

Hatua ya 3: Ujifunzaji wa msamiati

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne na kuwaomba watafute maana za msamiati uliopo kufuatana na jinsi uliviyotumiwa katika kifungu cha mazungumzo walichokisoma. Mwalimu awaombe wanafunzi kutumia kamusi pale wanapohitaji na azunguke darasani kuelekeza wanafunzi wanaotatizika katika kuitumia kamusi hiyo. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma sentensi walizopewa na kujadiliana kuhusu maana za msamiati uliopigiwa mistari huku wakitunga sentensi zao wenyewe. Ni vyema mwalimu azunguke pia darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaopata ugumu katika zoezi hilo. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja zoezi hilo la msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliopo, mwalimu achukue fursa hii kuwaauliza wanafunzi kama kuna maneno ambayo hayaeleweki ili maana yake ijadiliwe kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika kifungu cha habari kilichopo.

Katika hatua hii, ni vyema mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio unaomuonyesha kiwango cha ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi ambapo sentensi zao huchunguzwa, mawasiliano katika lugha rasmi kupitia mifano inayoeleweka, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha, ubunifu na ugunduzi kulingana na kile anachokizungumzia mwanafunzi katika sentensi yake. Kwa hivyo, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika utunzi wa sentensi zenye maana inayosaidia wanafunzi kupata ujuzi unaotakikana.

Hatua ya 4: Ujifunzaji wa sarufi (wakati uliopo)

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi wake maswali mbalimbali kuhusu wakati uliopo; tungo yakinishi. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi wake kutunga sentensi zao kwa kutumia wakati uliopo; tungo yakinishi. Wanafunzi nao, kwa

upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao kuhakikisha kwamba wanakumbuka vizuri waliyoyasoma kuhusu wakati uliopo. Maswali ya mwalimu yalenge kutambua ujuzi wa wanafunzi katika matumizi ya nafsi, viambishi nafsi na kiambishi cha wakati *na*. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma sentensi zilizopo kwa kutilia mkazo tofauti kati ya tungo yakinishi na tungo kanushi. Hivyo basi, katika zoezi la kwanza la sarufi, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika matumizi sahihi ya vitenzi katika tungo yakinskihi na tungo kanushi kwa kusisitizia matumizi ya maneno *ndiyo* na *hapana*. Kupitia zoezi hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wametambua tofauti kati ya tungo yakinishi na tungo kanushi ili waweze kutafakari ilivyo kuhusu hali ya kukubaliana na mtu ya kukana au kukanusha matendo mbalimbali katika tungo zao.

Ili kufikia lengo hili, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kujibu maswali yaliyotolewa katika zoezi la pili la sehemu ya sarufi kwa kuwatolea mifano ya tungo katika hali yakinishi na hali kanushi katika nafsi zote sita. Wanafunzi nao wajibu maswali kama wanavyoelekezwa na mwalimu na kusahihisha zoezi hilo mara moja wanapomaliza. Aidha, mwalimu aombe wanafunzi wengine kutoa maoni yao kuhusu sentensi zilizotungwa na wenzao huku akiwasaidia kurekebisha pale wanapotatizika. Hatimaye, mwalimu awaambie wanafunzi wafanye zoezi la sarufi linalohusu kugeuza sentensi zilizotolewa katika tungo yakinishi au tungo kanushi. Katika kusahihisha zoezi hili, ni vyema mwalimu achunguze ikiwa wanafunzi wote wanajua jinsi wanavyobadilisha viambishi katika tungo hasa viambishi tamati vya hali yakinishi na vya hali kanushi. Baada ya kusahihisha kwa pamoja zoezi hili mwalimu awaambie wanafunzi wachunguze sentensi zilizotolewa kama maswali na zile zilizotolewa kama majibu na kuwaomba wajadiliane kuhusu miundo yake. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutambua kwamba vingi vya vitenzi vya Kiswahili humalizika na *a* ilhali vitenzi vingine huweza kuishia na *e*, *u* na *i*. Hivyo basi, awaombe kuchunguza sifa hizo na kutoa mifano yao ya vitenzi vingine vyenye miundo hiyo tofauti, kisha awaelekeze ili waweze kujibu zoezi la nne la sehemu ya sarufi. Wanafunzi wasahihishe kwa pamoja zoezi hilo huku wakielekezwa na mwalimu kulinganisha sifa za vitenzi vilivyotolewa katika tungo yakinishi na tungo kanushi.

Isitoshe, katika kufanikisha ujifunzaji wa sarufi katika sehemu hii, wanafunzi waelekezwe kuhusu jinsi watakavyojadiliana katika makundi yao na kutambua sifa za umoja na za wingi wa tungo; kubadilisha nafsi kutoka nafsi za umoja hadi kwa nafsi za wingi, kubadilisha viambishi nafsi kutoka viambishi vya umoja hadi viambishi vya wingi au kinyume cha hayo huku hali kanushi na hali yakinishi zikilinganishwa. Vilevile, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wote wameshirikishwa kusahihisha

mazoezi yaliyopo kwa kuwachochea kupata ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi ambapo anaweza kuwaomba wanafunzi wengine kuchunguza majibu yanayotolewa na wenzao, suluhisho la matatizo ambapo anawaomba wanafunzi kutoa suluhisho la matatizo ya wenzao, ubunifu, ugunduzi na stadi za utafiti ambapo anawaomba wanafunzi kuchunguza mifano iliyopo na ile inayotolewa na wanafunzi wengine, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha na hata ujifunzaji wa muda mrefu katika harakati zake za kudumisha mawasiliano katika lugha rasmi kuitia mifano iliyotolewa katika mazoezi yaliyotolewa na mingine inayotolewa na wanafunzi wenye.

Hatua ya 5: Kusikiliza na kuzungumza

Mwalimu awaombe wanafunzi kufunga vitabu vyao na kufungua madaftari yao. Mwalimu aendelee kwa kuwasomea aya ifuatayo ili waiandike katika madaftari yao.

Wanafunzi wanafagia chooni . Mtoto mchafu anatupa takataka. Wanafunzi wazuri wanasadiana kusafisha popote palipo na uchafu shulen. Yeye anafaulu kupanda maua mazuri.Wao hawajali umuhimu wa usafi wa mazingira. Usiharibu mazingira. Zingatia umuhimu wa shughuli za usafi shulen. Huyu ni daktari mzuri. Yeye anajishughulisha na mambo ya usafi katika hospitali kuu mjini Kigali.

Katika zoezi hili la imla, mwalimu azingatie kwamba maneno yaliyopo yana utata kwa wanafunzi pale ambapo baadhi yake yana silabi ambazo wanafunzi hawajazizoea katika lugha yao ya mama kama vile mfuatano wa irabu mbili ambazo zinajitokeza katika silabi tofauti katika neno moja, matumizi ya sauti / na r ambazo ni fonimu tofauti katika lugha ya Kiswahili, sauti kama gh, na mfuatano wa konsonanti kama kt katika neno daktari na sp katika neno hospitali. Hali hii ichochee wanafunzi kutafiti kuhusu maneno mengine yenye kuwa na sifa hizo katika lugha ya Kiswahili kama njia ya ujifunzaji wa kudumu kwa wanafunzi pale wanapoweza kutumia maneno hayo katika mawasiliano yao na watu wengine bila tatizo lolote.

Hatua ya 6: Ufahamu

Katika hatua hii ya ufahamu, mwalimu awaombe tena wanafunzi kusoma kwa makini na kwa kimya kifungu cha habari kuhusu: *Usafi Shulen* huku wakiyajibu maswali yaliyotolewa kama maswali ya ufahamu. Baadaye, mwalimu ashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo.

Hatua ya 8: Hitimisho

Katika hatua hii ya somo, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza ili kuhakikisha kuwa wanaweza kurejelea umuhimu wa usafi shulen, vitu vinavyosafishwa, watu wanaoshiriki kusafisha mazingira ya shule,

athari za uchafu kwa maisha yao, kulinganisha shule mbili katika shughuli za usafi kwa kutumia ipasavyo maneno kama *kuliko na sawasawa*, kurejelea shughuli zao za kila siku za usafi shulenii, na kadhalika. Vilevile, hatua hii ya somo igusie matumizi ya wakati uliopo katika tungo kanushi kwa kulinganisha baadhi ya sentensi zenye vitenzi katika tungo yakinishi na tungo kanushi. Ili kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi wake katika namna ya kujibu zoezi la tano la sehemu ya sarufi na kuwaomba walifanye kama kazi mradi. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza somo litakalofuata.

e) **Zoezi la ziada**

Mwalimu atoe zoezi la ziada ambalo linalenga kuinua kiwango cha chini kwa wanafunzi dhaifu ; yaani wanafunzi wasioweza kuelewa haraka kama wenzao.

- a) *Tunga sentensi kwa kuonyesha vitu vinayyosafishwa shulenii.*
Kwa mfano : *Wanafunzi wanasa fishwa ubao.*

- b) *Tunga sentensi tatu katika umoja kwa kutumia vitenzi katika wakati uliopo, tungo yakinishi. Zigeuze sentensi hizo katika tungo kanushi.*
Kwa mfano: *Mimi ninazungumza vizuri lugha ya Kiswahili. (Tungo yakinishi)*
Mimi sizungumzi vizuri lugha ya Kiswahili. (Tungo kanushi)

- c) *Tunga sentensi tatu katika wingi kwa kutumia vitenzi katika wakati uliopo, tungo yakinishi. Zigeuze sentensi hizo katika tungo kanushi.*
Kwa mfano: *Nyinyi mnafurahi sana.*
Nyinyi hamfurahi sana.

Tungo yakinishi: Mtoto huyu anaimba nyimbo za Mungu

Tungo kanushi: Mtoto huyu haimbi nyimbo za Mungu

1. Tungo yakishi: Wanafunzi wanawatii walimu wao.
2. Tungo kanushi: Wanafunzi hawawatii walimu wao.
3. Tungo yakinishi: Hakimu anaamuru kwamba kila mwizi aadhibiwe kwa kosa lake.
4. Tungo kanushi: Hakimu haamuru kwamba kila mwizi aadhibiwe kwa kosa lake.
5. Tungo yakinishi: Mimi ninajivunia kusoma katika shule yangu.

- | | |
|---------------------|--|
| Tungo kanushi: | Mimi <u>sijivunii</u> kusoma katika shule yangu. |
| 4. Tungo yakinishi: | Sisi <u>tunazungumza</u> Kiswahili na Kiingereza |
| Tungo kanushi: | Sisi <u>hatuzungumzi</u> Kiswahili na Kiingereza |
| 5. Tungo yakinishi: | Nyinyi <u>mnaheshimu</u> wazazi wenu. |
| Tungo kanushi: | Nyinyi <u>hamheshimu</u> wazazi wenu |

Tathmini

Katika sehemu hii, mwalimu atathmini ikiwa malengo ya somo zima yameafikiwa kwa kiwango alichokitarajia. Hivyo basi, aulize maswali kwa kuchunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kutumia msamiati unaohusu usafi wa mazingira ya shule. Maswali mengine yatathmini kiwango cha wanafunzi katika matumizi ya wakati uliopo, hasa katika kutofautisha tungo yakinishi na tungo kanushi kwa kurejelea mambo muhimu yanayoweza kubadilika kama vile viambishi awali na viambishi tamati. Aidha, mwalimu achunguze ujuzi wa wanafunzi katika kudumisha mawasiliano katika lugha rasmi kwa kurejelea msamiati uliopatikana katika kifungu cha habari walichokisoma na kuutumia katika sentensi fupifupi. Katika sehemu hii ya tathmini, mwalimu awaulize pia maswali yanayoweza kuonyesha ikiwa wanafunzi wamepata picha kamili ya mienendo mizuri inayomtambulisha mwanafunzi anayejali usafi wa mazingira ya shule yake na hata mahali popote anapokwenda kama vile nyumbani, mjini, nk.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 66

1. Mutoni anasoma katika shule ya sekondari ya Bwiza.
2. Ni Aisha, Kabera na Marita wanaofagia darasani.
3. Wanasa fisha vyoo.
4. Ni Mutoni na Kayitare.
5. Shule ya Kimira.
6. Hapana.
7. Miti na maua.
8. Hapana. Wanafunzi wa shule ya sekondari ya Kimira hawajui umuhimu wa usafi.
9. Wanafunzi wa Kimira wanatupa takataka popote.
10. Wanafunzi wa shule ya Bwiza

Zoezi, ukurasa 66 - 67

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Ziwe sahihi. Kwa mfano:

1. Sare yangu ni safi.
2. Kwetu kuna bustani ya maua mengi.
3. Tunafaa kudumisha usafi nyumbani mwetu.

Zoezi la Sarufi, ukurasa 68

1. Hapana. Mimi sisomi kitabu cha Kiingereza.
2. Ndiyo. Mimi ninasoma kitabu cha Kiswahili.
3. Hapana. Wewe huandiki daftarini; wewe unaandika ubaoni.
4. Hapana. Yeye haingii kanisani; yeye anaingia darasani.
5. Ndiyo. Sisi tunacheza kandanda.
6. Hapana. Sisi hatuchezi karata.
7. Ndiyo. Nyinyi mnapenda kuimba.
8. Hapana. Nyinyi hampendi kucheza.
9. Hapana. Wao hawafuti ubao.
10. Ndiyo. Wao wanafagia darasani.

Zoezi la I, ukurasa 69

1. Yeye haimbi vizuri.
2. Yeye anazungumza Kiswahili sanifu.
3. Mimi sipendi somo la Kiingereza.
4. Sisi hatupuuzi masomo haya.
5. Mimi ninatunga sentensi.
6. Wao hawashiki madaftari.
7. Nyinyi mnajitambulisha mbele ya wanafunzi wengine.
8. Wewe huazimi kitabu.
9. Wao wanachota maji.
10. Nyinyi hamtaenda mjini Kigali.

Zoezi la 2, ukurasa 70

1. Kalisa hachezi mpira.
2. Mimi na wewe tunaimba vizuri.
3. Sisi hatuingii darasani.
4. Mama na baba hawalimi shamba.
5. Mimi ninafanya mtihani.
6. Wewe husikilizi redio.
7. Kayitesi na wewe mnaigiza mazungumzo mbele ya wanafunzi
8. Wewe na Aisha hamkimbii haraka sana.
9. Wao hawawezi kushinda vizuri.
10. Mutoni na Bwiza wanapenda somo la Kiswahili.

Zoezi la imla, ukurasa 70

Mwalimu awasomee wanafunzi maneno na vifungu vifuatavyo:

1. Wanafunzi wanafagia chooni.
2. Wanafunzi wazuri wanasaidiana kusafisha popote palipo na uchafu shulenii.
3. Usiharibu mazingira.
4. Zingatia umuhimu wa shughuli za usafi shulenii.
5. Yeye anajishughulisha na mambo ya usafi katika shule yao.

Zoezi la makundi, ukurasa 70

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

MADA KUU: MATUMIZIYA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI

Mada Ndogo: Msamiati katika mazingira ya nyumbani

Idadi Ya Vipindi: 11

Ujuzi upatikanao katika mada hii:

1. Kusikiliza kwa makini
2. Kusoma kifungu cha habari kinachojitokeza na kutumia msamiati mahsusni katika sentensi fupi kwa kuzingatia ngeli ya A – WA.

Malengo ya kujifunza

Uhusiano wake na masomo mengine:

Somo hili lina uhusiano na Jiografia kwa kutoa ramani inayoonesha mahali pa majengo ya kuishi mjini au vijijini, somo la Soshiolojia kwa kuzungumzia mfuatano wa vizazi, Ufundi wa kujenga nyumba na Ufugaji.

Zana au vifaa:

- Ramani ya Rwanda inayoonesha mpango mkuu wa mazingira
- Picha au michoro ya nyumba za jadi na za kisasa
- Michoro ya vifaa tofauti ndani ya nyuma
- Picha za mifugo tofauti
- Vitabu vya wanafunzi
- Vinasa sauti

Kigezo cha tathmini na upimaji

Uwezo wa kutumia msamiati wa kutaja aina na sehemu za nyumba, mifugo nyumbani pamoja na umuhimu wake.

Maelezo kwa mwalimu

a) Utangulizi wa mada

Mada hii inashughulikia msamiati wa mazingira ya nyumbani. Mazingira ya nyumbani ni mapana na kwa hivyo mwalimu anastahili kuwa wazi kwa masuala mengi kama: watu wanaopatikana nyumbani, vifaa vinavyojenga nyumba hizo, vifaa vya ndani ya nyumba, mifugo wanaofugwa na kwa ujumla, faida na hasara za watu kukaa pamoja ama kuchukiana, faida na hasa za mifugo, umuhimu wa usafi nyumbani na shughuli za kila kifaa, mtu ama mifugo.

Mada hii imegusia:

- Aina za nyumba; za jadi na za sasa
- Ujenzi wake (vifaa vya kutumika)
- Uzuri na upungufu wa nyumba za jadi na kisasa
- Uhusiano wa watu wa familia nyumbani
- Majina yanayobainisha watu wa familia
- Mifugo wanaopatikana nyumbani
- Majina yanayowabainisha mifugo hao
- Vifaa vinavyopatikana ndani ya nyumba
- Vyumba ndani ya nyumba
- Sehemu za nyumba kama vile, dari n.k
- Ngeli ya A – WA, umoja na wingi
- Vivumishi, vimilikishi vya sifa, vionyeshi na viulizi; ‘gani?’ na ‘-ipi?’
- Tingo mbalimbali katika umoja na wingi katika ngeli ya A – WA

b) Masuala mtambuka

- Amani na maadili
- Mazingira na ubora wake
- Kazi na ufundi
- Elimu na jamii
- Kilimo na ufugaji
- Utamaduni na usasa

c) Ujuzi wa jumla

- Ubunifu na ugunduzi
- Ujifunzaji wa muda mrefu
- Ushirikiano na stadi za maisha
- Mawasiliano katika lugha rasmi
- Usuhihishaji wa matatizo
- Stadi za utafiti

Somo la Kwanza

Aina za nyumba, watu wanaoishi humo na ujenzi wa nyumba (vifaa)

Muda: Vipindi 2

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutaja aina za nyumba, wanaoishi humo na vifaa vya ujenzi wa nyumba hizo.
- Kuzungumza kwa ufasaha, kusoma kwa usahihi kifungu cha habari au mazungumzo, kwa utambuzi wa silabi, herufi, maneno na sentensi.

b) Vifaa vya kujifunzia

- Picha na michoro mbalimbali
- Vinasa sauti
- Vitabu, mabango na magazeti
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 76

c) Maandalizi ya somo

Mwalimu asichukulie kwamba msamiati wa nyumba ni rahisi kwa sababu kila mtoto anatoka nyumbani. Sharti akumbuke kuwa mazingira ya nyumba ni tofauti kwa kila mtoto. Baadhi wanatoka mashambani wengine mjini. Pia wengine wanatoka katika tabaka la juu wengine katika tabaka la chini. Isitoshe, baadhi ni watoto wa mzazi mmoja na wengine ni yatima. Baadhi wanaishi katika nyumba za kisasa wengine bado wanaishi katika nyumba za jadi. Mwalimu ayatilie haya maanani.

Pia awafahamishe wanafunzi kwamba tunapoishi sio sharti kwamba sisi ni bora kuliko wengine ama hatuwezi kuwa watu tunaotaka kuwa katika jamii. Awafanye wanafunzi kujikubali na kujiamini bila kujilinganisha na watu wengine.

Hatua 1: Utangulizi wa somo

Mwalimu atumie mifano dhahiri katika jamii, mwalimu afafanue kwa msaada wa picha na michoro, taarifa za magazeti na hata fanani katika mazingira husika.

Awalekeze wanafunzi kutaja nyumba, vifaa vya ujenzi na wahusika. Asikilize na kuelekeza mawazo ya wanafunzi kwa lengo la kuwatia imani. Mpangilio mzuri wa darasa na vikundi ni muhimu kwa mwalimu kuhakikisha kwamba somo hili linafanikiwa.

- Mwalimu awaamkie wanafunzi nao wamwamkie kisha awakumbushe somo lililopita.
- Mwalimu awaulize maswali ya dodosa kuhusu michoro au pitcha zilizo katika *Kitabu cha Wanafunzi*, ukurasa 76.
- Anakili hoja na mawazo ya wanafunzi.
- Mwalimu azingatie usawa wa kijinsia na wanafunzi wenye taathira ya kuona na kusikia, labda waketi mbele ya darasa n.k. Kwa hivyo azingatie hisia zote; kuona, kugusa, kunusa n.k.

Hatua 2: Kusoma na ufahamu

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma kwa sauti na kwa zamu. Kisha, awaelekeze kusoma kimya kimya na kwa kuzingatia sauti na maneno. Mwalimu awaelekeze kunakili maneno mapya kwenye madaftari yao. Mwalimu awaulize maswali ya dodosa ili kuwafanya wanafunzi kuelewa zaidi. Kwa mfano: ‘unaona nini kwenye pitcha? ‘Unaweza kueleza mazingira ya michoro?’ Pia, kama kuna muda, wanaweza kuigiza mazungumzo n.k. Mwalimu asahihishe matamshi na usomaji usio sahihi. Pia awashirikishe wanafunzi wote katika usomaji na kujibu.

Hatua ya 3: Ujifunzaji wa msamiati

Mwalimu apitie maagizo yanayohusu msamiati na kuyafafanua. Pia aeleze msamiati ambao bado haujaleweka vyema na wanafunzi kabla ya kuwaelekeza kujibu zoezi ama kutunga sentensi.

Mwalimu achukue muda kuwaelekeza wanafunzi wanyonge huku akipendekeza kazi ya ziada kwa wanafunzi werevu. Hapa ndipo vifaa huwa muhimu kwa mwalimu. Pia anaweza kuwashirikisha kwa kuwakumbusha kuwa bweni na darasa ni mfano wa nyumba au makao.

Mwalimu atumie mifano zaidi ya michoro na msamiati uliopendekezwa ili kufanikisha somo zaidi kabla ya kujibu zoezi.

Mwalimu ahimize umuhimu wa nyumba. Kwa mfano:

- Kujikinga dhidi ya mvua, wanyama, baridi n.k
- Kuhifadhi vitu vya kibinagsi

- Makao ya familia
- Hutupa hadhi ya umilikaji n.k

Hatua ya 4: Sarufi

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu ngeli ya A – WA. Awaeleze wanafunzi kuwa majina katika ngeli ya A-WA huchukua upatanisho wa vitenzi wa kutumia kiambishi cha umoja ‘a-’ na cha wingi ‘ wa-’. Pia awaambie kuwa hii ni ngeli ya viumbe hai: watu, wadudu, wanyama, ndege na viumbe wa mbinguni kama Mungu, malaika, shetani. Mwalimu awaulize wanafunzi watunge sentensi fupifupi kwa kutumia watu wa familia kama: Baba anajenga nyumba; Mama anapika chakula; Dada analima shamba n.k.

Mwalimu asisitize umuhimu wa kuzingatia upatanisho wa kisarufi na ngeli ili kuepuka makosa ya viambishi. Kwa mfano: *ng’ombe inazaa* badala ya *ng’ombe anazaa*.

Hatua ya 5:Tahajia na matamshi bora

Hii ni sehemu muhimu sana. Mwalimu atumie sehemu hii kufundisha matamshi na maendelezo ya maneno kwa sauti ya Kiswahili sanifu. Atumie fursa hii kuhimiza mazungumzo na kuandika. Hii ndio fursa ya kuboresha mwandiko sio matamshi pekee. Atumie mabango na michoro kwa wingi. Pia kama mwalimu wa redio anaweza kupatikana ni vyema zaidi ama rekoda.

Hatua ya 6: Hitimisho

Mwalimu atumie fursa hii kukumbusha mambo yote muhimu katika somo hili. Maswali ya dodosa ni muhimu sana kuhusu nyumba, vifaa vya ujenzi na ujenzi wenyewe licha ya mazingira pamoja na dhima ya kuwa na nyumba.

Mazoezi ya ziada

Licha ya kuwapa wanafunzi wote zoezi, mwalimu awaelekeze wanafunzi dhaifu kwa kuwatengea muda zaidi kwa kutumia mabango na picha kuwashimiza watunge sentensi sahihi kuhusu mabango na michoro hiyo.

Mfano:

Mwalimu : Unaona nini kwenye bango?

Mwanafunzi: Ninaona nyumba ya matofali.

Tathmini

- Mwalimu atumie maswali ya dodosa.
- Ikiwezekana anaweza kuwatoa wanafunzi nje ya darasa ili watazame na kunyoosha vidole kuashiria majengo mbalimbali n.k. Asisitize matumizi ya lugha sanifu na sahihi.

MAJIBU

Zoezi la ufahamu, ukurasa 78

1. Habari
2. Habari ya asubuhi
3. Njema
4. Msonge, mabati na mawe
5. Watoto
6. Babu na nyanya
7. Jirani
8. Kuku, paka, kondoo na bata
9. Mbwa
10. Mazungumzo baina ya mama na baba

Msamiati wa nyumbani, ukurasa 78

1. Nyumba ya msonge, nyumba ya mabati na mawe, nyumba ya matofali na vigae, kasri
2. Matope, vigae, mawe, matofali, mabati
3. Wazazi, watoto, nyanya na babu
4. Ng'ombe, mbuzi, kuku, paka, kondoo, bata na mbwa

Zoezi la msamiati wa nyumbani, ukurasa 79-80

1. Ng'ombe, kuku, paka, mbwa, ngamia, farasi, bata, kondoo mionganini mwa wengine.
2. a) Ndege
b) Ndege
c) Ndege
d) Mnyama

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

3. Mbwa
4. Ng'ombe, mbuzi
5. Kuku, bata
6. Nyasi
7. Msonge, mabati na mawe
8. Ng'ombe

Zoezi la 1, ukurasa 81

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi.

Mwalimu licha ya kuwaacha wanafunzi kutoa mawazo yao kwa njia huru, atathmini hoja za wanafunzi na kuondoa fikra hasi. Kwa mfano: kudhani maskini ndio huishi nyumba za nyasi ama manyata n.k.

Zoezi la mjadala, ukurasa 81

Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi.

Zoezi la 1 ukurasa 83

Mwalimu atathmini usahihi wa majibu ya wanafunzi.

Zoezi la 2, ukurasa 83

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Awape wanaomaliza haraka zoezi jingine na wale wanyonge apitie nao zoezi.

Hali hii itumike katika maswali ya marudio na mjadala.

Vifaa mbalimbali vinavyopatikana nyumbani

Muda:Vipindi 2

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi maelezo chini ya michoro.
- Kusoma kwa makini maagizo.
- Kutaja vifaa mbalimbali vinavyopatikana nyumbani.

Mifano: sahani, kijiko, sofa, runinga, dari, mlango nk

b) Vifaa vya kujifunzia

- Michoro au picha katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 84.
- Magazeti
- Vitu dhahiri: vijiko, vikombe, kochi katika ofisi, kiti cha mwalimu, dawati n.k.
- Mabango

Utaratibu wa somo

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu aanze kwa kuwakumbusha wanafunzi somo lililotangulia. Mwalimu aulize maswali ya dodosi. Kisha awaelekeze wanafunzi kufasiri michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 85. Mwalimu atumie vitu dhahiri. Anaweza kupanga mapema ili kila mwanafunzi abebe kifaa kimoja kimoja na kuja nacho shulenii. Atahadhari wanafunzi wabebe vifaa vidogo vinavyobebeka kwa urahisi tu na visivyo hatari kama vile visu na vingine. Azingatie wanafunzi wasio na uwezo wa kuona ama kusikia ili wote washiriki kwa kugusa, kunusa ama kuigiza umbo la chombo kwa kutumia ishara. Wanafunzi wanaweza kujipanga kwa vikundi vidogo vidogo na kuelezana kuhusu vifaa vyao. Kwa mfano: kazi ya mwiko ni ipi? Kijiko kimetengenezwa kwa nini? Mwalimu

azingatie muda. Wanafunzi waimbe wimbo wa vifaa vya nyumbani katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 85.

Hatua ya 2: Kusikiliza na kuzungumza

Mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja na kueleza kazi mbalimbali za vifaa vya nyumbani na sehemu mbalimbali za nyumba. Awaongoze katika kujieleza kuitia sentensi sahihi za Kiswahili ili kukuza umilisi wao. Awaeleze kuwa kila kifaa ni muhimu. Pia awashauri kujua kuwa vifaa vingine ni ghali na vinahitaji muda kupatikana na utunzaji wake ni muhimu.

Hatua ya 3: Msamiati wa vifaa na sehemu za nyumba

Mwalimu atumie fursa hii kutathmini iwapo wanafunzi wanajua maana (jina) na matumizi ya vifaa mbalimbali vinavyopatikana nyumbani na sehemu za nyumba kama vile: mlango na dirisha. Awaongoze kutumia wimbo kuhusu vifaa na sehemu za nyumba kama njia ya kutambua matumizi ya kila kifaa. Pia awahimize kutunga sentensi sahihi kubainisha maana na matumizi ya vifaa husika. Hali inaweza kufanyika kwa kuwapanga katika makundi madogo madogo ili waigize kwa njia rahisi kisha mwalimu azunguke akitathmini. Wanafunzi wawili wanaweza kuunda kundi moja.

Hatua ya 4: Ufahamu

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma tena kifungu ‘wimbo’. Mwalimu ahimize kusoma kwa sauti na kwa zamu ili kila mwanafunzi ashiriki na pia kutathmini uwezo wa kutambua na kusoma silabi za Kiswahili wa kila mwanafunzi. Ahimize utamkaji sahihi kulingana na sauti za Kiswahili ili kukuza stadi ya kuzungumza na kusoma. Pia achunguze matumizi ya macho ya wanafunzi wakati wa kusoma. Itamwezesha mwalimu kujua wanafunzi amba wana matatizo ya kuona ama ugumu wa kutambua baadhi ya sauti. Pia atajua iwapo kuna ugumu wa kukumbuka. Mwalimu akosoe kila kosa la matamshi na kusoma papo hapo. Asisitize kusoma na kuhifadhi taarifa akilini kwa ajili ya kuitumia baadaye. Wanafunzi wanaweza kuimba wimbo huo kwa mahadhi yoyote mazuri.

Hatua ya 5: Sarufi - Ngeli ya A-WA

Sarufi ni uti wa mgongo wa kila lugha. Mwalimu awahimize wanafunzi kuhusu umuhimu wa kujieleza kuitia lugha sanifu na sahihi kwa kutunga sentensi katika umoja na wingi kwa kurejelea msamiati wa vifaa vinavyopatikana nyumbani.

Mifano: Baba ameketi kochini.

Kina baba wameketi makochini, n.k

Mwalimu ampe kila wanafunzi fursa ya kutumia nomino ya uhusiano wa kifamilia na kifaa cha nyumbani kutunga sentensi sahihi. Pia mwalimu asisitize kuwa sharti wanafunzi wasome mifano na maagizo vyema kabla ya kushiriki zoezi.

Mwalimu awape wanafunzi zoezi la ziada katika ngeli ya A – WA na kuwaelekeza wanafunzi wanyonge kwa kutumia picha na mabango ama vifaa dhahiri.

Hatua ya 6: Tahajia na matamshi bora

Mwalimu afahamu kwamba hii ni sehemu muhimu ya kufundisha matamshi na uandishi. Atumie fursa hii kuwaelekeza wanafunzi kwa kuandika kwa hati nzuri na zinazosomeka vizuri licha ya kutambua na kusoma sauti ngumu na maneno. Mwalimu anaweza kutumia imla kama mbinu ama zoezi la ziada.

Mifano:

Tamka maneno yafuatayo kwa usahihii.

Ghafla	Gharama	Saa	Zaa	Shamba
Zao	Shaka	Pika	Piga	Pisha

Hatua ya 7: Hitimisho

Hii ni hatua ya mwisho wa somo. Mwalimu aulize maswali ya dodosa na kutathmini kumbukumbu ya wanafunzi kuhusu somo hili ili kujua kama alifikia malengo yake au la kabla ya kuwapa maswali ya marudio.

MAJIBU

Zoezi la utangulizi, ukurasa 84

Stuli, mwiko, paa, mlango, dirisha, kijiko, sebule, makochi, sahani, kikombe, kabati, uma, runinga, redio, godoro, meza, ukuta n.k.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 86

1. Kuleta hewa safi ndani ya nyumba
2. Kitanda
3. Karai
4. Nje ya nyumba
5. Runinga
6. Kochi
7. Mwiko
8. Chumba cha kulala
9. Sebuleni
10. Kijiko

Zoezi, ukurasa 86

1. Stuli, mwiko, mto, mlango, dirisha, kijiko, kochi, karai, sahani, kikombe, kitanda, kabati, uma, runinga, redio, zulia, vitambaa
2. Veranda, paa, dari, sakafu

Zoezi la I, ukurasa 87

1. Kikombe, kijiko, mwiko, sahani, kisu
2. Kitanda, mto
3. Kochi, runinga, meza, kitii
4. Kabati
5. Runinga
6. Dari
7. Mlango
8. Dirisha
9. Kochi
10. Uma

Zoezi la 2, ukurasa 88

1. Kiti/kochi
2. Kijiko
3. Zulia
4. Kikombe
5. Karai
6. Sebule
7. Redio
8. Kitanda
9. Dari/paa

Zoezi la 1, ukurasa 89

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

Zoezi la 2, ukurasa 89

1. Paka atamla panya.
2. Punda alivuta gari.
3. Ng'ombe anakula nyasi.
4. Kuku anataga yai.
5. Bata anaogelea.
6. Mbuzi analala.
7. Kondoo anapiga kelele.
8. Ngamia alisafirisha mtu.
9. Njiwa anapaa angani.
10. Batamzinga anaatamia yai.

Zoezi la Imla, ukurasa 90

Mwalimu amsomee mwanafunzi orodha ya maneno haya ili amsomee mwanafunzi mwenzake naye ayaandike:

- 1.Sebule
- 2.Vitambaa
- 3.Veranda
- 4.Kifaranga
- 5.Ndama

Zoezi la ziada, ukurasa 90

Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi. Ahakikishe kuwa wanafunzi wanazingatia mada ya mjadala.

Mifugo wanaopatikana nyumbani na vivumishi vya ngeli ya A – WA

Muda: Vipindi: 2

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutazama michoro au picha kwa makini.
- Kusoma kwa usahihi maelezo chini ya michoro au picha.
- Kusoma kwa makini maagizo.
- Kutaja wanyama mbalimbali wanaopatikana nyumbani.
- Kutaja kazi ya mifugo mbalimbali wanaofugwa.

b) Vifaa vya kujifunza

- Michoro au picha
- Magazeti
- Mabango
- Vinasa sauti

c) Maandalizi ya somo:

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu aanze kwa kuwakumbusha wanafunzi kuhusu somo lililopita. Mwalimu awaulize maswali ya dodosi. Hatimaye awaelekeze wanafunzi katika kufasiri michoro au picha zilizo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 91 na kuwapa nafasi ya kutoa mawazo yao. Wanafunzi wataje mifugo kulingana na umbo, kazi (faida) zao n.k. Mwalimu anaweza kuwapeleka wanafunzi wake nyanjani kuwaona baadhi ya wanyama. Awaulize maswali kama vile: ‘*Mwanadamu anatofautiana vipi na mbuzi?*’

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi na kuwauliza wazungumzie sifa za mnyama fulani na umuhimu na hasara zake kama njia ya kumtambulisha vyema. Awashirikishe wanafunzi wote hasa wenye taathira mbalimbali.

Hatua ya 2: Kusikiliza na kuzungumza

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua wanyama na sifa ambazo wamepewa. Kwa mfano: ng'ombe mnono - ng'ombe wanono.

Mbali na sifa, wanafunzi waongozwe kueleza umbo, faida na hasara za wanyama wa nyumbani. Pia watumie sifa kama vile: pembe, masikio, mikia n.k. Awape nafasi ya kutoa maelezo zaidi ili kukuza umilisi wao wa kimawasiliano na matamshi. Mwalimu awaeleze wanafunzi kutambua sifa za kiuchumi na kijamii za mifugo wa nyumbani. Matumizi ya michoro na picha ni muhimu.

Hatua ya 3: Msamiati kuhusu mifugo

Mwalimu atumie sehemu hii kuhimiza wanafunzi kuwatambua wanyama wa nyumbani kufuatia milio, mazao yao, umbo na umuhimu wao nyumbani. Awaelekeze kubainisha wanyama wa nyumbani kwa kutunga sentensi sahihi kuwahuusu. Mwalimu akosoe sentensi za wanafunzi na kuwaelekeza katika kutunga sentensi sahihi. Pia awaelekeze kujibu zoezi kikamilifu.

Hatua ya 4: Ufahamu

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma tena sentensi zinazoandamana na michoro. Mwalimu atumie sehemu hii kupima matamshi na uwezo wa kusoma kwa sauti sahihi za Kiswahili na kuelewa wanachosema. Mwalimu afafanue maneno katika ngeli ya A – WA. Achunguze namna wanapitisha macho wakati wa kusoma ili kubaini uwezo wa kusoma na kutamka barabara. Pia mwalimu atathmini ugumu wa wanafunzi wa kutamka na kuwaelekeza barabara. Hatimaye, awaongoze katika kujibu zoezi.

Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 92

Maneno yaliyopigwa mstari ni:

1. Nomino: ngamia, mbwa, kondoo na paka.
2. Vivumishi: mkubwa, mkali, mchanga na mjanja.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika namna ya kutumia kamusi kutafuta maana ya nomino walizotaja awali.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 92-93

1. Baba na mama
2. Ng'ombe
3. Wanono
4. Punda
5. Mkubwa
6. Ngamia
7. Mkali
8. Mwembamba
9. Mmoja
10. Yeye (mbuzi)

Zoezi la makundi, ukurasa 93

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

Zoezi, ukurasa 93

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi.

Zoezi la 1, ukurasa 94

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi na kuwaelekeza vilivyo.

Zoezi la 2, ukurasa 94

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu vimilikishi na kuwaelekeza vilivyo.

Zoezi la 3, ukurasa 95

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi ili kutambua usahihi wa sentensi hizo.

Mazoezi ya ziada

Hili ni muhimu kwa wanafunzi wanyonge. Mwalimu anastahili kuipa sehemu hii umuhimu mkubwa. Wanafunzi wote hawalingani. Wanafunzi werevu wanaweza kupewa kazi ya ziada kama maswali ya marudio wakati yeye anawashughulikia wanafunzi dhaifu kupitia somo hili tena.

Mwalimu awaulize wanafunzi watafute maana za maneno yafuatayo na baadaye wayatungie sentensi sahihi:

- a) Wafugaji
- b) Mizigo
- c) Kuwinda
- d) Njiwa

Tathmini

Kuna njia nyingi za mwalimu kutathmini wanafunzi kutegemea uwezo wa wanafunzi wake. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali na kwa utaratibu fulani ili kutathmini uelewa wao wa somo. Anaweza kuwaomba wanafunzi wataje majina ya watu wa familia, mifugo na kutunga sentensi zenyet majina katika ngeli ya A – WA kwa kutumia vivumishi na viashiria pamoja na viulizi. Pia mwalimu abuni kazi ya ziada pale ambapo anashuku kwamba bado kuna utepetevu mionganoni mwa wanafunzi wake. Kutumia vikundi kutamfaidi sana mwalimu kwa kuwaruhusu wanafunzi kujifunza kutoka kwa wenzao.

Hatua ya 5: Sarufi

Sarufi ni muhimu na mwalimu awakumbushe wanafunzi umuhimu huu. Mwalimu awafafanulie wanafunzi maana ya vivumishi. Awaeleze kuwa kivumishi ni neno la sifa na hueleza zaidi kuhusu nomino.

Mfano: Mbuzi **mchanga, mkubwa, mnono** n.k.

Mwalimu awahimiza wanafunzi kutunga sentensi zao sahihi kwa kutumia watu na mifugo wanaopatikana nyumbani.

Mfano: Kaka anachunga ng'ombe mweusi. Mwalimu ampe kila mwanafunzi fursa ya kutumia mnyama mmoja na mtu wa familia katika sentensi. Mwalimu atahadhari kuhusu jinsia na usawa wa kutunga sentensi zinazodunisha ama kubagua kwa njia yoyote. Hatimaye awaelekeze wanafunzi kujibu mazoezi ipasavyo na kukosoa kazi ya wanafunzi.

Hatua ya 6:Tahajia na matamshi bora

Sehemu hii ina umuhimu sana kwa kufundisha matamshi na kuboresha mwandiko wa wanafunzi. Mwalimu atilie mkazo sehemu hii.

Hatua ya 7: Hitimisho

Huu ni mwisho wa somo na mwalimu anastahili kutumia fursa hii kutathmini iwapo wanafunzi wake walielewa somo au la. Atumie muda huu kurekebisha sehemu ambazo ni dhaifu kwa kutoa mazoezi ya ziada kwa wanafunzi wanyonge na kazi zaidi kwa wanafunzi werevu.

Majina yanayohusishwa na watu na uhusiano wao kijamii pamoja na vivumishi vyta ngeli ya A-WA

Muda: Vipindi 2

Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kuwataja watu wote wa kifamilia wanaopatikana nyumbani.
- Kufasiri michoro au picha kikamilifu.
- Kusoma kwa makini, ufasaha na kwa usahihi.
- Kusoma na kuelewa maagizo vyema.

d) Vifaa vya Kujifunza

- a) Michoro na picha
- b) Mabango
- c) Magazeti
- d) Fanani au wanafunzi wenywewe

Hatua ya I: Utangulizi

Mwalimu awakumbushe wanafunzi kuhusu somo la awali. Awaulize maswali rahisi nao wayajibu. Awakumbushe masuala muhimu yanayohusu ngeli ya A – WA na vivumishi ambavyo wamesoma tayari. Kisha awaelekeze katika kutafsiri michoro au picha huku akiwaacha watoe mawazo yao huru naye akiyanakili kwenye ubao mawazo yao ili aulize maswali ya kufuatisha kwa lengo la kuchochea mazungumzo zaidi. Awaelekeze wanafunzi kutunga sentensi sahihi pamoja na vivumishi vilivyoonyeshwa: viulizi na vionyeshi. Hatimaye awaelekeze kusoma na kuigiza mazungumzo baina ya kaka na dada.

Mwalimu afafanue uhusiano uliopo baina ya kaka na dada yake. Pia achunguze iwapo kuna maneno yanayowatatiza wanafunzi na kuwaelekeza ipasavyo. Wanafunzi wanaweza kuigiza kwenye makundi ya wanafunzi wawili wawili hata watatu. Mmoja anaweza kuigiza kama hadhira ama mwelekezi na kuwasikiliza waigizaji.

Hatua ya 2: Kusikiliza na kuzumgumza

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma tena sehemu ya utangulizi (michoro) na hatimaye mazungumzo baina ya kaka na dada. Mwalimu hatimaye anaweza kuwaelekeza wanafunzi wake wajipange kwenye vikundi vya kuigiza mazungumzo. Mwalimu ahakikishe kuwa sio wanafunzi wa kike au wa kiume tu ndio wanaigiza kulingana na wahusika walijotajwa. Mwalimu azuie tabia zote za kibaguzi kwa wanafunzi wenye taathira. Pia ahakikishe wanapewa nafasi ya kuigiza vilivyo.

Mwalimu amakinike katika makosa yote ya matamshi ya wanafunzi na kuyakosoa. Haya ni mambo yanayohitaji kukosolewa papo kwa hapo.

Hatua ya 3: Msamiati

Umilisi wa msemaji wa lugha yote unategemea wingi wa msamiati alionao katika lugha husika. Hii ni sehemu muhimu kwani mwalimu hana budi kuwa mvumilivu wakati wa kuwaongoza wanafunzi kufahamu maana na matumizi ya maneno. Mbali na kutamka, mwalimu anastahili kuwaelekeza wanafunzi kutungia msamiati mpya sentensi fupifupi na rahisi kama njia ya kujifahamisha na miktadha ya matumizi na kufahamu zaidi. Wanafunzi katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili wanaweza kuulizana maswali kwa kutumia watu wa familia na vivumishi viulizi na viashiria.

Mifano:

1. Huyu ni nani?
2. Yule ni nani?
3. Dada yupi?
4. Mama gani?
5. Kaka huyu wake.
6. Babu yule wangu.

Hatimaye, awaongoze kuelewa vivumishi ambavyo vimetumika katika sentensi na kutunga sentensi zao wenyewe kwa kufuata mifano iliyo katika *Kitabu cha Wanafunzi*, ukurasa 100-101. Mwalimu atoe zoezi la ziada kwa wanafunzi walikuwa na ugumu wa kutunga sentensi kwa kutumia vivumishi husika.

Hatua ya 4: Ufahamu

Ufahamu ni muhimu katika kufundisha stadi za kusoma: kusoma kwa sauti na hatimaye kusoma kimya kimya kwa kujitegemea. Mwalimu ana fursa nzuri ya kuwashirikisha wanafunzi wote katika ushirikiano wa kusoma kwa zamu na pia kuwalinganisha bila kutegemea rangi, jinsia ama tabaka.

Hatimaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujibu maswali ya ufahamu, pia atathmini iwapo wanafunzi wanazidi kuimarika katika uwekaji wa taarifa na kuitumia baadaye kwa njia ya kukumbuka walichokisoma awali.

Hatua ya 5: Sarufi

Kufikia sasa, wanafunzi wameifahamu ngeli ya A – WA na hata vivumishi mbalimbali. Mwalimu achukue fursa hii kuwakumbusha vivumishi vya sifa, vimilikishi na hatimaye atoe mazoezi zaidi kwa vivumishi viulizi na viashiria. Aidha asisitize matumizi bora ya viambishi vya ngeli katika umoja na wingi pamoja na vivumishi viashiria na viulizi.

Mifano:

1. Kaka huyu wake ni mzuri.
2. Mama yupi analima shamba?
3. Dada gani anasoma vyema?
4. Huyu babu analala n.k.

Hatimaye awaelekeze wanafunzi kufanya mazozi katika sehemu hii na kuwakosoa wanafunzi.

Hatua ya 6: Tahajia na matamshi bora

Hii ni sehemu muhimu ambayo mwalimu anatakiwa kutumia kufundisha matamshi ya sauti tata za Kiswahili pamoja na hati nzuri ya wanafunzi wake. Mwalimu atumie abjadi (alfabeti) kuwasaidia wanafunzi wanyonge kujikumbusha matamshi ya sauti ngumu kwao kwa msaada wa irabu.

Mfano:

g na gh

kh na k

sh na s

Mwalimu awakumbushe wanafunzi kuwa hili ni tukio na zoezi ambalo huendelea kwa muda wote wa kujifunza lugha yoyote ile hata zile wanafunzi wazijuazo tayari: kama

lugha ya mama n.k. Mwalimu abuni msamiati zaidi na kuwauliza wanafunzi kutamka na kuandika (imla)

Hatua ya 7: Hitimisho

Mwalimu anaweza kuhitimisha kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodosa pamoja na kuwaongoza kufanya mazoezi kwa kujitegemea ili kutathmini uwezo wa kila mwanafunzi katika ufahamu wake wa somo hili. Mwalimu anaweza kutumia mbinu kama kujibu, kuuliza maswali, kuandika na kukumbuka habari fulani inayohusiana na somo kabla ya kuhitimisha kwa kuleta mawazo yao yote pamoja.

E. Mazoezi ya ziada

Mazoezi haya yawalenge wanafunzi wanyonge ili kuwasaidia kumudu somo kama wanafunzi werevu. Mwalimu anaweza kuwapitisha kwenye somo hili tena ama kwa njia ya kubuni zoezi jipya.

F. Tathmini

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali ya kutathmini ufahamu wa wanafunzi. Pia anaweza kuwaongoza kufanya zoezi pekee yao. Kisha asahihishe kwa lengo la kutathmini kufanikiwa kwa somo lake. Pia anaweza kuwauliza wanafunzi wajiuilize maswali wenyewe kwa wenyewe na wajibu. Zoezi la kuandika linaweza kutumiwa na mwalimu, kwa mfano kushiriki katika uandishi wa imla. Mwalimu anaweza kuwaonyesha wanafunzi vitu na wanafunzi wataje nomino ama kinyume chake. Mwalimu atumie mbinu ambayo anadhani inafaa sana kwa kiwango cha wanafunzi wake.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 98-99

1. Kaka
2. Ule
3. Sebule
4. Huyo
5. Ule
6. Yupi
7. Deki
8. Tom
9. Lile
10. Gani

Zoezi la kuigiza, ukurasa 99

Mwalimu atathmini maigizo ya wanafunzi na kuwaelekeza katika kufikia malengo ya somo.

Zoezi la msamiati, ukurasa 99

Mwalimu atathmini usahihi wa sentensi za wanafunzi. Asahihishe na kuwapa mwongozo ufaao.

Zoezi la 1, ukurasa 101

Mwalimu atathmini mifano ya wanafunzi na kuwaelekeza vyema. Pia asahihishe na kukosoa mifano isiyo sahihi.

Zoezi la 2, ukurasa 102

1. Kivumishi kimilikishi
2. Kivumishi cha sifa
3. Kivumishi cha sifa
4. Kivumishi kiashiria
5. Kiashiria (hii), kimilikishi (yake)
6. Kivumishi cha sifa
7. Kivumishi kiashiria
8. Kivumishi kiulizi
9. Kivumishi kiulizi

Zoezi la ziada, ukurasa 102

1. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi na kuwaelekeza zaidi.
2. a) Ng'ombe amezaa.
 - Kaka yangu mkubwa.
 - Mbuzi huyu wangu.
 - Mlango huu ni mpana.
 - Nyumba ndogo imejengwa.

Uhusiano wa kifamilia pamoja na vivumishi vya ngeli ya A-WA

Muda:Vipindi 2

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kuwataja watu wenyewe uhusiano wa kijamaa wanaopatikana nyumbani
- Kufasiri michoro au picha
- Kusoma kwa makini, usahihi na kwa ufasaha maelezo yanayoandamana na michoro au picha
- Kusoma na kuelewa maagizo
- Kujibu mazoezi kikamilifu.

b) Vifaa vya kujifunza

- Michoro au picha
- Magazeti
- Wanafunzi wenyewe
- Mabango

c) Utaratibu wa somo

Hatua ya I: Utangulizi

Somo hili linashughulikia kipengele cha sarufi kinachohusiana na ngeli ya A-WA na vivumishi vyote vilivyofundishwa. Hili ni hitimisho la msamiati wote wa mazingira ya nyumbani uliofundishwa katika masomo yaliyotangulia.

Mwalimu anashauriwa atumie somo hili kutathmini kwa ujumla iwapo ufundishaji wa msamiati wa nyumbani ulifanikiwa au la.

Mwalimu atumie fursa hii kuitia msamiati wa vifaa vya nyumbani, watu wanaopatikana nyumbani, aina za nyumba na vifaa vinavyozijenga, mifugo pamoja na vivumishi vya sifa, vimilikishi, vionyeshi na viulizi katika ngeli ya A – WA. Mwalimu anaweza kuwagawa wanafunzi katika makundi na kuwaongoza waulizane maswali na kuyajibu. Mwalimu aelegeze mkondo wa maswali na majibu. Atathmini matamshi, usomaji na ufahamu. Wakati huo asisitize matumizi ya ngeli ya A – WA. Kisha awaelekeze wanafunzi kufasiri michoro na kuigiza mazungumzo baina ya mzazi na mtoto.

Hatua ya 2: Kusikiliza na kuzungumza

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma na kuigiza mazungumzo baina ya mzazi na mtoto. Akosoe makosa yote ya kimatamshi, kusoma kwa kusitasita pamoja na uachaji wa baadhi ya sauti, silabi au maneno wakati wa kusoma. Mwalimu awapange wanafunzi katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili kisha awaelekeze wasome na kuigiza huku wakielekezana na kukosoana wao wenyewe kwa mwongozo wa mwalimu.

Hatimaye, mwalimu awaongoze wanafunzi katika kufasiri michoro na wahusika katika mazungumzo. Mwalimu ahimize kujieleza kwa kuzingatia matamshi sahihi ya sauti za Kiswahili, viambishi vya ngeli na msamiati unaofaa kulingana na somo.

Hatua ya 3: Msamiati

Mpaka sasa utaratibu wa kufundisha msamiati umezoeleka. Mwalimu achukue fursa hii kuwataka wanafunzi kutaja iwapo wanakumbuka msamiati mbalimbali katika jumla ya msamiati wa mazingira ya nyumbani. Kisha awaongoze wanafunzi kuitia zoezi la msamiati. Awashirikishe wanafunzi wote na kuhimiza kwamba wanukuu maneno mapya ndani ya madaftari yao.

Hatua ya 4: Ufahamu

Mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kushirikiana katika kutafuta majibu kwa maswali ya ufahamu. Mwalimu akosoe makosa yote ya kauli ama majibu ambayo sio sahihi. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wa jinsia zote, wenye taathira mbalimbali. Awape wanafunzi werevu kazi zaidi na atunge zoezi la ziada

kwa wanafunzi wale wanyonge. Anaweza kuashiria michoro na kuwataka wataje kinachoashiriwa. Pia imla inaweza kufaa katika kipindi hiki. Mwalimu atue maneno na kuwasomea wanafunzi ili wayaandike kwa hati nzuri na kwa maendelezo sahihi hasa sauti zinazotatanisha.

Hatua ya 5: Sarufi

Mwalimu awaongoze wanafunzi kupitia mazoezi yote ya kisarufi na kutathmini matumizi sahihi ya ngeli ya A-WA pamoja na vivumishi vya ngeli hii vilivyofundishwa. Akosoe makosa yote ya kisarufi na matumizi mabaya ya vivumishi. Mwalimu anashauriwa kubuni mazoezi zaidi hasa kwa wanafunzi werevu. Aidha kutunga mazoezi ya ziada kwa wanafunzi wanyonge.

Hatua ya 6: Tahajia na matamshi bora

Msamiati ambao umetumika kwa wingi ni ule wa mazingira ya nyumbani. Mwalimu atumie fursa hii kutilia mkazo sehemu ambazo ziliwatatiza wanafunzi katika uelewa.

Hatua ya 7: Hitimisho

Mwalimu aulize maswali na kuwashauri kuwa wanafunzi wafanye maswali ya marudio kupima umilisi wao wa somo zima. Mwalimu asahihishe kazi za wanafunzi na kuwapa mwongozo wa kujiiamarisha katika somo lijalo. Awapongeze wanaofanya vyema na kuwahimiza wale wanyonge kujikaza kwa kuwapa tumaini bila kuwadhalilisha.

E. Zoezi la ziada

Mwalimu abuni zoezi la ziada kwa wanafunzi wanyonge. Atumie picha zaidi na michoro. Kama anaweza kupata vifaaa dhahiri atumie: kwa mfano bidhaa kama sahani, vikombe, sufuria na vijiko n.k. Mwalimu awape wanafunzi mianzo ifuatayo ya sentensi ili wazikamilishe kwa maneno mwafaka:

- a) Kaka yangu _____.
- b) Mama yetu _____.
- c) Mjomba wao _____.
- d) Binamu huyu _____.
- e) Babu yule _____.

F. Tathmini

Mwalimu awaulize wanafunzi kutaja na kuorodhesha msamiati wa nyumbani katika vikundi vidogo na hatimaye mwanafunzi binafsi. Pia atumie imla kuwataka wanafunzi kutumia muda mfupi kutaja ama kueleza dhana fulani inayotokana na msamiati wa nyumbani. Pia anaweza kuwahimiza wanafunzi kuuliza maswali kutokana na somo na kisha kutoa majibu. Mwalimu akadirie kila jibu na swali kisha kutoa kauli yake kwa wanafunzi bila kuwadhalilisha.

MAJIBU

Zoezi la ufahamu, ukurasa 106

- a) Nyanya
- b) Shangazi
- c) Bavyaa
- d) Kitukuu
- e) Babu

Zoezi la kuigiza, ukurasa 108

Mwalimu atathmini vitendo vyta wanafunzi.

Zoezi la utafiti, ukurasa 108

Mwalimu atathmini kazi ya wanafunzi na kutoa mwongozo ufaao.

Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 108

1. Mzazi na mtoto
2. Mutoni
3. Nzuri
4. Jirani
5. Matusi
6. Uadui
7. Pole baba
8. Amani

9. Kaka
10. Mbuzi na ng'ombe

Zoezi la mjadala, ukurasa 108

Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi.

Zoezi la ubunifu, ukurasa 109

Mwalimu awahimize wanafunzi kuwa wabunifu. Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi.

Zoezi la sarufi, ukurasa 109

1. a) Yetu
b) Yangu
c) Wako
d) Wake
e) Yenu
2. d, e, h, g, i, j
3. Mwalimu atathmini majibu ya mwanafunzi.
4. a) Gani
b) Yupi
c) Yupi
d) Kipi
e) Yupi/gani

Zoezi la tahajia, ukurasa 111

Mwalimu atathmini kazi ya wanafunzi.

Mada Kuu: Msamiati wa Mazingira Mbalimbali

Mada Ndogo: Msamiati wa Mazingira ya Utawala

Idadi ya vipindi: 10

Ujuzi upatikanao katika mada hii:

- Kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa makini matini zinazojitokeza katika mazingira ya utawala.
- Kutumia msamiati unaohusika katika sentensi fupi fupi kwa kuzingatia majina ya ngeli ya *U-I* na *I-ZI*.

Malengo ya kujifunza:

Uhusiano wake na Masomo Mengine:

- *Jiografia* kwa kutoa ramani ya Rwanda ikionyesha maeneo ya kiutawala, ramani ya Afrika ikionyesha Rwanda katika Afrika ya Mashariki pamoja na nchi jirani zake.

Vifaa vya Kujifunzia:

- Ramani ya Rwanda inayoonyesha maeneo ya kiutawala
- Ramani ya Afrika
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 114
- Vinasasauti

Kigezo cha Tathmini na Upimaji:

- Uwezo wa kuhusisha mahali au kitu na pembe nne za dunia; kueleza maeneo ya kiutawala na nembo za taifa.
- Uwezo wa kutumia kwa usahihi siku za wiki na miezi katika mawasiliano rahisi na kuzingatia matumizi sahihi ya majina ya ngeli ya *U - I* na *I - ZI*.

Maelezo kwa Mwalimu:

a) Utangulizi wa Mada

Mada hii inashughulikia msamiati wa mazingira ya utawala. Kwa hivyo, majina ya mikoa, wilaya, tarafa, kata na viji ni mbalimbali, nchi zinazopakana na nchi ya Rwanda yamezungumziwa katika mada hii. Vilevile, baadhi ya nembo za taifa, miradi mbalimbali ya kimaendeleo, ya kudumisha amani na maisha mema kwa wananchi nayo imezungumziwa kama njia muhimu ya kutambulisha uongozi bora uliopo. Mbali na hayo, mada hii imebainisha pia matumizi ya ngeli za *U-I* na *I-ZI* pamoja na vivumishi mbalimbali vinavyoambatana. Katika ujifunzaji wa masomo yaliyoandalowi katika mada hii, ni vyema mwalimu azingatie hapo mwanzoni kwamba uzalendo ndilo jambo msingi katika mafunzo yoyote kwa wananchi.

Kwa hivyo, mwalimu amsaidie mwanafunzi kukuza uwezo wake wa kuelewa mambo kadhaa yapatikanayo katika shughuli za kiutawala na za uongozi bora wa nchi yake ili aweze kujivunia uraia wake. Nafasi ya ushirikiano mionganini mwa wananchi na raia wengine katika nchi za Afrika Mashariki na hata nchi za kiafrika kwa jumla ni muhimu idhihirishwe ili kumjenga mwanafunzi Mnyarwanda kujihisi alivyo na uwezo wake wa kutoa mchango katika ujenzi wa taifa lake. Mwanafunzi aelekezwe katika uchunguzi wa juhudini na miradi mbalimbali inayofanywa katika kudumisha amani na kujenga taifa lenye uwezo wa kujitegemea na mshikamano na mataifa mengine katika Afrika Mashariki na hata barani kote. Mwanafunzi asaidiwe kujivunia kuwa Mnyarwanda mwenye matarajio mema na mwenye uwezo wa kusuluhisha matatizo yanayoweza kujitokeza ili kudumisha amani na kutoa mchango wake katika miradi mbalimbali ya kimaendeleo kwa wananchi wote.

Dhana muhimu zinazojitokeza katika mada hii ni pamoja na *nchi*, *taifa*, *nembo za taifa*, *eneo*, *kijiji*, *kata*, *tarafa*, *wilaya*, *jimbo*, *mkoa*, *uongozi*, *utawala*, *halmashauri*, *viongozi*, *raia*, *mwananchi*, *miradi*, *maendeleo*, *bendera*, *ramani*, *wimbo wa taifa*, *chama cha ushirika*, *msimu*, *bima*, *ngeli*, *sarufi* na sentensi.

Masuala Mtambuka

- Amani na maadili
- Usawa wa kijinsia
- Elimu ya pamoja
- Elimu kuhusu fedha
- Mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo
- Utamaduni wa kiusanifishaji
- Masomo ya ujinsia na uzazi

b) Ujuzi wa jumla

- Usuluhishaji wa matatizo
- Mawasiliano katika lugha rasmi
- Stadi za utafiti
- Ubunifu na ugunduzi
- Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha
- Ujifunzaji wa muda mrefu

Somo la Kwanza

Nchi yangu

Muda: Vipindi 4

a) Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi
- Kutambua na kuonyesha kwenye ramani mahali ambapo Rwanda inajitokeza
- Kudhihirisha nchi zinazopakana na Rwanda
- Kuonyesha majimbo na sehemu mbalimbali za nchi
- Kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati wa mazingira ya utawala
- Kutumia majina ya ngeli ya *I - ZI* pamoja na vivumishi vinavyoambatana

b) Vifaa vya kujifunzia

- Michoro ya ramani ya nchi ya Rwanda, na chati yenyenye mchoro wa dira
- Vifaa mbalimbali kama vile kitabu cha mwanafunzi, ubao, rula, kifutio, chaki na kadhalika
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

c) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu msamiati wa mazingira ya utawala na linatarajia hasa kuitambulisha nchi ya Rwanda. Kwa hivyo, mwalimu ajaribu kuleta vifaa mbalimbali na atumie michoro tofauti inayoweza kusaidia wanafunzi kuelewa kwa urahisi. Mwalimu atumie kwa mfano ramani ya nchi ya Rwanda yenyenye kudhihirisha wazi mipaka ya mikoa na wilaya, mchoro wa wilaya moja unaodhihirisha maeneo mengine kama vile tarafa na mchoro wa dira. Vilevile, ni vyema mwalimu azingatie wakati unaofaa kwa kuonyesha hadharani vifaa alivyovileta ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa vizuri, ni lazima mwalimu atafute

mifano ya kutosha katika maeneo ambayo wanafunzi wanayafahamu. Katika somo hili, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli inayohusika.

d) Utaratibu wa somo

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuwauliza maswali ya dodoso nao wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu alichangamshe darasa lake kwa kuwauliza maswali kuhusu michoro iliyoko katika kitabu cha mwanafunzi huku akilenga kuwaelekeza kubainisha mipaka ya nchi ya Rwanda, mikoa yake na wilaya zilizopo. Wanafunzi nao wajibu maswali ya mwalimu wao kupitia yale wanayoyaona katika michoro iliyopo.

Hatua ya 2: Kusoma na kufahamu

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha habari kinachohusika kwa kuandika msamiati mpya wanaokutana nao. Wanafunzi, kwa upande wao, wasome kwa kimya pamoja na kuandika msamiati huo mpya katika madaftari yao. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wamesoma kwa kimya kama ilivyotakikana, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu cha habari wanapomaliza kukisoma. Kwa mfano, anaweza kuwauliza maswali yafuatayo: *Ni nani anayezungumza katika kifungu hiki cha habari? Nchi yake ni ipi?* Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliiyoyasoma katika kifungu hicho. Kwa mfano: *Ni Munezero anayezungumza katika kifungu hiki cha habari. Nchi yake ni Rwanda.* Baada ya kupata picha ya uelewa wa jumla wa wanafunzi kuhusu kifungu kinachohusika, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa sauti kifungu hicho. Wanafunzi wasome kulingana na maelekezo ya mwalimu. Katika hatua hii ya somo, ni lazima mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi mara moja wanapofanya makosa.

Hatua ya 3: Ujifunzaji wa msamiati

Mwalimu apange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba watafute maana za msamiati mpya waliokutana nao huku wakizingatia jinsi ulivyotumiwa katika kifungu walichokisoma. Mwalimu awaombe wanafunzi kutumia kamusi pale wanapohitaji na azunguke darasani kuelekeza wanaotatizika katika kuitumia kamusi hiyo. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma sentensi walizopewa na kujadiliana kuhusu maana za msamiati uliopigiwa misitari ili waweweze kutunga sentensi zao wenye. Ni vyema mwalimu azunguke pia darasani ili kusaidia na kuelekeza wanafunzi. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja zoezi hilo la msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliopo, mwalimu achukue

fursa hii kuuliza kama kuna msamiati wowote ambao haujaeleweka ili maana yake ijadiliwe kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika kifungu cha habari walichokisoma. Katika hatua hii ya ujifunzaji wa msamiati, ni lazima mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio unasaidia wanafunzi kupata ujuzi unaotakikana kuhusu tafakuri tunduizi, ubunifu na ugunduzi, stadi za utafiti na mawasiliano katika lugha rasmi. Kwa hivyo, kupitia mifano iliyopo, mwalimu awaelekeze ili waweze kutunga sentensi zenye maana kulingana na ujuzi unaotarajiwa.

Hatimaye, mwalimu atoe maelekezo kuhusu zoezi la pili la msamiati ambapo atawaomba wanafunzi wake kuchunguza picha na michoro iliyopo katika kitabu cha mwanafunzi ili waweze kuihusisha na sentensi fupifupi walizotolewa. Wanafunzi wajadiliane katika makundi yao ya wanafunzi watatu watatu na kufanya zoezi hilo kikamilifu. Mwalimu azunguke darasani kuhakikisha kuwa hakuna mwanafunzi anayetatizika katika kuyajibu maswali ya zoezi hilo. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote kusahihisha zoezi hilo. Kupitia picha na michoro iliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanajua wimbo wa taifa kwa kuwaomba waimbe wimbo huo, kutoa mifano mbalimbali ya shughuli za kimaendeleo, kubainisha shughuli zinazofanywa katika kazi za pamoja za wananchi *umuganda* na kadhalika.

Hatua ya 4: Matumizi ya lugha

Katika hatua hii ya matumizi ya lugha, mwalimu awaombe kwanza wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu ili waweze kujadiliana kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa katika vijiji vyao na ambazo zinachangia katika maendeleo ya vijiji hivyo na hata nchi nzima. Wanafunzi wajadiliane kuhusu shughuli hizo na mwalimu azunguke darasani ili kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kujitokeza mbele ya wenza ili kuwaelezea shughuli hizo. Wanafunzi wengine waulize maswali kuhusu shughuli hizo na wachangie na wenza tajriba za vijiji vyao kuhusu shughuli hizo. Kuhusu zoezi la pili, mwalimu awaambie wanafunzi wajipange katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujibu maswali yaliyopo. Wanafunzi wajigawe kama walivyoelekezwa na mwalimu wao na kujibu zoezi hilo kuhusu uongozi na maeneo mbalimbali. Mwalimu awaombe wanafunzi kujibu kwa pamoja zoezi hilo ambapo kila kundi linajitokeza mbele ya wenza na kuwaelezea yale waliyoyajibu. Katika kuwaelekeza wanafunzi hawa, mwalimu awaombe kutoa majibu yote yanayowezekana katika makundi yao kwani majibu huweza kutofautiana kulingana na maeneo ambapo wanafunzi wanatoka. Hali kadhalika, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kusoma dira. Awape mwelekeo kuhusu pembe za Dunia, msamiati wa siku za wiki, miezi ya mwaka na usomaji wa kifungu kuhusu miezi ya mwaka.

Hatua ya 5: Sarufi (Ngeli ya I-ZI)

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kusoma sentensi zilizopo ili waweze kuchunguza na kujadiliana kuhusu sifa za vifungu nya maneno vilivyopigiwa mistari. Wanafunzi wajigawe kama walivyoambiwa na mwalimu wao na kusoma kwa pamoja huku wakichunguza sifa za vifungu vilivyopigiwa mistari katika sentensi hizo. Mwalimu awaombe wanafunzi kulinganisha miundo ya vifungu vilivyopigiwa mistari katika sentensi zote kuitia mfano uliopo katika kitabu cha mwanafunzi huku akilenga kubainisha kuwa viambishi nafsi katika nafsi ya tatu huweza kubadilika kulingana na jina kiima lililotumiwa. Arejelee mifano ya majina ya watu ambayo ndiyo wanafunzi wameyazoea katika nafsi ya tatu ili wanafunzi watambue mabadiliko yanayofanywa katika muktadha ambapo majina hayo hubadilika. Kutokana na mfano kama ; *Mwalimu anaandika* anaweza kubadilisha jina *mwalimu* na kuweka *kalamu* ambapo kiambishi a kitabadilika na kuwa i katika sentensi *Kalamu inaandika*.

Hivyo basi, mwalimu awaombe wanafunzi wake kuchunguza majina yaliyotolewa katika mifano iliyopo na ambayo yana kiambishi nafsi i katika kitenzi. Halafu, awaombe wanafunzi kuchunguza wingi wa mifano iliyotolewa katika zoezi la pili la sehemu ya sarufi. Ili wanafunzi waweze kuelewa ipasavyo, anaweza kutumia njia aliyoitumia hapo juu kwa kutangulia na wingi wa majina ya watu ambapo atazingatia mfano kama ; *Walimu wanaandika* na *Kalamu zinaandika* kwa kutilia mkazo mabadiliko ya jina *walimu* na *kalamu* ambayo yanaathiri matumizi ya nafsi wa kuhusu *walimu* na zi kuhusu wingi wa *kalamu*. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi kuandika wingi wa sentensi zilizopo katika zoezi la pili ili waweze kutafakari kuhusu sifa za majina yanayotumia viambishi nafsi i katika umoja na zi katika wingi. Ili kuhakikisha ikiwa wanafunzi wameshaelewa matumizi ya ngeli hii ya *I-ZI*, ni vyema mwalimu awaombe kutafuta mifano mingine yenye sifa hizo katika kifungu walichokisoma kuhusu *nchi yangu* kama wanavyoelezewa katika zoezi la tatu.

Aidha, mwalimu awaombe wanafunzi kuchunguza sentensi zilizopo katika zoezi la nne na kubainisha sifa za maneno yaliyopigiwa mistari. Mwalimu azingatie kwamba maneno hayo yaliyopigiwa mistari ni vivumishi vimilikishi na kuwa si mara yao ya kwanza kukutana navyo. Kwa hivyo, aelekeze wanafunzi ili wabainishe mabadiliko yanayoweza kujitokeza ikiwa majina ya ngeli ya *I-ZI* yanatumiwa. Ulingenishaji unaofanywa katika sehemu A na sehemu B ya zoezi hili ulenge kuonyesha umilikisho wa kitu kwa mtu mmoja au umilikisho wa vitu kwa mtu mmoja au watu wengi ili wanafunzi waweze kuelewa. Mwalimu atumie mifano katika hali halisi ambapo anaweza kuwaomba wanafunzi kujitokeza mbele ya wenza na kuwaonyesha umilikishi uliopo kuitia vifaa kama kalamu na vitabu vinavyomilikiwa na mwanafunzi mmoja au wanafunzi wengi. Kuhusiana na zoezi la nne, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma sentensi walizozipewa huku akisisitizia matumizi ya vivumishi nya sifa.

Kwa hivyo, wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu na kujadiliana kuhusu sifa za vivumishi hivi ambapo vinaeleza zaidi kuhusu majina ya ngeli ya *I-ZI* ili kutambua muundo wake. Mwalimu atoe mifano inayoelewaka katika kuwaelekeza wanafunzi wake kupata tofauti kati ya mifano ya majina mengine. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika, kisha awashirikishe wanafunzi wote wakati wa kusahihisha zoezi hilo. Wanafunzi wapewe nafasi ya kuuliza maswali pale wasipoelewa na watoe maoni yao ili mwalimu apate kiwango cha uelewa wao kabla ya kuendelea na sehemu ya mazoezi ya jumla.

Aidha, baada ya mwalimu kutambua kwamba wanafunzi wameelewa mambo muhimu katika ujifunzaji wao wa matumizi ya ngeli ya *I-ZI* na vivumishi vinavyoambatana, ni vyema awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kujibu zoezi la kwanza na la tatu la sehemu ya mazoezi ya jumla. Kwa hivyo, mwalimu azunguke darasani kuchunguza ikiwa wanafunzi wanaelewa na kujibu maswali kama inavyostahili ili kuwaelekeza wale wanaotatizika. Halafu, mwalimu awaombe wanafunzi wote kusahihisha kwa pamoja mazoezi hayo. Kwa hivyo, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wote wameshirikishwa kusahihisha mazoezi yaliyopo kwa kuwachochea kupata ujuzi kuhusu tafakuri tunduizi ambapo anaweza kuwaomba wanafunzi wengine kuchunguza majibu yanayotolewa na wenzao, usuluhisho wa matatizo ambapo anawaomba wanafunzi kutoa suluhihisho la matatizo ya wenzao, ubunifu, ugunduzi na stadi za utafiti ambapo anawaomba wanafunzi kuchunguza mifano iliyopo na ile inayotolewa na wanafunzi wengine.

Hatua ya 6: Kusikiliza na kuzungumza

Mwalimu awaombe wanafunzi kufunga vitabu vyao na aendeleee kwa kuwasomea maneno yafuatayo ili wayaandike katika madaftari yao.

- nchi, mwananchi, jamhuri, rais, raia, mkoa, kata, wilaya, tarafa, hospitali, barabara, mfereji, kaskazini, serikali, magharibi, kusini, mashariki.

Wamalizapo kuandika maneno haya, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha zoezi hili huku akisisitizia pale ambapo wanafunzi hutatizika. Baadaye, awaombe wanafunzi kujitokeza mbele ya wenzao mmoja baada ya mwengine ili ajitambulishé kwa kutaja jina lake, mkoa au jimbo lake, wilaya yake, tarafa yake, kata yake na hata kijiji chake. Atumie mfano uliopo katika kitabu cha mwanafunzi ili waweze kuelewa kile wanachotakiwa kukifanya katika zoezi hili.

Hatua ya 7: Ufahamu

Katika hatua hii ya ufahamu, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma tena kwa makini na kwa kimya kifungu cha habari kuhusu *nchi* yangu huku wakijibu maswali yaliyotolewa kama maswali ya ufahamu. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika

kusahihisha maswali hayo huku akitilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

Hatua ya 8: Hitimisho

Katika hatua hii ya mwisho wa somo hili, mwalimu ahitimishe somo kwa kuuliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyofunza ili kutambua ikiwa wanaweza kutaja maeneo mbalimbali ya nchi ya Rwanda kama vile ; mikoa, wilaya, nchi zinazopakana na Rwanda, pembe za dunia kama vile kaskazini, kusini, mashariki na magharibi. Mambo mengine yanayohusiana na uongozi nayo yarejelewe na hata vyeo vya uongozi vilivyopatikana katika somo hili. Maswali mengine yahusu matumizi ya ngeli ya I-ZI ambapo mwalimu atawaomba wanafunzi kudhihirisha sifa muhimu walizojifunza kutambua ngeli hii na vivumishi vinavyoambatana nayo. Ili kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu zoezi la pili la mazoezi ya jumla katika sehemu ya sarufi na kuwaomba walifanye kama kazi mradi. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza somo la pili la mada hii ya msamati wa mazingira ya utawala.

Mazoezi ya ziada

Ili kuwasaidia wanafunzi wa kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaelekeze wanafunzi hao dhaifu kutazama darasa lao na kutunga sentensi zao kwa kutumia vifaa vilivyopo. Mwalimu awape mfano wa sentensi na kuwaelekeza kuhusu kile wanachotakiwa kufanya. Kama vile ;

Swali: Tunga sentensi zako kwa kutumia maneno yafuatayo:

1. *nchi*
2. *kata*
3. *tarafa*
4. *wilaya*
5. *kalamu*
6. *nyumba*
7. *serikali*
8. *nzuri*
9. *kubwa*
10. *zangu*

Mfano: Nchi yangu inaendelea vizuri.

e) **Tathmini**

Katika sehemu hii, mwalimu atathmini ikiwa malengo ya somo zima yameafikiwa kwa kiwango alichokitarajia. Hivyo basi, awaulize wanafunzi maswali mbalimbali yenye kuchunguza uwezo wa wanafunzi katika kutambua maeneo mbalimbali ya utawala wa nchi ya Rwanda kwa kurejelea pitcha na michoro iliyotumiwa kujifunzia somo hili. Vilevile, maswali mengine yaelekezwe kwa msamiati unaohusu utawala katika matumizi ya ngeli ya *I-ZI* pamoja na vivumishi vinavyoambatana nayo. Aidha, mwalimu awaulize maswali ya kuchunguza ujuzi wa wanafunzi kuhusu mawasiliano katika lugha rasmi kwa kurejelea msamiati uliopatikana katika kifungu cha habari kilichopo. Kwa mfano atumie ramani ya Rwanda na michoro mingine aliyoitumia katika somo hili, arejelee shughuli mbalimbali zinazofanywa kama nia ya kuendeleza nchi yao, nembo mbalimbali zinazoitambulisha nchi ya Rwanda, wimbo wa taifa, dira na kadhalika. Kutokana na sentensi zinazotolewa na wanafunzi, mwalimu achunguze ikiwa wanafunzi wamepata pitcha kuhusu mienendo mizuri inayotakikana na ambayo humtambulisha mwananchi mzuri mwenye kupenda na kujivunia nchi yake.

Zoezi la 1, ukurasa 116 -117

Wanafunzi wazingatie mifano ya sentensi zilizoandikwa katika kitabu cha mwanafunzi na watunge sentensi zao kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari ambayo ndiyo haya yafuatayo :

1. Bara
2. Rais
3. Wilaya
4. Mwananchi
5. Wabunge
6. Mchango
7. Mtaa
8. Barabara
9. Hospitali
10. Kimaendeleo
11. Jamhuri
12. Serikali
13. Sheria

Zoezi la 2, ukurasa 117 - 118

a,

b,

c

Zoezi la I, ukurasa 118

Baadhi ya shughuli za kimaendeleo zinazofanywa katika vijiji mbalimbali na ambazo zaweza kujadiliwa ndizo hizi zifuatazo:

- Umuganda
- Gira inka Munyarwanda
- Ubudehe
- Itorero

Zoezi la 2, ukurasa 118

1. Nchi yangu ni Rwanda.
2. Bara langu ni Afrika.
3. Rwanda inazungukwa na nchi mbalimbali : Kusini kuna Burundi, Kaskazini kuna Uganda, Mashariki kuna Tanzania, Magharibi kuna Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.
4. Mkoa wangu ni Mkoa wa Kusini/Mkoa wa Kaskazini/Mkoa wa Magharibi au Mji wa Kigali, Wilaya yangu ni Nyarugenge/Kicukiro/Gasabo/Nyagatare/Gatsibo/Rusizi/Rubavu/Gicumbi/Nyamasheke/Musanze/Bugesera/Kayonza/Kamonyi/Nyamagabe/Ngoma/Gakenke/Kirehe/Burera/Ngororero/Karongi/Huye/Nyanza/Rutsiro/Gisagara/Ruhango/Muhanga/Rwamagana/Nyabihu/Nyaruguru au Rulindo, Tarafa yangu ni (tarafa moja kati ya tarafa 416 zipatikanazo nchini), Kata yangu ni (Moja kati ya kata 20148 zipatikanazo nchini).
5. Wananchi wa Rwanda wanaitwa Wanyarwanda, Wananchi wa Burundi wanaitwa Warundi, Wananchi wa Uganda ni Waganda na wananchi wa Kenya ni Wakenya.
6. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.
7. Watu wanaowawakilisha Wanyarwanda na kuandaa sheria nzuri ni Wabunge.
8. Mojawapo kati ya shughuli zinazoendeleza nchi yangu ni shughuli za Umuganda.
9. Mkuu wa Mkoa wangu anaitwa (taja jina lake), Mkuu wa wilaya yangu ni (taja jina lake), Mkuu wa tarafa yangu anaitwa (taja jina lake), Mkuu wa Kata yangu ni (taja jina lake) na Mkuu wa kijiji changu anaitwa (taja jina lake).
10. Kwa kujichagulia viongozi wazuri wananchi wa Jamhuri ya Rwanda wanashiriki wote.

Zoezi la 3, ukurasa 120

1. Kaskazini Magharibi
2. Mashariki Kusini Mashariki
3. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

Zoezi la mjadala, ukurasa 121

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi kisha atathmini maelezo ya wanafunzi.

Zoezi la 1, ukurasa 122

1. Disemba, Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei, Juni, Julai, Agosti, Septemba, Oktoba, Novemba
2. Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei, Juni, Julai, Agosti, Septemba, Oktoba, Novemba, Disemba

Zoezi la 2, ukurasa 122-123

1. Msimu wa mvua nyingi.
2. Kipindi kirefu cha jua kali.
3. Kipindi kirefu cha mvua kiasi

Zoezi la 3, ukurasa 123

1. Juni
2. Mei
3. Julai
4. Januari

Zoezi la 1, ukurasa 124

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi

Zoezi la 2, ukurasa 124

Sifa za vifungu

- Kila kifungu kinaundwa kwa jina na kitenzi.
- Vitenzi vyote vimo katika hali yakinishi.

- Kila kitenzi kina kiambishi nafsi ‘i’ katika umoja na ‘zi’ katika wingi.

Zoezi la 3, ukurasa 124

1. Shule zile zimefunguliwa.
2. Ngazi zilizonunuliwa zimevunjika.
3. Saa zao zimeuzwa.
4. Kofia za kina baba zimepota.
5. Taa zile zitazimika.

Mazoezi ya marudio

Zoezi la 1, ukurasa 125

Mfano:

Swali : Nchi ya Burundi napakana na nchi ya Tanzania.

Jibu : Nchi ya Burundi inapakana na nchi ya Tanzania.

1. Jamhuri ya Rwanda inapakana na Jamhuri ya Burundi huko kusini.
2. Wilaya za Rubavu na Ngororero zinajitokeza katika jimbo la Magharibi.
3. Jamhuri za bara la Afrika zinashirikiana katika maendeleo ya wananchi wake.
4. Nchi za Afrika Mashariki zinatumia lugha ya Kiswahili.
5. Tarafa ya Nyarugenge imejengwa katikati mjini Kigali.
6. Nchi za Ubelgiji na Ufaransa zinajitokeza barani Ulaya.
7. Nchi ya Marekani na raia wengi.
8. Nchi ya Uchina na teknolojia nzuri.
9. Shule yangu walimu wenye bidii lakini shule ya Muneza na shule ya Musana zina walimu wavivu.
10. Karatasi zangu zimeanguka chini.

Zoezi la 2, ukurasa 125 - 126

Umoja

1. Nyumba yangu inajengwa.
2. Kalamu yako inaandika vizuri.
3. Sauti yako inapendeza sana.
4. Baiskeli yake imeharibika.
5. Suruali yake imechafuka sana.
6. Ndege yake imeanguka.
7. Mama anafua nguo yake.
8. Wewe unapaza sauti yako.
9. Kampuni yao imestawi tena.
10. Barabara yangu inajengwa kijijini.

Wingi

- Nyumba zetu zinajengwa.
 Kalamu zenu zinaandika vizuri.
 Sauti zenu zinapendeza sana.
 Baiskeli zao zimeharibika.
 Suruali zao zimechafuka sana.
 Ndege zao zimeanguka.
 Mama wanafua nguo zao.
 Nyinyi mnapaza sauti zenu.
 Kampuni zao zimestawi tena.
 Barabara zetu zinajengwa vijijini.

Zoezi la 3, ukurasa 126

1. Nguo yake imechanika.
2. Kaka yako anavuka mpaka wa Gatuna kuenda nchi ya Uganda.
3. Dada yangu na kaka yetu wanajifunza vizuri.
4. Mama yetu analima shamba na baba yetu anavuna.
5. Mtoto wangu anaenda kwenye ofisi ya wilaya yetu.
6. Tarafa yangu ina miradi ya kuendeleza wananchi.
7. Baiskeli yetu imetengenezwa.
8. Kalamu zangu zinaandika vizuri.
9. Nyumba yetu inajengwa mjini Kigali.
10. Nchi yao inatajirika siku baada ya siku.

Zoezi la kuigiza, ukurasa 126

Mwalimu atathmini usahihi wa sentensi za wanafunzi wakati wa maigizo.

- Kila mwanafunzi ajitambulise mbele ya wenzake kwa kutaja jina lake, mkoa wake, wilaya yake, tarafa yake, kata yake na kijiji chake.

Zoezi la imla, ukurasa 126

Mwalimu awasomee wanafunzi maneno yafuatayo:

- *nchi, mwananchi, jamhuri, rais, raia, mkoa, kata, wilaya, tarafa, hospitali, barabara, mfereji, kaskazini, serikali, magharibi, kusini, mashariki.*

Somo la Pili

Ofisi ya tarafa yangu

Muda: Vipindi 4

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha mazungumzo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi.
- Kutaja na kueleza vyeo vya viongozi mbalimbali.
- Kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati wa mazingira ya utawala.
- Kutaja na kupanga majina ya miezi ya mwaka.
- Kutumia majina ya ngeli za *U-I* pamoja na vivumishi vinavyoambatana (vivumishi vimilikishi).

b) Nyenzo/Vifaa vya kujifunzia

- Vinasasauti
- Michoro ya mazingira ya utawala: ofisi za viongozi, viongozi na raia wengine
- Vifaa vya shule kama vile vitabu, kalamu, kifutio, ubao, chaki, n.k.
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 127.
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

c) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu msamiati wa mazingira ya utawala kwa kuwekea mkazo majina

ya viongozi na wajibu wao katika kuwahudumia wananchi. Kwa hivyo, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wake wanahitaji kupata mifano ya shughuli kadhaa zinazofanywa na viongozi hao huku nafasi ya wananchi katika shughuli hizo ikibainishwa. Mwalimu aandae michoro na picha zinazolenga kuonyesha jinsi ambavyo viongozi na wanaoongozwa hushirikiana kupanga miradi mbalimbali inayochangia kuboresha maisha ya wananchi. Wanafunzi wapewe nafasi ili watoe mchango wao kuhusu uongozi wa maeneo yao na mwalimu awaelekeze kupata mifano mizuri inayoonyesha uongozi bora uliopo. Hivyo basi, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vyote vinavyopendekezwa kufunzia somo hili na azingatie wakati unaofaa wa kuonyesha vifaa hivyo hadharani ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Kwa kuwa somo hili litatoa maelezo pia kuhusu matumizi ya ngeli ya *U-I*, ni vyema mwalimu afikirie kwanza mifano dhahiri inayoweza kusaidia wanafunzi kuelewa tofauti iliyopo kati ya ngeli ya *I-ZI* ambayo ilijadiliwa katika somo lilitangulia. Katika somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi kulingana na maelekezo yaliyotolewa katika kila zoezi linalohusika.

d) Utaratibu wa somo

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake nao wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu wao. Baadaye, awachangamshe wanafunzi wake kwa kuuliza maswali mbalimbali kuhusu michoro iliyopo katika kitabu cha mwanafunzi na wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na kile wanachokiona katika picha katika michoro hiyo. Ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kupata ujuzi kuhusu tafakuri tunduizi, ubunifu na ugunduzi kupitia picha iliyopo. Kwa mfano, anaweza kuwaauliza maswali kuhusu viongozi wapatikanao katika tarafa, wajibu wao na huduma zinazopewa wananchi. Ili kuwasaidia wanafunzi kuwasiliana katika lugha rasmi na kuimarishe ujuzi kuhusu ushirikiano, utawala binafsi na stadi za kimaisha, mwalimu awaelekeze wanafunzi ili watunge sentensi zenye kuonyesha jinsi ambavyo viongozi wote katika tarafa hushirikiana kumhudumia mwananchi na kutatua shida zake kwa muda unaofaa kupitia michoro iliyopo. Hivyo basi, wanafunzi watazame picha na kujibu maswali waliyoulizwa huku wakijaribu kutambua nafasi ya uongozi bora.

Hatua ya 2: Kusoma na kufahamu

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha mazungumzo kinachohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Wanafunzi nao wasome kwa kimya na kuandika msamiati huo. Baadaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu hicho cha mazungumzo ili kuhakikisha kuwa wamesoma. Kwa mfano awaulize: *Uwera na Sugira wako wapi? Sugira anataka nini?*

Wanafunzi wayajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hicho. Kwa mfano: *Uwera na Sugira wako kwenye ofisi ya tarafa yao. Sugira anataka kitambulisho.* Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi kusoma kwa sauti kifungu cha mazungumzo kinachohusika na wanafunzi wasome kwa sauti mmoja baada ya mwingine. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanasoma kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi huku akisahihisha pale ambapo wanafunzi hufanya makosa.

Hatua ya 3: Ujifunzaji wa msamiati

Mwalimu atoe maelekezo kuhusu namna ya kutafuta maana za msamiati mpya ambao uliorodheshwa na wanafunzi wakati wao wa kusoma kifungu cha mazungumzo kilichopo. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu na kujadiliana kuhusu msamiati huo. Wanafunzi wazingatie matumizi ya msamiati huo katika kifungu kilichopo na wajadiliane kuhusu msamiati huo huku wakitumia kamusi pale panapohitajika. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi na kuwaelekeza pale wanapotatzika. Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika zoezi la kwanza la msamiati. Mwalimu awaombe wanafunzi kuchunguza mifano iliyopo katika makundi yao ya wanafunzi watatu na kutunga sentensi zao wenyewe kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari. Ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuwaambia kwamba wanaweza kuchunguza pia matumizi ya maneno hayo katika kifungu cha mazungumzo walichokisoma ili waweze kuelewa kwa urahisi. Wanafunzi wajibu swali hilo kama walivyoelekezwa na mwalimu azunguke darasani kuwasaidia pale wanapotatzika.

Kuhusiana na zoezi la pili, mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kukamilisha mapengo yaliyoachwa katika sentensi walizotolewa kwa kutumia maneno yaliyopo. Wanafunzi wafanye zoezi hilo kulingana na maelekezo ya mwalimu wao na kusahihisha kwa pamoja baada ya kulimaliza. Wakati wa kujibu mazoezi haya, mwalimu ajaribu kuwapa wanafunzi wake nafasi ya kutafakari kuhusu baadhi ya mambo yanayojitokeza katika utunzi wa sentensi zao. Vilevile, mwalimu achukue fursa hii kwa kusaidia wanafunzi wake kutafuta suluhisho la matatizo kwa kurejelea wajibu wa viongozi mbalimbali katika kuwashudumia wananchi. Utunzi wa sentensi za wanafunzi pia uhakikishe kuwa wanapata ujuzi kuhusu ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha hasa katika mazingira ya utawala.

Hatua ya 4: Matumizi ya lugha

Katika hatua hii, mwalimu alenge kuwasaidia wanafunzi kuwa na ujuzi unaowasaidia kuwasiliana katika lugha rasmi. Kwa hivyo, awaombe wanafunzi kusoma sentensi fupifupi zilizopo. Mwalimu awaambie wanafunzi waandike majina ya miezi yapatikanayo katika sentensi zilizopo na wayapange kuanzia mwezi wa kwanza hadi mwezi wa mwisho wa mwaka. Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi ili wafanye

zoezi la pili ambapo wanafunzi wanajadiliana kuhusu misimu na vipindi nya mvua na juu nchini. Kuhusiana na zoezi la tatu, mwalimu awaombe wanafunzi kuonyesha shughuli za kitaifa zinazofanywa katika miezi iliyotolewa yaani mwezi wa Aprili, Julai na Agosti. Ili kurahisisha zoezi hili kwa wanafunzi, mwalimu afafanue zoezi hili kwa kurejelea mfano : *Katika mwezi wa Mei, Wanyarwanda wanaadhimisha siku kuu ya Wafanyakazi.* Kupitia mazoezi yaliyotolewa katika sehemu hii, mwalimu achunguze ujuzi wa wanafunzi kuhusu stadi za utafiti, ubunifu na ugunduzi ambapo wanafunzi wanajadiliana na kutafiti kuhusu mambo mbalimbali yanayotakikana kudhihirishwa katika mazoezi hayo.

Hatua ya 5: Sarufi - Ngeli ya U-I na vivumishi vimilikishi

Katika hatua hii ya ujifunzaji wa sarufi, mwalimu awaombe kwanza wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili wasome sentensi zilizopo na kujadiliana kuhusu sifa za vifungu nya maneno vilivyoandikwa kwa hati mlazo. Wanafunzi wajigawe kama walivyoambwa na mwalimu na kusoma kwa pamoja katika makundi yao huku wakichunguza sifa za vifungu hivyo. Mwalimu awaombe wanafunzi kulinganisha miundo ya vifungu hivyo katika sentensi zote walizopewa kupitia mifano ya tungo iliyopo katika kitabu cha mwanafunzi huku akilenga kubainisha viambishi nafsi nya vitenzi katika hali za umoja na wingi kwa kurejelea viambishi nya majina kiima yaliyotumiwa. Mwalimu achukue fursa hii kwa kudhihirisha viambishi ngeli vilivyopo katika mifano hii ; yaani m katika jina kiima, u ambayo ni kiambishi nafsi cha umoja wa jina katika kitenzi na i ambayo ni kiambishi nafsi cha wingi wa jina katika kitenzi husika.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kuandika umoja au wingi wa sentensi zilizopo katika zoezi la kwanza la sehemu ya sarufi. Ili kuwekea mkazo yale ambayo mwanafunzi anapaswa kuchunguza katika ujifunzaji wake wa sarufi katika sehemu hii, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma sentensi zilizopo huku wakichunguza kanuni zinazowaelekeza katika matumizi ya majina ya ngeli za *U-I* na kuwaomba wafanye zoezi la tatu. Zoezi hili lisahihishwe kwa pamoja na mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wameelewa sifa za miundo ya majina ya ngeli hizi ili waweze kutunga sentensi zao wenyewe katika zoezi la nne. Mwalimu awaombe wachunguze sentensi zilizopo katika zoezi la nne, kwa minajili ya kuwawezesha wanafunzi kujitungia baadaye sentensi kamili zenye sifa zinazofanana. Yaani, sentensi zenye majina ya ngeli ya *U-I* na vivumishi vimilikishi.

Ni vyema mwalimu agusie mifano mingine yenye kutumia majina ya ngeli nyingine kama vile *I-ZI* na A-WA kwa kuwachochea wanafunzi kutakafari kuhusu mabadiliko ya miundo ya majina, vivumishi na vitenzi vinavyoandamana na majina hayo. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kufanya zoezi la saba katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kulisahihisha kwa pamoja. Ni vyema mwalimu arejelee mambo yanayoonekana kuwatatiza wanafunzi kupitia zoezi hili huku akiwaelekeza kugundua sifa za miundo ya ngeli ya *U-I* na vivumishi vinavyoambatana kupitia maelekezo yaliyomo katika kitabu cha mwanafunzi.

Hatua ya 3: Kusikiliza na kuzungumza

Hatua ya tatu inahusu kusikiliza na kuzungumza. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi kutamka kwa usahihi maneno yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi kwa utambuzi wa herufi na silabi zipatikanazo katika majina ya miezi yaliyotolewa mwanafunzi. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kuigiza mazungumzo kati ya Uwera, Sugira na Mpigapicha kwa kuhakikisha kwamba wanafunzi wanazungumza ipasavyo. Kwa hivyo, ni vyema asahihishe matamshi ya wanafunzi pale ambapo wanafanya makosa.

Katika sehemu hii ya kusikiliza na kuzungumza, mwalimu anatakiwa pia kuwaelekeza wanafunzi kuhusu namna ya kufanya zoezi lililopo katika kitabu cha mwanafunzi. Hivyo basi, awaombe wafunge vitabu vyao na aendelee kwa kuwasomea maneno na vifungu vifuatavyo ili waviandike katika madaftari yao.

Halmashauri, mawaziri, tunaishi nchini Rwanda, katikati mwa nchi yangu, mpaka, nchi ya kidemokrasia, mimi ni Mnyarwanda, viongozi wanashirikiana na wananchi, wananchi wanajichagulia viongozi, kufanya shughuli, kujenga hospitali, mitaa ya biashara, shughuli mbalimbali, Februari, Machi, Julai, Agosti, Septemba, Desemba.

Katika zoezi hili la imla, mwalimu azingatie kwamba maneno yaliyopo yana utata kwa wanafunzi pale ambapo baadhi yake yana silabi ambazo wanafunzi hawajazoea katika lugha yao ya mama kama vile mfuatano wa irabu mbili ambazo zinajitokeza katika silabi tofauti matumizi ya sauti / na r ambazo ni fonimu tofauti katika lugha ya Kiswahili, sauti m yenye kutamkwa kama silabi isiyo na irabu, gh na ch. Hali hii ichochee wanafunzi kutafiti kuhusu maneno mengine yenye kuwa na sifa hizo katika lugha ya Kiswahili kama njia ya ujifunzaji wa kudumu kwa wanafunzi pale wanapoweza kutumia maneno hayo katika mawasiliano yao na watu wengine bila tatizo lolote.

Hatua ya 4: Ufahamu

Katika hatua hii ya ufahamu, mwalimu awaombe tena wanafunzi kusoma kwa makini na kwa kimya kifungu cha mazungumzo kilichopo huku wakijibu maswali waliyotolewa katika sehemu ya ufahamu. Baadaye, mwalimu ashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha zoezi hilo.

Hatua ya 5: Hitimisho

Katika hatua hii ya mwisho wa somo hili, mwalimu ahitimishe somo kwa kuuliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu walijojifunza kama vile maswali ya kutaja vyeo vya viongozi mbalimbali na kueleza wajibu wa viongozi hao. Vilevile, maswali mengine yanaweza kuwaelekeza wanafunzi kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati wa mazingira ya utawala ambaao ulipatikana katika kifungu hiki cha mazungumzo, kutaja na kupanga majina ya miezi ya mwaka na kutumia kwa usahihi majina ya ngeli ya *U-l* pamoa na vivumishi vinavyoambatana nayo. Ili kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze

wanafunzi kuhusu kazi mradi. Hivyo basi, awaombe watunge sentensi zinazofanana na zile zilizomo katika zoezi la sehemu ya sarufi. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza somo la tatu la mada hii ya msamiati wa mazingira ya utawala.

e) Mazoezi ya ziada

Ili kuwasadia wanafunzi wa kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe wanafunzi hawa kufanya mazoezi yafuatayo :

- 1) *Panga siku za wiki kuanzia Jumatatu hadi siku ya mwisho.*
- 2) *Panga majina ya miezi kuanzia Januari hadi mwezi wa mwisho wa mwaka.*
- 3) *Tunga sentensi kwa kutumia :*
 - a) *mkoa*
 - b) *mito*
 - c) *mirefu*
 - d) *mkono*
 - e) *mdogo*

f) Tathmini

Katika sehemu hii ya tathmini, mwalimu alenge kutambua ikiwa ujifunzaji umefanywa kwa namna ya kuridhisha. Kwa hivyo, apime uwezo wa wanafunzi kwa kuwa uliza maswali tofauti yenye kudhamiria kuchunguza ikiwa wanaweza kutaja vyeo vya viongozi mbalimbali waliozungumziwa katika somo hili, wajibu wao katika kuwashudumia wananchi, majina ya miezi pamoja na kutumia msamiti wa mazingira ya utawala katika sentensi fupifupi na hata kubainisha sifa na matumizi ya ngeli ya U-I pamoja na vivumishi vinavyoambatana nayo. Vilevile, mwalimu achunguze ujuzi wa wanafunzi kuhusu kutafakari na kukuza stadi zao za utafiti juu ya mienendo mizuri inayotambulisha kiongozi mzuri na wananchi.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 129

1. *Uwera na Sugira wanakutania kwenye tarafa yao ya Nyarubaka.*
2. *Sugira anatafuta kitambulisho.*
3. *Uwera, yeye anataka kumwona afisa wa elimu.*
4. *Uwera anahitaji kubadilisha shule.*
5. *Uwera anataka kuendeleza masomo yake katika shule ya Nyamabuye.*
6. *Uwera alimtembelea nyanya yake na kumsaidia kazi za kilimo.*
7. *Wakulima hupanda mimea tofauti tofauti.*
8. *Msimu wa mvua hujitokeza mwezi wa Septemba hadi Disemba.*
9. *Wanyama hukosa nyasi kipindi cha jua kali.*
10. *Sugira atarudi kupata kitambulisho Jumatatu.*

Zoezi la I, ukurasa 130

Wanafunzi wazingatie mifano ya sentensi zilizoandikwa katika kitabu cha mwanafunzi na watunge sentensi zao kwa kutumia maneno yaliyopigwa mstari ambayo ndiyo haya yafuatayo:

1. Msimu
2. Afisa wa Kilimo
3. Mimea
4. Mwezi
5. Anahudumia
6. Kitambulisho
7. Picha
8. Mto

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi.

Zoezi la 2, ukurasa 130 - 131

1. Katika mwezi wa Aprili kuna mvua nyingi sana.
2. Nchini Rwanda, mwaka una vipindi viwili vya mvua na vipindi viwili vya juu.
3. Sasa ni zamu yangu ya kuonana na mkuu wa wilaya.
4. Kuanzia Juni hadi Agosti ni msimu wa juu kali.
5. Mkuu wa shule yangu anatuomba kuleta picha za kuweka juu ya vitambulisho vya shule.
6. Mimea mingi inapandwa wakati wa mvua.
7. Mto Akanyaru unapitia kwenye mpaka wa nchi za Rwanda na Tanzania.
8. Mkuu wa kata ya Rwigerero anapenda kuhudumia wananchi na kutatua shida zao.
9. Gasore anatoka kuomba kitambulisho kwenye ofisi ya mkuu wa tarafa yake.
10. Afisa wa Elimu anapenda kuchunguza usafi shulenii.

Zoezi la 1, ukurasa 132

<u>Umoja</u>	<u>Wingi</u>
<u>Mwaka unaanza.</u>	<u>Miaka inaanza.</u>
<u>Mwezi una siku nyingi.</u>	<u>Miezi ina siku nyingi.</u>
<u>Mmea unapandwa.</u>	<u>Mimea inapandwa.</u>
<u>Mto unafurika.</u>	<u>Mito inafurika.</u>
<u>Mguu unatembea.</u>	<u>Miguu inatembea.</u>
<u>m/mw → u</u>	<u>mi → i</u>

Zoezi la 2, ukurasa 132 - 133

1. **Mkeka unatandazwa chini**

Jibu: *Mikeka inatandazwa chini.*

2. **Mtego unanasa wanayama.**

Jibu: *Mitego inanasa wanyama.*

3. **Mgongo unasafishwa vizuri sana..**

Jibu: *Migongo inasafishwa vizuri.*

4. **Mwezi unaanza leo.**

Jibu: *Miezi inaanza leo.*

5. **Mwaka unatosha kukamilisha miradi yote.**

Jibu: *Miaka inatosha kukamilisha miradi yote*

Zoezi la 3, ukurasa 133 - 134

Umoja	Wingi
1. Mchango umetolewa.	Michango imetolewa.
2. Mguu unanenepa.	Miguu inanenepa.

- | | |
|-------------------------|----------------------|
| 3. Mpapai unachumwa. | Mipapai inachumwa. |
| 4. Mtama unalimwa. | Mitama inalimwa. |
| 5. Mgomba umepandwa. | Migomba imepandwa. |
| 6. Mnasaki umeuzwa. | Minasaki imeuzwa. |
| 7. Mgongo unapendeza. | Migongo inapendeza. |
| 8. Mlango umefungwa. | Milango imefungwa |
| 9. Msitu unatisha. | Misitu inatisha. |
| 10. Mto umefurika. | Mito imefurika. |
| 11. Msumari umenichoma. | Misumari imenichoma. |
| 12. Mwili umesafishwa. | Miili imesafishwa. |
| 13. Mti umeanguka. | Miti imeanguka. |
| 14. Mchungwa umekatwa. | Michungwa imekatwa. |
| 15. Mkekka umeharibika. | Mikekka imeharibika. |

Zoezi la 4, ukurasa 134

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sentensi zizingatie upatanisho sahihi wa kisarufi katika ngeli ya U-I.

Zoezi la ziada, ukurasa 134 - 135

1. Muhire na Mukamunana wanatandika mkekka yao katika chumba cha wageni.
2. Msumari wako unapigiliwa ndani ya mti wake.
3. Ni lazima watoto wasafishe miguu yao.
4. Mji wa Kigali umeimarisha usafi. Wageni wote wanassema kuwa ni mji mzuri sana.
5. Mkoo wa Kaskazini unatunza wanyama vizuri.
6. Mikono yao inafanya kazi vizuri.
7. Mguu wako unatibiwa sasa hivi.
8. Milima yangu ina miti mirefu
9. Miti yako inapatikana sana wakati wa kiangazi.
10. Miji yenu inajengwa nchini Rwanda.

Utawala Bora

Muda: Vipindi 2

a) **Malengo ya somo**

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha mazungumzo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi.
- Kutaja na kueleza miradi mbalimbali ya kimaendeleo.
- Kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati wa mazingira ya utawala.
- Kutumia majina ya ngeli ya U - I pamoja na vivumishi vinavyoambatana.

b) **Vifaa vya kujifunzia**

- Vinasasauti
- Michoro ya mazingira ya utawala: shughuli za kimaendeleo, viongozi na raia wakiwa pamoja
- Vifaa vya shule kama vile vitabu, kalamu, kifutio, ubao, chaki, n.k.,
- Kitabu cha mwanafunzi, ukurasa 136

c) **Maandalizi ya somo**

Somo linazungumzia uongozi bora na linatolewa katika vipindi viwili. Kwa hivyo, mwalimu arahishe ujifunzaji wake kwa kuleta vifaa vyote vyenye kudhihirisha nafasi ya wananchi katika kupanga miradi mbalimbali inayofanywa kama vile, shughuli za *Gira inka, Ubudehe, Umuganda*, na kadhalika. Kwa hivyo, mwalimu aandae picha tofauti zenye kuonyesha raia na viongozi wao katika mikutano yao ya kupanga pamoja shughuli hizo zinazofanywa kama njia ya kuboresha maisha ya wananchi. Ni vyema pia mwalimu azingatie wakati unaofaa kuonyesha vifaa hivyo hadharani ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Mwalimu atumie maelezo kamili yanayochora shughuli inayohusika ili kuwawezesha wanafunzi kuelewa vizuri hasa wanafunzi wasioweza kuona picha na michoro iliyopo. Katika somo hili, mwalimu

ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

d) Utaratibu wa somo

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu aamkie wanafunzi na wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu wao. Mwalimu aulize maswali mbalimbali kuhusu michoro iliyopo katika kitabu cha mwanafunzi na wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na kile kinachoendelea katika michoro hiyo. Ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kupata ujuzi kuhusu tafakuri tunduizi, ubunifu na ugunduzi kuitia picha iliyopo. Hivyo basi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua miradi mbalimbali ya kimaendeleo iliyopo nchini na jinsi ambavyo wananchi hushirikishwa katika miradi hiyo kuitia picha waliyoonyeshwa na kujibu maswali waliyoulizwa.

Hatua ya 2: Kusoma na kufahamu

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha mazungumzo kinachohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Wanafunzi nao wasome kwa kimya na kuandika msamiati huo. Baadaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu hicho ili kuhakikisha kuwa wamesoma. Kwa mfano, *Keza anaenda wapi? Ni kazi gani iliyotangazwa?* Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hicho cha mazungumzo. Kwa mfano: *Keza anaenda kwenye ofisi ya tarafa yake. Kazi iliyotangazwa ni ya kusajili watu wasiojiweza.* Hatimaye, mwalimu awaambie wanafunzi wasome kwa sauti kifungu cha mazungumzo kinachohusika nao wanafunzi wasome kwa sauti mmoja baada ya mwingine. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanasoma kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi huku akisahihisha pale ambapo wanafunzi watafanya makosa.

Hatua ya 3: Ujifunzaji wa msamiati

Katika hatua hii ya ujifunzaji wa msamiati, mwalimu atoe maelekezo kuhusu namna ya kutafuta maana za msamiati mpya ambao uliorodheshwa na wanafunzi wakati wa kusoma kifungu cha mazungumzo kilichopo. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujadiliana kuhusu msamiati huo. Wanafunzi wazingatie matumizi ya msamiati huo katika kifungu kilichopo na wajadiliane kuhusu msamiati huo huku wakitumia kamusi pale panapohitajika. Mwalimu naye azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi na kuwaelekeza pale wanapotatizika. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kuchunguza mifano ya sentensi iliyopo katika zoezi la kwanza la msamiati na kutunga sentensi zao wenyewe kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari. Ni vyema mwalimu kuwaelekeza wanafunzi kwa kuwaambia

kwamba wanaweza kuchunguza pia matumizi ya maneno hayo katika kifungu cha mazungumzo walichokisoma ili wapate ufhamu unaohitajika wakati wa kutunga sentensi zao. Wanafunzi wajibu swali hilo kama walivyoelekezwa na mwalimu naye azunguke darasani kuelekeza wanafunzi pale wanapotatizika.

Kuhusiana na zoezi la pili, mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kukamilisha mapengo yaliyoachwa katika sentensi walizotolewa kwa kutumia maneno yaliyopo ndani ya mabano. Wanafunzi wafanye zoezi hilo kulingana na maelekezo ya mwalimu wao na kusahihisha kwa pamoja baada ya kulimaliza. Wakati wa kujibu mazoezi haya ya msamati, mwalimu ajaribu kuwapa wanafunzi nafasi ya kutafakari kuhusu baadhi ya mambo yanayojitokeza katika utunzi wa sentensi kama vile shughuli za kimaendeleo zinazojitokeza, juhudzi za viongozi katika kuinua kiwango cha maisha ya wasiojiweza, na kadhalika. Vilevile, mwalimu achukue fursa hii ili kuwasaidia wanafunzi wake kutafuta suluhisho la matatizo kwa kurejelea wajibu wa viongozi mbalimbali katika kuwashudumia wananchi na kuwashirikisha katika mambo yote yanayofanywa kwa ajili yao. Hivyo basi, utunzi wa sentensi na uchunguzi wa sentensi zilizopo uhakikishe kwamba wanafunzi wanapata ujuzi kuhusu stadi za utafiti, usuluhisho wa matatizo, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha hasa katika mazingira ya utawala.

Hatua ya 4: Matumizi ya lugha

Katika hatua hii, mwalimu alenge kuwasaidia wanafunzi kuwa na ujuzi unaowasaidia kuwasiliana katika lugha rasmi. Kwa hivyo, awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujadiliana kuhusu miradi mbalimbali inayofanywa katika vijiji vyao. Miradi hiyo ihusu kuinua kiwango cha maisha ya wananchi, kudumisha amani na kuendeleza nchi kwa jumla. Wanafunzi, kwa upande wao, wajigawe kama walivyoambiwa na kujadiliana kuhusu miradi hiyo. Mwalimu awaelekeze kwa kuwapa mifano ya miradi hiyo na kuwaelezea kuhusu jinsi ambavyo wanaweza kutunga sentensi zao. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwapa kitangulizi kama: *Miradi inayofanywa katika vijiji yetu ni... na kuwaomba wanafunzi wakamilishe kwa kutumia miradi inayofanywa kama Gira inka, umuganda, na kadhalika.* Mwalimu azunguke darasani ili kuelekeza na kusaidia pale anapoulizwa na wanafunzi. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kujitokeza mbele ya wenzao ili kuwaelezea kuhusu miradi hiyo na wanafunzi wengine watoe maoni yao kwa kubainisha umuhimu wa miradi hiyo kama njia ya kuwapa uwezo wa kutafakari kuhusu miradi hiyo.

Hatua ya 5: Sarufi - Ngeli ya U-I na vivumishi vinavyoambatana navyo

Hatua hii inahusu ujifunzaji wa sarufi. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujadiliana kuhusu miundo ya sentensi zilizopo huku mkazo ukiwekwa kwenye viambishi vilivyopigiwa mistari. Wanafunzi wajigawe katika makundi kama walivyoambiwa na mwalimu na kusoma kwa pamoja sentensi hizo huku wakichunguza sifa za viambishi vilivyopigiwa

mistari. Mwalimu awaombe pia wanafunzi kulinganisha miundo ya viambishi hivyo kwa kubainisha miundo ya vivumishi vya sifa vinapoambatana na majina ya ngeli ya *U-I* katika umoja na wingi. Awaelekeze kutambua kwamba kiambishi *m* huwekwa mwanzoni mwa kivumishi katika umoja ambapo kiambishi *mi* huwekwa katika wingi. Viambishi nafsi *u-i* navyo vielezwe kama njia ya kubainisha umoja na wingi wa majina hayo.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kuchunguza sentensi katika zoezi la kwanza la sehemu ya sarufi ili waweze kutunga sentensi zao wenyewe zinazofanana nazo. Ili kuwekea mkazo yale ambayo wanafunzi wanapaswa kuchunguza katika ujifunzaji wake wa sarufi katika sehemu hii, mwalimu awaombe kusoma kwa makini sentensi zilizopo huku wakichunguza sifa na miundo iliyopigiwa mstari yaani; matumizi ya majina ya ngeli ya *U-I* pamoja na vivumishi vya sifa vinavyoandamana nayo. Zoezi hili lisahihishwe kwa pamoja na mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wameshaelewa sifa za miundo hiyo ili waweze kukamilisha sentensi walizopewa katika zoezi la pili na kugeuza sentensi kwa kuziandika katika umoja au wingi katika zoezi la tatu.

Aidha, mwalimu awaombe wanafunzi kuchunguza vifungu vya majina na vivumishi vya sifa ambapo wanafunzi wanaweza kujumuisha matumizi ya viambishi vya majina kwa vivumishi vyote. Mwalimu asisitize kwamba baadhi ya vivumishi vya sifa havikubali kuchukua viambishi vya majina vinavyoolezea. Zoezi la nne la sehemu hii ya sarufi linalenga kuchunguza ikiwa wanafunzi wameshatambua matumizi mwafaka ya viambishi vilivyojitokeza katika ujifunzaji wa ngeli ya *U-I* wakati vinapoambatana na vivumishi vya sifa. Hivyo basi, awaelekeze ipasavyo kwa kutoa maelezo kamili ili wafanye zoezi hilo na kulisahihisha kwa pamoja mara moja baada ya kulikamilisha.

Hatua ya 6: Kusikiliza na kuzungumza

Mwalimu awaombe wanafunzi kufunga vitabu vyao na aendelee kwa kuwasomea maneno na vifungu vya maneno vifuatavyo ili waviandike katika madaftari yao.

Rais wa Jamhuri ya Rwanda, kazi ya muda mfupi, shughuli za kusajili watu wasiojiweza, mkutano wa kuandaa orodha ya watu, miradi inayosaidia wananchi, bima ya afya, nao ni mradi mzuri pia, msaada, barabara, hospitali, umaskini.

Katika zoezi hili la imla, mwalimu azingatie kwamba maneno yaliyopo yana utata kwa wanafunzi pale ambapo baadhi yake yana silabi ambazo wanafunzi hawajazoea katika lugha yao ya mama kama vile mfuatano wa irabu mbili ambazo zinajitokeza katika silabi tofauti na matumizi ya sauti *l, r, gh, dh, ch* na *silabi m* na *mu*. Hali hii ichochee wanafunzi kutafiti kuhusu maneno mengine yenye kuwa na sifa hizo katika lugha ya Kiswahili kama njia ya ujifunzaji wa muda mrefu kwa wanafunzi pale wanapoweza kutumia maneno hayo katika mawasiliano yao na watu wengine bila tatizo lolote. Baada ya kusahihisha zoezi hilo, mwalimu awaombe wanafunzi kuigiza mazungumzo kati ya Keza na Simbi kwa kuhakikisha kwamba wanafunzi wanazungumza ipasavyo. Mwalimu asahihishe papo hapo matamshi ya wanafunzi ikiwa wanafanya makosa.

Hatua ya 7: Ufahamu

Katika hatua hii ya ufahamu, mwalimu awaombe tena wanafunzi kusoma kwa makini na kwa kimya kifungu cha mazungumzo kilichopo huku wakijibu maswali yaliyotolewa katika sehemu ya ufahamu. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo.

Hatua ya 8: Hitimisho

Katika hatua hii ya mwisho wa somo, mwalimu ahitimishe kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Kwa mfano, awaulize maswali kuhusu miradi mbalimbali inayochangia kuinua kiwango cha maisha ya wananchi na ile ya kimaendeleo. Maswali mengine yahusu nafasi ya wananchi katika kuandaa shughuli hizo katika juhudhi za kuimarisha uongozi bora. Vilevile, maswali ya mwalimu yaegemee juu ya utunzi wa sentensi fupifupi katika matumzi ya majina ya ngeli ya *U-I* pamoja na vivumishi vya sifa kwa kulenga kuwapa wanafunzi picha kamili ya majina ya ngeli hii na vivumishi vinavyoambatana nayo. Ili kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu kazi mradi. Hivyo basi, mwalimu awaombe wafanye zoezi katika sehemu ya sarufi na zoezi hili lisahihishwe kabla ya kuanza somo litakalofuata.

e) **Mazoezi ya ziada**

Kwa ajili ya wanafunzi dhaifu wenye kiwango cha chini katika ujifunzaji, mwalimu awaombe wanafunzi hawa kufanya zoezi lifuatalo:

Swali: Andika umoja au wingi wa sentensi zinazofuata.

Umoja	Wingi
1. Mgomba mrefu unapendeza.	_____.
2. _____.	Miti mirefu imechomwa.
3. Mwembe umepandwa shambani.	_____.
4. Msumari mbaya unanichoma.	_____.
5. _____.	Mito mibovu inafurika.
6. Mchungwa mfupi.	_____.
7. _____.	Mikono mizuri inapendeza.
8. Mnanasi mkubwa umekauka.	_____.
9. _____.	Mikeka safi inatengezwa.

f) Tathmini

Katika sehemu hii ya tathmini, mwalimu alenge kutambua ikiwa ujifunzaji umefanywa kwa namna ya kuridhisha. Kwa hivyo, apime uwezo wa wanafunzi kwa kuwauliza maswali tofauti yenyе kudhamiria kudhihirisha shughuli na miradi mbalimbali inayofanywa kuendeleza nchi, wajibu wa viongozi na nafasi ya wananchi katika miradi hiyo. Vilevile, maswali mengine yachunguze uwezo wa wanafunzi katika matumizi ya msamiati wa utawala waliojifunza katika somo hili hasa kwa kuwaomba kutunga sentensi fupi fupi. Isitoshe, ni lazima mwalimu aulize maswali mengine ya kuchunguza uwezo wa wanafunzi wa kutumia majina ya ngeli ya U-l pamoja na vivumishi vyta sifa vinavyoandamana nayo. Katika sehemu hii, ni vyema pia mwalimu aulize maswali kwa ajili ya kutathmini kiwango cha kutafakari kuhusu mienendo mizuri inayomtambulisha kiongozi mzuri na mwananchi mzalendo wa nchi yake. Uwajibikaji kazini, amani na ushirikiano kati ya viongozi na wananchi uchukuliwe kama njia nzuri ya kuendeleza nchi.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 137-138

1. Keza ana haraka kwa sababu anataka kufika kwenye ofisi ya tarafa yake.
2. Keza amesoma tangazo la kazi ya muda mfupi.
3. Viongozi wamepanga shughuli za kusajili wasiojiweza.
4. Wasiojiweza ni watu maskini.
5. Mradi wa Gira Inka Munyarwanda unasaidia sana wananchi.
6. Mkutano wa viongozi na wananchi umefanywa.
7. Katika kijiji changu wananchi wote wamejitokeza kuandaa orodha ya watu maskini.
8. Watu wanaopatwa na magonjwa wanaweza kujitibisha kwa urahisi.
9. Ushirika katika bima ya afya ni muhimu sana.
10. Watu wanajiepusha na magonjwa kwa kuwa na miili safi.

Zoezi la I, ukurasa 138 - 139

Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo:

11. Kuomba
12. Wanajali
13. Misaada
14. Afya
15. Inasaidia
16. Kupambana
17. Ametajirika

Mwalimu atathmini usahihi wa sentensi za wanafunzi wote.

Zoezi la 2, ukurasa 139

1. Baba yangu anafanya shughuli za biashara mjini Kigali.
2. Si vizuri kuendeleza tabia za kuomba misaada kutoka nchi zilizoendelea.
3. Leo tunafanya mkutano na mkurugenzi wa shule yetu.
4. Watu wasiojiweza wanasaidiwa na serikali ya Rwanda ili watoke katika hali yao ya umaskini.
5. Nchi yangu ina miradi wa kufundisha raia wote umuhimu wa kilimo bora.
6. Nchi yangu ina miradi mbalimbali; kujenga barabara, kujenga vituo vya afya na hospitali.
7. Wanakijiji wanafanya mkutano na mkuu wa kijiji ili kupanga miradi ya maendeleo ya kijiji chao.
8. Mimi nimetoa ombi langu kwa Mkuu wa shule ili anipe ruhusa.
9. Mukamwiza ni tajiri sana. Yeye ana fuga ng'ombe wa kisasa.
10. Mkuu wa tarafa yangu anafanya kazi nzuri kwa kuendeleza tarafa yake.

Zoezi la 1, ukurasa 141

1. Mti huu ni mrefu lakini miti ile ni mifupi.
2. Miguu yake ni mizuri.
3. Mlima wa Kigali ni mrefu sana lakini milima mingine ni mifupi.
4. Mimea hii ni mizuri.
5. Miradi mikubwa imepangwa na serikali ya nchi yangu.
6. Mlango mdogo umefunguliwa.
7. Misaada mizuri inatolewa kwa nchi zinazoendelea.
8. Mchango wa viongozi ni mkubwa katika maendeleo ya nchi.
9. Mgomba mrefu umepandwa.
10. Migomba mirefu imepandwa.

Zoezi la 2, ukurasa 142

Umoja

1. Mchungwa mrefu umekatwa.
2. Mgomba mbovu umeungua.
3. Mlango mbovu umefungwa.

Wingi

1. Michungwa mirefu imekatwa.
2. Migomba mibovu imeungua.
3. Milango mibovu imefungwa.

- | | |
|------------------------------------|----------------------------------|
| 4. Mkate mtamu umetupwa. | Mikate mitamu imetupwa. |
| 5. Mguu mdogo unauma. | Miguu midogo inauma. |
| 6. Mgongo mzuri unasafishwa. | Migongo mizuri inasafishwa. |
| 7. Mti mdogo umechomwa. | Miti midogo imechomwa. |
| 8. Mto mchafu umefurika. | Mito michafu imefurika. |
| 9. Mlima mrefu unaonekana. | Milima mirefu inaonekana. |
| 10. Mnasaki mkubwa umezaa matunda. | Minasaki mikubwa imezaa matunda. |

Zoezi la 3, ukurasa 142 - 143

1. Mwaka una miezi mingi.
2. Miguu yake inauma.
3. Mlima huu una miti mirefu
4. Misumari mirefu imeletwa.
5. Penseli zako zimepotea.
6. Shule yenu ina wanafunzi na walimu wazuri.
7. Miradi mikubwa imepangwa na serikali ya nchi yangu.
8. Nchi yangu inasaidia wananchi .
9. Misaada mizuri inatolewa kwa wananchi.
10. Mchango wa viongozi ni mkubwa katika maendeleo ya nchi.

Zoezi la 4, ukurasa 143

1. Mtoto mbaya anakimbia.
2. Walimu wazuri wanafundisha.
3. Migomba mibovu imepandwa.
4. Mtu safi anatembea.
5. Watoto safi wanajifunza Kiswahili.
6. Nyumba ndefu zinasafishwa.
7. Mwanafunzi anaandika kwa kutumia kalamu nzuri.
8. Kalisa na Mutoni wanapanda milima mirefu.
9. Mwalimu huyu ni tajiri.
10. Kamana amesaidia mtu maskini.

Zoezi la Imla, ukurasa 143

Mwalimu awasomee wanafunzi vifungu vifuatavyo.

- Rais wa Jamhuri ya Rwanda, kazi ya muda mfupi, Shughuli za kusajili watu wasiojiweza, mukutano wa kuandaa orodha ya watu, miradi inayosaidia wananchi, bima ya afya, nao ni mradi mzuri pia, msaada, barabara, hospitali, umaskini.

MADA KUU: MSAMIATI WA MAZINGIRA MBALIMBALI

Mada Ndogo: Msamiati wa mazingira ya sokoni

Idadi ya vipindi: 11

Ujuzi upatikanao katika mada hii:

- Kusikiliza kwa makini, kusoma kifungu cha habari kinachohusu, kuzungumza kwa kuuliza bei kuhusu bidhaa tofauti.
- Kuhesabu idadi ya watu au vitu kwa kuzingatia matumizi sahihi ya vivumishi vya idadi, kimazungumzo na kimaandishi.

Malengo ya kujifunza:

Uhusiano wake na masomo mengine:

- *Hesabu-* katika mada ya faida na hasara.
- *Ujasiriamali-* kuhusu taasisi ya fedha na masoko.

Vifaa vya kujifunzia:

- Bidhaa tofauti zipatikanazo sokoni
- Pesa
- Picha au michoro ya watu na bidhaa sokoni
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 147
- Vinasasauti

Kigezo cha tathmini na upimaji:

- Uwezo wa kuuza na kununua bidhaa tofauti, kuhesabu vitu darasani au vitu vingine vipatikanavyo katika mazingira yake.

Maelezo kwa mwalimu:

a) **Utangulizi wa mada**

Mada hii inajishughulisha na msamiati upatikanao katika mazingira ya sokoni. Hivyo basi, majina ya bidhaa, biashara za aina mbalimbali zinazoweza kufanywa,

aina za pesa, wanunuzi na wauzaji, hesabu na vivumishi nya idadi huzungumziwa katika mada hii. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha inayotumiwa sana katika shughuli za kibiashara hasa katika eneo la Jumuia ya Afrika Mashariki, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua nafasi ya lugha hii ambapo Kiswahili huchukuliwa kama lugha ya kimataifa inayowaunganisha raia wote katika jumuia hii. Mwalimu atafute mbinu za kuwachochea wanafunzi wake kutambua umuhimu wa ujifunzaji wa lugha hii nchini Rwanda kwa kuonyesha kuwa nchi hii ina faida kubwa katika kuijunga na nchi nyingine za Jumuia ya Afrika Mashariki. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutumia msamiati unaojitokeza katika mazingira ya kununua na kuuza kama njia ya kutosheleza mengi ya mahitaji na kudumisha mawasiliano yao katika lugha rasmi. Kupitia somo hili, mwalimu amsaidie mwanafunzi kukuza uwezo wake wa kujadiliana kuhusu mambo kadhaa yapatikanayo katika shughuli za ununuzi na uuzaji kwa jumla na hasa katika mazingira ya sokoni kama vile kuhesabu, kuuliza bei ya vitu na kujibu maswali kadhaa yanayohusu bidhaa, pesa zinazotumiwa, bidhaa zipatikanazo na pia kupima bidhaa kwa vipimo tofauti tofauti.

Dhana muhimu zinazojitokeza katika mada hii ni pamoja na soko, *bidhaa, mteja, hesabu, kununua, kuuza, biashara, mfanyakibashara, pesa, duka, sarufi, kivumishi, idadi, sentensi*.

Masuala mtambuka

- Amani na maadili
- Elimu ya pamoja
- Elimu kuhusu fedha
- Mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo
- Utamaduni wa kiusanifishaji
- Masomo ya ujinsia na uzazi

b) Ujuzi wa jumla

- Usuluhishaji wa matatizo
- Mawasiliano katika lugha rasmi
- Stadi za utafiti
- Ubunifu na ugunduzi
- Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha
- Ujifunzaji wa muda mrefu

Somo la Kwanza

Mnunuzi na muuzaji

Muda: Vipindi 4

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi
- Kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati wa mazingira ya shule
- Kuhesabu kuanzia moja hadi elfu moja.

b) Vifaa vya kujifunzia

- Michoro ya soko, wanunuzi na wauzaji pamoja na bidhaa zao
- Vifaa mbalimbali kama vile kitabu cha mwanafunzi, ubao, kifutio, rula, raba, chaki na kadhalika
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum

c) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu msamiati wa mazingira ya sokoni na lina vipindi vinne. Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili. Mazingira ya soko yachorwe kwa kubainisha shughuli mbalimbali zipatikanazo hasa shughuli za kuuza na kununua. Hivyo basi, mbali na vitu halisi vinavyoweza kuuzwa na kununuliwa, aina mbalimbali za pesa zitumiwazo katika nchi tofauti, picha za watu wanaonunua na wanaouza, maduka yapatikanayo sokoni na bidhaa mbalimbali zidhahirishwe wazi katika mazingira ya sokoni. Ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa shughuli zinazofanywa katika mazingira ya sokoni, mwalimu awaombe wanafunzi kurejelea mifano ya masoko ya aina mbalimbali ambayo wanafunzi wanayafahamu na awaombe kutoa mifano ya bidhaa zinazouzwa katika masoko hayo. Mifano mingine ioneshe kwamba kuna masoko maalum yanayouza vitu mahususi na yale yanayouza vitu mbalimbali. Aidha, mwalimu azingatie wakati unaofaa wa kuonyesha hadharani vifaa alivyovileta ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Ikiwa kuna

wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu atumie vifaa hivyo kwa kuwaomba wao wenye kuvigusa huku wakitaja majina ya vifaa hivyo. Katika somo hili, mwalimu atahakikisha kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi yanayotakiwa kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli inayohusika darasani.

d) **Utaratibu wa somo**

Hatua ya I: Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake nao wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Baadaye, mwalimu awachangamshe wanafunzi wake kwa kuwaauliza maswali kuhusu mchoro ulioko katika kitabu cha mwanafunzi huku akilenga kuelekeza wanafunzi kubainisha tofauti kati ya kununua na kuuza, mnunuzi na muuzaji na baadhi ya bidhaa zipatikanazo sokoni. Kwa mfano anaweza kuwaauliza; *Mnaona nini kwenye picha hizi? Watu hawa wako wapi? Watu hawa wanafanya nini?* Wanafunzi nao wajibu maswali ya mwalimu wao kutokana na yale wanayoyaona katika mchoro uliopo. Kwa mfano wanawenza kujibu mwalimu kwa kusema: *Tunaona watu. Watu hawa wako sokoni. Watu hawa wanaauza vitu.* Kupitia mchoro huu, mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kupata ufahamu kwamba walemavu, wanawake na wanaume wote huweza kufanya biashara zinazopatikana katika mazingira ya sokoni ili kuboresha maisha yao.

Hatua ya 2: Kusoma na ufahamu

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha mazungumzo kilichopo kwa kuandika msamiati mpya wanaokutana nao. Wanafunzi wasome kwa kimya pamoja na kuandika msamiati huo mpya kwenye madaftari yao. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wamesoma kwa kimya kama iliviyotakiwa, mwalimu awaaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu cha mazungumzo mara moja wanapomaliza kusoma. Kwa mfano, anaweza kuwaauliza maswali yafuatayo: *Ni watu gani wanaozungumza katika kifungu hiki cha mazungumzo? Je, Muuzaji ameleta machungwa?* Wanafunzi kwa upande wao wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliiyoyasoma katika kifungu hicho cha mazungumzo. Kwa mfano; *Ni muuzaji na mnunuzi wanaozungumza. Hapana. Muuzaji hajaleta machungwa.* Baada ya kupata picha ya uelewa wa jumla wa wanafunzi kuhusu kifungu kinachohusika, mwalimu awaambie wanafunzi wasome kwa sauti kifungu hicho. Katika hatua hii, ni lazima mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

Hatua ya 3: Ujifunzaji wa msamiati

Mwalimu apange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba watafute maana za msamiati mpya kufuatana na jinsi ulivytumiwa katika kifungu cha mazungumzo walichokisoma. Halafu, mwalimu atoe maelekezo kuhusu zoezi la kwanza la msamiati na kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa zoezi hilo. Mwalimu awaombe wanafunzi wajadiliane kuhusu maana ya sentensi zilizopo ili

waweze kutumia msamiati uliopigiwa mstari katika sentensi zao wenyewe. Mwalimu azunguke darasani kuchunguza jinsi ambavyo wanafunzi wanafanya zoezi hilo ili aweze kuelekeza wale wanaotatizika. Baada ya kujibu maswali yaliyotolewa katika zoezi hili, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote wakati wa kuyasahihisha.

Kuhusu zoezi la pili la msamiati, mwalimu awaombe wanafunzi kujipanga katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kufanya zoezi lililopo kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kwa kuwaambia warejelee matumizi ya msamiati husika katika kifungu cha mazungumzo walichokisoma ili waweze kuelewa ipasavyo maana zake. Wanafunzi wajipange kama walivyoambiwa na mwalimu wao na kujibu maswali katika zoezi la pili la msamiati. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kuyasahihisha maswali ya mazoezi hayo kwa kurejelea mifano mingine inayoweza kuwasaidia kuelewa msamiati uliopo huku akigusia mienendo na ushirikiano uliopo kati ya muuzaji na mnunuzi au mfanyabiashara na mteja wake, aina za bidhaa zinazopatikana na kutoa mifano dhahiri yenye kuonyesha vitendo vya kupanda kwa bei za vitu, kupunguza, kununua, aina za pesa zinazoweza kutumiwa kununua vitu hasa katika maeneo tofauti ya Jumuia ya Afrika Mashariki, kuweka vizuri bidhaa ili zisiharibike, na kadhalika.

Hatua ya 4: Matumizi ya lugha

Katika sehemu hii, mwalimu atangulie kwanza kwa kuuliza wanafunzi wake kuhusu idadi za vitu vilivyopo katika mazingira ya shule. Kwa mifano, anaweza kuchukua vitabu vinne akawauliza swali kama ; *Mimi nina vitabu vingapi ?* Wanafunzi nao wajibu maswali ya mwalimu kwa kusema kwa mifano ; *Wewe una vitabu vinne.* Mwalimu aendelee kwa kuwaauliza wahesabu vitabu kwa kuweka juu kitabu kimoja kimoja huku akitaja jina la tarakimu anayoifikia ; *moja mbili, tatu, nne.* Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wake kusoma tarakimu zilizopo katika kitabu cha mwanafunzi kuanzia moja hadi elfu moja. Katika kujifunza hesabu hizi, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wake wanasoma tarakimu kwa njia inayofaa mpaka mia moja na awaombe kuzitaja bila kuzisoma. Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi ili waweze kuijundia wao wenyewe kanuni zinazowarahisishia kuhesabu mpaka elfu moja kupitia mifano iliyopo katika kitabu cha mwanafunzi. Ni vyema kuwaomba wanafunzi kufunga vitabu vyao ili wafanye zoezi la kwanza katika sehemu hii ambapo kila mwanafunzi anapewa muda ili ahesabu kuanzia moja hadi mia moja. Ni lazima mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanatamka kwa usahihi tarakimu zilizopo kwa kusahihisha makosa pale yanapojitokeza. Mwalimu aendelee kwa kuwaomba wanafunzi wake kufanya zoezi la pili na la tatu kuhusu hesabu baada ya kuhakikisha kwamba wamefunga vitabu vyao. Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wameelewa vizuri, mwalimu aandike mazoezi hayo ubaoni huku wanafunzi wakiendelea kuyafanya au awe ameshaandika kwenye karatasi ambazo anawagawia na kuwaomba wayajibu papo hapo. Baadaye, mwalimu

awaombe wanafunzi kusahihisha mazoezi hayo kwa pamoja.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufahamu aina mbalimbali za vipimo ambavyo hutumiwa katika hesabu. Pia, alama za hesabu ziangaziwe pamoja na matumizi yake katika sentensi.

Hatua ya 5: Kusikiliza na kuzungumza

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi, neno na sentensi katika kifungu cha mazungumzo kinachohusika huku wakijaribu kukariri mazungumzo kati ya muuzaji na mnunuzi. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kuigiza mazungumzo yaliyopo kati ya muuzaji na mnunuzi. Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi mara moja yanapojitokeza. Yaani, awasidie kutamka kwa usahihi herufi, silabi, maneno na sentensi za Kiswahili zilizopo katika kitabu cha mwanafunzi.

Hatua ya 6: Ufahamu

Katika hatua hii ya ufahamu, mwalimu awaelekeze tena wanafunzi kusoma kwa makini na kwa kimya kifungu cha mazungumzo kati ya muuzaji na mnunuzi huku wakiyajibu maswali yaliyotolewa kama maswali ya ufahamu. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

Hatua ya 7: Hitimisho

Katika hatua hii ya mwisho wa somo hili, mwalimu ahitimishe somo kwa kuwa uliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza ili kutambua ikiwa wanaweza kutaja majina ya bidhaa mbalimbali zinazopatikana katika mazingira ya sokoni na kuhesabu kuanzia moja hadi elfu moja. Ili kusaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi wake katika namna ya kujibu zoezi la tatu kuhusu matumizi ya lugha kama kazi mradi. Yaani, kazi ya nje ya darasa. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza somo la pili la mada hii ya msamiati wa mazingira ya sokoni.

e) **Mazoezi ya ziada**

Ili kuwasaidia wanafunzi wa kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaelekeze wanafunzi hao dhaifu kuandika tarakimu zifuatazo:

Swali la kwanza:

Andika tarakimu hizi kwa maneno:

1. 361
2. 490
3. 483
4. 132

5. 761
6. 859
7. 999
8. 888
9. 777
10. 626

Swali la pili:

Andika tarakimu hizi:

1. Mia moja sabini na saba
2. Mia tisa hamsini na tatu
3. Mia tano themanini na nane
4. Mia tatu thelathini na moja
5. Mia saba na sabini

f) Tathmini

Mwalimu atathmini ikiwa ujifunzaji umefanywa kwa kiwango cha kuridhisha. Kwa hiyo, awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kurejelea majina ya bidhaa zipatikanazo sokoni kuitia picha na michoro iliyopo pamoja na vifaa vingine alivyovileta darasani. Vilevile, awaulize maswali mbalimbali kwa kupima uwezo wa wanafunzi wa kutambua shughuli mbalimbali zipatikanazo sokoni kama vile kuza, kununua, kupunguza bei, kupandisha bei na hata mienendo inayotambulisha muuzaji na mnunuzi na jinsi wanavyopaswa kushirikiana ili kila mmoja apate kile anachokitaka.

Zoezi la ufhamu, ukurasa 149 - 150

1. Muuzaji hana machungwa kwa sababu hayapatikani siku hizi.
2. Mnunuzi anataka kununua maembe matatu, nyanya, sukari kilo tatu na chumvi kilo moja na nusu.
3. Embe moja ni faranga hamsini.
4. Muuzaji anauza nanasi, maembe na maparachichi.
5. Mnunuzi anataka maembe matatu.
6. Mnunuzi anataka kununua mafungu matatu ya nyanya.
7. Mnunuzi ananunua kilo moja ya sukari kwa faranga mia sita na hamsini.
8. Mnunuzi ananunua kilo moja na nusu ya chumvi kwa faranga mia mbili.
9. Fungu moja la nyanya analinunua faranga sabini.
10. Muuzaji anamwekeea vitu katika mkoba mzuri.

Zoezi la 1, ukurasa 150 - 151

Wanafunzi wazingatie mifano ya sentensi zilizoandikwa katika Kitabu cha Mwanafunzi na watunge sentensi zao kwa kutumia maneno yaliyopigwa mistari ambayo ni yafuatayo:

1. Bei
2. Rahisi
3. Biashara
4. Kununua
5. Angalia
6. Inauzwa
7. Ghali
8. Mafungu
9. Imepanda.
10. Anapunguza
11. Kunapatikana
12. Mteja
13. Tayari
14. Pesa
15. Mkoba

Zoezi la 2, ukurasa 151 - 152

1. Kaka yangu anauza magari mjini Kigali. Watu wengi wanunua kwake magari mazuri ya aina ya Nissan.
2. Muuzaji huyu ameleta matunda mengi. Yeye anauza maembe, ndizi, nanasi na machungwa.
3. Muuzaji anaweka vitu vya wateja katika mikoba mizuri.
4. Mjini Musanze kuna soko la matunda mengi sana.
5. Mwanamke huyu ana pesa nyingi. Yeye ni mfanyabiashara.
6. Kuna watu wengi wanaonunua viazi vitamu.
7. Mukamana ni mteja wa kaka yangu. Kila siku, yeye hununua vitu vingi katika duka lake.
8. Muuzaji huyu amepunguza bei ya kilo moja ya vitunguu kutoka faranga mia moja hadi faranga hamsini.
9. Mchele umekosekana mjini Huye na bei yake imepanda hadi mia tisa kwa kilo moja.
10. Mama yangu ananituma sokoni. Mimi ninaenda sokoni kununua mafungu mawili ya nyanya.

Zoezi la 1, ukurasa 153

- Wanafunzi wahesabu kuanzia moja hadi mia moja.

Zoezi la 2, ukurasa 153

1. 99: tisini na tisa
2. 77: sabini na saba
3. 219: mia mbili na kumi na tisa
4. 349: mia tatu arobaini na tisa
5. 440: mia nne na arobaini
6. 677: mia sita sabini na saba
7. 798: mia saba tisini na nane
8. 888: mia nane thamanini na nane
9. 933: mia tisa thelathini na tatu
10. 988: mia tisa themanini na nane
11. 88: themanini na nane
12. 54: hamsini na nne
13. 255: mia mbili hamsini na tano
14. 333: mia tatu thelathini na tatu
15. 506: mia tano na sita
16. 705: mia saba na tano
17. 832: mia nane thelathini na mbili
18. 894: mia nane tisini na nne
19. 967: mia tisa sitini na saba
20. 999: mia tisa tisini na tisa

Zoezi la 3, ukurasa 153 -154

1. 69
2. 55
3. 77
4. 84
5. 95
6. 181
7. 144
8. 202
9. 279
10. 319

11. 404
12. 444
13. 483
14. 557
15. 660
16. 633
17. 667
18. 884
19. 966
20. 999

Zoezi la ufahamu, ukurasa 154

1. Baada ya kusafisha vyombo.
2. Lita tatu za mafuta ya kupikia na kilo mbili za mchele.
3. Maziwa
4. Kilometra moja.
5. Mililita mia tano za soda ya Fanta.

Zoezi, ukurasa 155

1. Kilometra
2. Mafuta ya kupikia, soda na maziwa
3. Sukari, nyama na mchele

Zoezi, ukurasa 156

- a) Nne ongeza kumi ni sawasawa na kumi na nane.
- b) Kumi na tano ni ndogo kuliko kumi na saba
- c) Arubaini na nne gawanya kwa kumi na moja ni sawasawa na nne.
- d) Kumi mara kumi ni sawasawa na mia moja.
- e) Tisini ni kubwa kuliko sitini.

Biashara mbalimbali

Muda: Vipindi 3

a) Malengo ya somo

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi
- Kutaja majina ya bidhaa mbalimbali zipatikanazo dukani
- Kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati wa mazingira ya sokoni
- Kuhesabu kuanzia elfu moja hadi elfu kumi
- Kutamka kwa usahihi sauti za kipekee katika Kiswahili; *dh* na *th*.

b) Vifaa vya kujifunzia

- Vinasasauti
- Michoro ya vifaa tofauti vipatikanavyo dukani
- Vifaa vya kitamaduni vinavyouzwa na kununuliwa ili vitumike kama mapambo nyumbani; mikeka, njuga, ngoma, vifaa viliviyotengenezwa kwa udongo. n.k.
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 157

c) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu *wafanyabiashara wazuri* na lina vipindi vitatu. Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kujifunzia somo hili. Mbali na vifaa vya shule vinavyozungumziwa katika kifungu cha habari kinachohusika, vifaa vya kitamaduni vitumiwavyo kama mapambo nyumbani navyo vionyeshwe ili kurahisisha ujifunzaji wa somo hili. Mwalimu ajaribu kuchochea wanafunzi kupata ufahamu kuhusu umuhimu wa vifaa hivyo na kuwaelekeza ili wapate kwamba utamaduni unaweza kuleta faida kubwa katika shughuli za kibiashara. Vilevile, ni vyema mwalimu azingatie wakati unaofaa wa kuonyesha hadharani vifaa alivyovileta ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu atumie vifaa hivyo kwa kuwaomba wao wenyewe kuvigusa huku wakitaja majina ya

vifaa hivyo. Katika somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli inayohusika darasani.

d) **Utaratibu wa somo**

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake nao wajibu maamkizi. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu somo lililopita. Mwalimu awachangamshe wanafunzi wake kwa kuwaauliza maswali kuhusu michoro iliyopo katika kitabu cha mwanafunzi. Kwa mfano, anaweza kuuliza swali lifuatalo; *Mnaona nini kwenye picha hizi?* Wanafunzi watazame picha na michoro iliyopo na kujibu maswali ya mwalimu kwa kuelezea kile kinachoendelea katika picha hizo. Kwa mfano; *Mimi ninaona duka.* Kupitia picha na michoro iliyopo, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tunduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaauliza maswali mengine yanayoingiliana na kile kinachoendelea katika picha husika. *Vitu hivi vinatumwiwa wapi?* *Vitu hivi vina umuhimu gani?* Wanafunzi nao wakifikiri na kugundua matumizi ya vifaa vilivyopo. Kwa mfano: *Vitu hivi vinaapatikana nyumbani.* *Vitu hivi ni mapambo ya nyumbani,* na kadhalika.

Hatua ya 2: Kusoma na kufahamu

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha habari kinachohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Wanafunzi nao wasome kwa kimya kwa kuandika msamiati huo mpya. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu hicho walichokisoma ili kuhakikisha kuwa wamesoma. Kwa mfano, anaweza kuuliza maswali yafuatayo: *Mukamana anafanya nini?* *Muneza anafanya nini?* Wanafunzi kwa upande wao wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hicho. Kwa mfano: *Mukamana anafanya biashara ya kuuza vifaa vya shule.* *Muneza anafanya biashara ya kuuza bidhaa za kitamaduni.* Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu kilichopo, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa sauti kifungu hicho cha habari. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanasoma kwa usahihi na awarekebishe mara moja pale wanapofanya makosa.

Hatua ya 3: Ujifunzaji wa msamiati

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba watafute maana za msamiati mpya waliorodhesha kufuatana na jinsi ulivyotumiwa katika kifungu cha habari walichokisoma. Mwalimu awaombe wanafunzi kutumia kamusi pale panapohitajika na azunguke darasani kuwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kusoma sentensi walizopewa na kujadiliana kuhusu maana za msamiati uliopigwa

mistari huku wakitunga sentensi zao wenyewe. Ni vyema mwalimu azunguke pia darasani ili kusaidia na kuelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe kusahihisha kwa pamoja zoezi hilo. Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wameelewa msamiati uliopo, mwalimu achukue fursa hii kuuliza kama kuna msamiati wowote ambao hawajaelewa ili maana yake ijadiliwe kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika kifungu cha mazungumzo kilichopo. Katika hatua hii ya ujifunzaji wa msamiati, ni vyema mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio unaomwonyesha kwamba wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tunduizi, usuluhisho wa matatizo na mawasiliano katika lugha rasmi. Kwa hivyo, awaelekeze ipasavyo ili sentensi zinazotungwa na mifano inayotolewa iwe na maana inayotakikana katika kumpa mwanafunzi ujuzi wa aina tofauti.

Hatua ya 4: Matumizi ya lugha

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize kwanza wanafunzi maswali machache kwa kurejelea hesabu walizojifunza katika somo lililopita. Yaani, achunguze ikiwa wanawenza kuhesabu kuanzia moja hadi elfu moja. Baadaye, aendelee kwa kuwaomba wasome tarakimu zilizopo katika kitabu cha mwanafunzi kuanzia elfu moja hadi elfu kumi. Katika kujifunza hesabu hizi, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanasoma tarakimu zilizopo kwa njia inayofaa kwa utambuzi wa herufi na silabi zilizopo katika maneno husika. Kupitia mifano ya hesabu iliyopo katika kitabu cha mwanafunzi, mwalimu awaelekeze wanafunzi ili waweze kuijundia kanuni zinazowarahisishia kuhesabu mpaka elfu kumi. Hivyo basi, mwalimu awaombe wanafunzi kufanya zoezi la kwanza na la pili katika sehemu hii na azunguke darasani kurahisha ujifunzaji wa hesabu katika sehemu hii. Wanafunzi wafanye mazoezi hayo kulingana na maelekezo ya mwalimu na kuyasahihisha kwa pamoja mara moja wanapomaliza.

Hatua ya 4: Kusikiliza na kuzungumza

Hatua hii inahusu kusikiliza na kuzungumza. Mwalimu awaombe kwanza wanafunzi kusoma maneno yaliyopo katika kitabu cha mwanafunzi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutofautisha kwanza sauti za *dh* na *th* kuitopia maneno walijotolewa. Halafu, tofauti za kimatamshi kati ya *d* na *dh*, *t* na *th* nazo zibainishwe. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanatamka kwa njia mwafaka sauti hizo na awarekebishe pale wanapofanya makosa. Hivyo basi, wanafunzi wasome maneno yaliyopo mmoja baada ya mwingine kwa kuzingatia maelekezo ya mwalimu. Ili kuthibitisha kwamba wanafunzi hawa wameelewa tofauti kati ya sauti hizo, ni vyema mwalimu agawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu na kuwaomba watafute maneno mengine yenye sauti hizo.

Aidha, mwalimu aendelee kwa kuwasomea maneno na vifungu vya maneno vifuatavyo ili waviandike katika madaftari yao:

*theluthi, thelathini, dhima, dharura, thamani, ghali,
dini, idhini, tafadhali, dawa, dhambi, thamani, tamaa*

Muuzaji anaomba nyongeza ya vitunguu vitatu.

Mfanyabiashara anauzu bidhaa zake.

Anathibitisha kauli yake.

*Bei ya lita moja ya mafuta ya kupikia ni faranga mia saba
na thelathini.*

Katika zoezi hili la imla, mwalimu azingatie kwamba maneno yaliyopo yanabeba sauti zenye utata kwa wanafunzi pale ambapo baadhi yake yana silabi ambazo hawajazizoea katika lugha yao ya mama. Kwa mfano, anaweza kusisitiza matamshi ya mfuatano wa irabu mbili ambazo zinajitokeza katika silabi tofauti na sauti nyingine za kipekee katika Kiswahili kama vile *gh*, *dh* na *th*. Hali hii ichochee wanafunzi kutafiti kuhusu maneno mengine yenye kuwa na sifa hizo katika lugha ya Kiswahili kama njia ya ujifunzaji wa kudumu pale ambapo wanafunzi wanaweza kutumia maneno hayo katika mawasiliano yao na watu wengine katika lugha rasmi.

Isitoshe, mwalimu awaelekeze wanafunzi ili wafanye zoezi la pili na la tatu katika sehemu hii ambapo katika makundi yao ya wanafunzi watatu, wanajadiliana kwanza kuhusu mienendo na tabia za mfanyabiashara mzuri na za mfanyabiashara mbaya. Ili kufanya mazoezi haya kwa njia inayofaa, mwalimu awaombe wanafunzi kujadiliana kuhusu kazi ambazo wangependa kuzifanya baada ya kumaliza masomo yao. Wanafunzi nao wajadiliane kulingana na maelekezo ya mwalimu wao. Baadaye, mwalimu aliombe kila kundi lijitekeze mbele ya darasa kuwaelezea wenzao kile walichokubaliana katika kundi lao. Mwalimu achukue fursa hii kuchochea wanafunzi ili wapate mienendo inayotarajiwa katika shughuli yoyote wanayodhamiria kuifanya katika maisha yao. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kupata ujuzi kuhusu tafakuri tunduizi, ubunifu na ugunduzi, usuluuhisho wa matatizo yanayoweza kujitokeza, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha na jinsi ya kutafiti kuhusu mienendo mizuri na kazi zinazowezekana. Wanafunzi wajadiliane kuhusu mambo hayo na waelekezwe kwamba kazi yoyote inaweza kuinua maisha ya yule anayefanya kama imefanywa vizuri.

Hatua ya 6: Ufahamu

Katika hatua hii ya ufahamu, mwalimu awaombe tena wanafunzi kusoma kwa makini na kwa kimya kifungu cha habari kuhusu ‘*Biashara mbalimbali*’huku wakiyajibu maswali yaliyotolewa kama maswali ya ufahamu. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

Hatua ya 7: Hitimisho

Katika hatua hii ya mwisho wa somo hili, mwalimu ahitimishe kwa kuuliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee kwa mfano kuchunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kutaja majina ya bidhaa mbalimbali zipatikanazo dukani , kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati wa mazingira ya sokoni, kuhesabu kuanzia elfu moja hadi elfu kumi na kutofautisha sauti *dh* na *th*. Ili kusaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi namna ya kujibu zoezi la kwanza katika sehemu ya *kusikiliza na kuzungumza*. Zoezi hili lifanywe kama zoezi la nje ya darasa, yaani kama kazi mradi kwa wanafunzi. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza somo la tatu la mada hii ya msamiati wa mazingira ya sokoni.

e) Mazoezi ya ziada

Mwalimu aulize maswali yafuatayo katika zoezi la ziada ambapo anatarajia kuinua kiwango cha chini kwa wanafunzi dhaifu.Yaani, wanafunzi wasioweza kuelewa haraka kama wenzao.

Swali la kwanza:

Andika tarakimu hizi kwa maneno:

1. 3613
2. 4394
3. 5483
4. 6131
5. 7601
6. 8519
7. 9096
8. 2808
9. 7107
10. 6623

Zoezi la pili:

Andika tarakimu hizi:

1. *Elfu moja mia moja sabini na saba*
2. *Elfu nne mia tisa tisini na tatu*
3. *Elfu tisa mia tano themanini na moja*
4. *Elfu tano mia tatu sabini na moja*
5. *Elfu nane mia saba sabini na tisa*

f) Tathmini

Katika sehemu hii, mwalimu atathmini ikiwa malengo ya somo zima yameafikiwa kwa kiwango alichokitarajia. Hivyo basi, awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu majina ya bidhaa zipatikanazo dukani, maswali kuhusu vitendo na mienendo inayotakikana katika shughuli za biashara na arejelee picha zilizotumiwa kujifunzia somo hili ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wameelewa. Vilevile, mwalimu achunguze ujuzi wa wanafunzi katika kudumisha mawasiliano katika lugha rasmi kuitia msamati uliopatikana katika kifungu cha habari kilichopo. Ni vyema pia mwalimu achunguze ikiwa wanafunzi wameshatambua umuhimu wa kuheshimu wateja na ushirikiano mwema unaotakikana kati ya mnunuzi na muuzaji. Mwishowe, mwalimu aulize maswali kwa kupima uwezo wa wanafunzi wa kuhesabu mpaka elfu kumi.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 158

Soma tena kifungu cha habari hapo juu kuhusu “Biashara mbalimbali” kisha, jibu maswali yafuatayo.

1. Mukamana anafanya biashara yake mjini Karongi.
2. Msimamizi wa wafanyabiashara huko Karongi ni Mukamana.
3. Yeye anaomba wafanyabiashara kuheshimu wateja wao na kuacha kufanya dhambi kwa kuwaibia na kuwanyang’anya pesa zao.
4. Mukamana anafanya biashara ya kuuza bidhaa mbalimbali, hasa vifaa vya shule ; daftari, rula, vitabu vya kusoma, kalamu, penseli, karatasi, vifutio, chaki na kadhalika.
5. Muneza anauza bidhaa za utamaduni wa Rwanda.
6. Muneza anapata faida ya faranga elfu tano kila siku.
7. Wengi wa wateja wa Muneza wanatoka katika nchi za Afrika ya Mashariki: Kenya, Tanzania, Uganda na Burundi.
8. Wengi wa wateja wake wanazungumza lugha ya Kiswahili.
9. Mtoto wake anataka kuanzisha pia biashara yake mjini Kigali baada ya kumaliza masomo yake.

Zoezi la I, ukurasa 159

Wanafunzi wazingatie mifano ya sentensi zilizoandikwa katika kitabu cha mwanafunzi na watunge sentensi zao kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mistari ambayo ni yafuatayo:

1. Baadhi
2. Idhini
3. Usiwadharau

4. Dhambi.
5. Dhima
6. Thamani
7. Bidhaa
8. Anadhamiria
9. Kunyang'anya
10. Utamaduni

Zoezi la 2, ukurasa 159 - 160

1. Katika mji huu kuna biashara ya kuuza bidhaa za aina nyingi.
2. Jiepushe na kufanya dhambi kwa kunyang'anya watu wasiojiweza.
3. Wanafunzi wote wanadhamiria kupata alama nzuri katika somo la Kiswahili.
4. Wafanyabiashara wabaya wanadharau wateja wao.
5. Yeye ana idhini ya kuanzisha shule ya sekondari kule kijiji Bugarama.
6. Shangazi yangu ana duka la mavazi mjini Muhanga. Yeye anapata faida kubwa.
7. Rais wa Jamhuri ya Rwanda anaomba Wanyarwanda kudumisha amani ili uchumi uweze kustawi vizuri.
8. Kiswahili kina dhima kubwa katika mawasilano na kinatumika sana katika shughuli za kibiashara, Afrika Mashariki.
9. Utamaduni wa Wanyarwanda una thamani kubwa na unavutia wageni wengi wanaokuja nchini.
10. Acha kunyang'anya watu na kuwaibia pesa zao. Sheria ya Rwanda inaweza kukupa adhabu kali.

Zoezi la majadiliano, ukurasa 160

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, jadiliana kuhusu mienendo ya mfanyabiashara mzuri halafu mjitokezee mbele ya darasa na kuwaelezea wenzenu kuhusu mienendo hiyo.

Baadhi ya mienendo ya mfanyabiashara mzuri:

- Kukaribisha wateja wake kwa heshima.
- Kuheshimu wateja wake kwa kusikiliza maombi yao na kuongea nao vizuri.
- Kupima kwa njia nzuri kile anachoomba mteja bila kumwibia.
- Kuwapa wateja huduma nzuri.
- Kutunza bidhaa zake kwa njia nzuri ili zisiharibike.
- Kulipa ushuru au kodi kwa serikali.

- Kufanya kazi yake kwa njia halali.
- Kuzingatia mahitaji ya wateja wake.

Zoezi la kujieleza, ukurasa 160

Elezea wenzako kazi unayodhamiria kuifanya baada ya kumaliza masomo yako.

Baadhi ya kazi zinazoweza kutajwa na wanafunzi:

- Kufanya biashara za kibinafsi kama vile kuanzisha kampuni, kufanya kazi katika makampuni ya watu wengine
- Kufanya kazi ya serikali kama vile; ualimu, udaktari, uongozi, na kadhalika

Zoezi la I, ukurasa 161

Andika tarakimu hizi kwa kutumia maneno:

1. Elfu moja mia sita sitini na sita
2. Elfu mbili na ishirini na moja
3. Elfu mbili na tisini na tano
4. Elfu sita mia tisa sitini na moja
5. Elfu saba mia sita hamsini na nane
6. Elfu tano mia mbili na kumi na tisa
7. Elfu moja mia mbili thelathini na sita
8. Elfu moja mia saba arubaini na nane
9. Elfu mbili na thelathini na sita
10. Elfu mbili mia tano sitini na tisa
11. Elfu nane mia tatu sitini na tisa
12. Elfu sita mia nne ishrini na nane
13. Elfu nne mia saba sitini na tano
14. Elfu moja mia tatu na sitini
15. Elfu moja mia nne sitini na tisa
16. Elfu mbili na sabini
17. Elfu tatu mia tatu arubaini na nane
18. Elfu tisa mia sita na kumi na mbili
19. Elfu tano mia tisa sabini na nne
20. Elfu tatu mia tisa sabini na tatu

Zoezi la 2, ukurasa 161-162

A. Andika tarakimu zifuatazo.

1. 3555
2. 7993
3. 6082
4. 4044
5. 2202
6. 3039
7. 4088
8. 6999
9. 5772
10. 9984

B. Kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 162

Soma kwa usahihi maneno yafuatayo.

- Wanafunzi wasome kwa kutofautisha sauti za *th* na *dh*.
- Wanafunzi wasome kwa kutofautisha sauti za *d* na *dh*.
- Wanafunzi wasome kwa kutofautisha sauti *t* na *th*.

Zoezi la imla, ukurasa 163

Funga kitabu chako, kisha katika daftari lako, andika kwa usahihi maneno na vifungu vya maneno utakavyosomewa na mwalimu wako.

- theluthi, thelathini, dhima, dharura, thamani, ghali, dini, idhini, tafadhali, dawa, dhambi, thamani, tamaa
- Muuzaji anaomba nyongeza ya vitunguu vitatu.
- Mfanyabiashara anauza bidhaa zake.
- Anathibitisha kauli yake.
- Bei ya lita moja ya mafuta ya kupikia ni faranga mia saba na thelathini.

Mazingira ya Sokoni

Muda: Vipindi 4

a) **Malengo ya somo**

Kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha habari kinachohusika kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi.
- Kutunga sentensi fupifupi kwa kutumia msamiati wa mazingira ya sokoni.
- Kutambua vivumishi vya idadi katika sentensi fupi fupi.
- Kutumia vivumishi vya idadi katika sentensi fupi fupi.

b) **Nyenko/Vifaa vya kujifunzia**

- Vinasasauti
- Vifaa vya shule kama vile; vitabu, kalamu, kifutio, ubao, chaki, n.k.
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 164
- Michoro ya watu mbalimbali katika shughuli zao sokoni

c) **Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu *biashara ya mamangu* na lina vipindi vinne. Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kujifunzia somo hili. Kwa mfano, mwalimu alete bidhaa tofauti zinazouzwa na kununuliwa sokoni, michoro inayodhihirisha mazingira ya sokoni ambapo wanunuza na wauzaji hupatanikana na kuongea dhidi ya bei za bidhaa hizo. Mbali na hayo, mwalimu akumbuke kwamba vivumishi vya idadi ni jambo muhimu katika kufanikisha mawasiliano kati ya mnunuzi na muuzaji. Hivyo basi, ajiandae ipasavyo ili aweze kuwaelekeza wanafunzi katika kutambua viambishi mwafaka vinavyotumiwa kulingana na jina pamoja na idadi inayorejelewa katika sentensi zinazotolewa. Mwalimu azingatie kwamba baadhi ya vivumishi hivyo, vya idadi havichukui viambishi vya nomino ilhali vivumishi vingine vinatumia viambishi kulingana na nomino au jina linalovumishwa.

Aidha, mwalimu aamue wakati unaofaa wa kuonyesha hadharani vifaa alivyovileta ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu atumie vifaa hivyo kwa kuwaomba wao wenye we kuvigusa huku wakitaja majina ya vifaa hivyo. Katika somo hili, mwalimu atahakikisha kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli inayohusika darasani.

d) **Utaratibu wa somo**

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu awaamkue wanafunzi wake na kuwaauliza maswali kuhusu somo lililopita na wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu wao. Mwalimu achukue fursa hii kusahihisha kazi iliyotolewa wanafunzi kama kazi mradi. Mwalimu alichangamshe darasa lake kwa kuwaauliza wanafunzi maswali kuhusu michoro iliyoko katika kitabu cha mwanafunzi. Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye picha hizi?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu maswali waliooulizwa. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao. Kwa mfano: *Mimi ninaona soko.* Katika sehemu hii, mwalimu agusie maswali yanayoolekeza wanafunzi kutafakari kuhusu nafasi ya wanawake katika shughuli za kibiashara zipatikanazo sokoni na umuhimu wake kwa familia nzima. Masuala mengine yazushwe kuhusiana na uwezo wa walemovu amba o na wanaweza kujitafutia kazi mbalimbali sokoni na kuendeleza maisha yao bila kutegemea watu wengine. Mwalimu aandae vizuri hoja na mifano kadhaa zinazoweza kuchochea wanafunzi kupata ujuzi kuhusu tafakuri tunduizi na stadi za kutafiti kuhusu kazi nyaginezo zinazoweza kufanywa na kuboresha maisha ya watu wenye uwezo mdogo.

Hatua ya 2: Kusoma na kufahamu

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha habari kinachohusika huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Hivyo basi, wanafunzi wasome kwa kimya huku wakiandika msamiati huo. Baada ya kusoma kwa kimya, mwalimu awaaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu hicho ili kuhakikisha ikiwa wamesoma. Aulize kwa mfano: *Mimi ninaitwa nani? Mama yangu anafanya nini?* Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao kulingana na yale walioyasoma katika kifungu hicho. Kwa mfano: *Mimi ninaitwa Mugenzi. Mama yangu anafanya biashara sokoni Nyamasheke.* Hatimaye, mwalimu aulize wanafunzi kusoma kwa sauti kifungu cha mazungumzo kinachohusika na wanafunzi wasome kwa sauti mmoja baada ya mwengine. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanasoma kwa usahihi na kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi huku akisahihisha pale ambapo wanafanya makosa. Mwalimu ahakikishe pia kwamba wanafunzi wanasoma kwa kuzingatia matumizi ya alama mbalimbali za uakifishaji katika kifungu cha habari kilichopo.

Hatua ya 3: Ujifunzaji wa msamiati

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na awaombe kutafuta maana za msamiati mpya waliokutana nao wakati wa kusoma kifungu cha habari kilichopo. Wanafunzi nao wajadiliane na watumie kamusi pale wanapoihitaji ili kutafuta maana za msamiati huo. Wazingatie pia matumizi yake katika kifungu cha habari walichokisoma na mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanaotatizika na kuwaelekeza katika matumizi ya kamusi hiyo. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kufanya zoezi la kwanza la msamiati kwa kuwafafanulia kile kinachotarajiwa katika zoezi hilo. Hivyo basi, wanafunzi wachunguze michoro iliyopo na kuihusisha na majina ya matunda na bidhaa nyingine yaliyoandikwa katika kitabu cha mwanafunzi. Hatimaye, mwalimu ashirikishe wanafunzi wote kusahihisha zoezi la msamiati.

Hatua ya 4: Matumizi ya lugha

Hatua hii inahusu matumizi ya lugha. Kwa hivyo, mwalimu alenge kuwasaidia wanafunzi kupata ujuzi na stadi katika kuwasiliana katika lugha rasmi kuitopia mjadala uliotolewa katika kitabu cha mwanafunzi. Mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kuelezeana kwanza kuhusu aina za biashara zipatikanazo sokoni huku wakibainisha zile ambazo wangefurahia kuzifanya. Ili kuimarisha ujuzi wa wanafunzi kuhusu tafakuri tunduizi na usuluhishaji wa matatizo, ni vyema mwalimu awaombe wanafunzi kutoa sababu za uchaguzi wanaoufanya kuhusu biashara hizo wanazozipenda. Mwalimu awatolee mfano wa biashara kama vile biashara ya ushonaji nguo na viatu. Hali hii ichochee wanafunzi katika kugundua aina nyingine za biashara zinazofanya na mwalimu awaelekeze ili waweze kutetea hoja na mifano ya biashara ambazo wangependa kuzifanya huku wakibainisha umuhimu na faida ambazo wangeweza kuzipata kutokana na biashara hizo.

Hatua ya 5: Ujifunzaji wa sarufi - Vivumishi vya idadi

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kusoma sentensi zilizopo kwa kutilia mkazo utambuzi wa sifa za vifungu vya maneno vilivyopigiwa mstari. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuwaonyesha kuwa kila sentensi iliyotolewa inafuatwa na swali linalouliza kuhusu idadi ya vitu vilivyzungumziwa katika sentensi hiyo. Wanafunzi nao wajigawe na kujadiliana kuhusu sentensi hizo ili waweze kufanya zoezi linalofuata. Katika uchunguzi wao, wanafunzi wapate kwamba katika kuuliza swali kuhusu idadi ni lazima watumie kiulizi *ngapi* na kukiambatanisha na kiambishi kinachofanana na kile kilichotumiwa katika jina linalotaja vitu vinavyoelezewa na idadi iliyopo. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kufanya zoezi la kwanza la sehemu ya sarufi. Hivyo basi, awaelekeze kwa kuwafafanulia mfano uliopo ambapo anaweka mkazo katika matumizi ya neno linalotaja idadi na kiulizi *ngapi*. Wanafunzi kwa upande wao, wafanye zoezi hilo kwa kuzingatia maelekezo ya mwalimu wao na kusahihisha kwa pamoa wanapomaliza zoezi hilo.

Kupitia majibu yaliyotolewa na wanafunzi pamoja na mifano iliyopo katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu uundaji wa kanuni ya kutumia neno ngqipi. Mwalimu achukue fursa hii kuwaambia wanafunzi kwamba maneno yanayotaja idadi za vitu ni vivumishi nya idadi. Ili kudumisha ujifunzaji wa matumizi ya vivumishi nya idadi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu jinsi ya kujibu swali la sehemu ya sarufi. Wanafunzi watunge sentensi zao kwa kutumia vivumishi nya idadi na kutoa maswali kuuliza idadi zilizotumiwa katika sentensi hizo. Aidha, mwalimu awaombe wanafunzi kuchunguza sentensi zilizotolewa katika zoezi la nne na kujadiliana kuhusu sifa za vifungu vilivyopigiwa mistari. Kupitia zoezi hili, mwalimu achunguze ikiwa wanafunzi wametambua matumizi ya vivumishi nya idadi pamoja na majina yanayohusika kwa kutilia mkazo vivumishi visivyokubali kuchukua viambishi nya majina kama vile sita, saba, tisa na kumi. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi kufanya zoezi la sarufi kama njia binafsi ya kuchunguza matatizo yaliyopo katika matumizi ya aina hii ya vivumishi. Wanafunzi wafanye zoezi hili na kulisahihisha wanapolikamilisha. Katika kurahisha ujifunzaji wa matumizi ya idadi katika sentensi, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi ili waweze kuijundai kanuni inayohusika na matumizi ya vivumishi nya idadi huku akirejelea mifano ya sentensi walizozitunga na mifano mingine inayoeleweka.

Hatua ya 6: Kusikiliza na kuzungumza

Hatua hii inahusu kusikiliza na kuzungumza. Hivyo basi, mwalimu awaombe wanafunzi kufunga vitabu vyao na aendelee kwa kuwasomea sentensi zifuatazo ili waziandike katika madaftari yao.

- i. *Dadangu Mukamusoni ananunua bidhaa nzuri na kuziwa sokoni.*
- ii. *Dhima ya biashara ni kutajirisha watu kwa kuwatoa katika umaskini.*
- iii. *Mwizi amekamatwa na polisi kwa kuwaibia wafanyabiashra na wateja wao katika soko la Nyamasheke.*
- iv. *Usimdharaa mtu kwa biashara ndogondogo anayoifanya.*
- v. *Fanya kazi yako kwa bidii ili uweze kutajirika na usimdhulumu mnyonge.*
- vi. *Ni lazima kila mfanyabiashara aliipe kodi kulingana na faida anayoipata.*
- vii. *Kodi inadhamiria kuinua uchumi wa nchi na kuiendeleza.*
- viii. *Biashara ya mamangu ina thamani kubwa.*
- ix. *Mukamusoni anaiza bidhaa nyngi sokoni Nyarugenge.*
- x. *Mhudumie mteja wako na usimdharaa kamwe.*

Katika zoezi la imla, mwalimu azingatie kwamba maneno yaliyopo yana utata kwa wanafunzi pale ambapo baadhi yake yana silabi ambazo wanafunzi hawajazizoea katika lugha yao ya mama kama vile mfuatano wa irabu mbili ambazo zinajitokeza katika silabi tofauti, matumizi ya sauti *dh, th, l, r* na *m* yenye kutumiwa kama silabi isiyo na irabu ambazo ni katika lugha ya Kiswahili. Hali hii iwachochee wanafunzi kutafiti kuhusu maneno mengine yenye kuwa na sifa hizo katika lugha ya Kiswahili kama njia ya ujifunzaji wa kudumu kwa wanafunzi pale wanapoweza kutumia maneno hayo katika mawasiliano yao na watu wengine bila tatizo lolote.

Hatua ya 7: Ufahamu

Katika hatua hii ya ufahamu, mwalimu awaombe tena wanafunzi kusoma kwa makini na kwa kimya kifungu cha habari kuhusu *Biashara ya mamangu* huku wakijibu maswali yaliyotolewa kama maswali ya ufahamu. Wanafunzi nao wasome kama walivyoambwi na mwalimu na kujibu maswali waliyopewa. Baadaye, wanafunzi wote washirikishwe kwa kusahihisha maswali hayo.

Hatua ya 8: Hitimisho

Katika hatua hii ya kuhitimisha somo hili, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza ili kuhakikisha kama wanaweza kurejelea majina ya bidhaa zilizozungumziwa katika somo hili. Vilevile, maswali kuhusu matumizi ya vivumishi vya idadi na kiulizi *ngapi* nayo yaulizwe wanafunzi huku yakilenga kuwapa picha kamili ya utambuzi wa vivumishi hivyo na matumizi yake sahihi katika sentensi. Ili kusaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu zoezi la tatu la sehemu ya sarufi na kuwaomba walifanye kama kazi mradi . Yaani kazi ya kufanya nje ya darasa. Zoezi hili litasahihishwa kabla ya kuanza somo litakalofuata.

e) **Mazoezi ya ziada**

Mwalimu awatake wanafunzi dhaifu, yaani wanafunzi wa kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, kujibu maswali katika zoezi lifuatalo.

Swali la kwanza:

Soma tena kifungu cha habari kuhusu biashara ya mamangu kisha uandike vifungu vya maneno vyenye kuzingatia majina pamoja na vivumishi vya idadi.

Swali la pili:

Tunga sentensi tano kwa kutumia neno ngapi.

f) Tathmini

Katika sehemu hii ya tathmini, mwalimu alenge kutambua ikiwa ujifunzaji umefanywa kwa namna ya kuridhisha. Kwa hivyo, aulize maswali tofauti yenyе kudhamiria kuchunguza uwezo wa wanafunzi katika kutaja bidhaa zinazopatikana sokoni, huduma na kazi nyingine zinazoweza kufanywa sokoni na kuleta faida. Vilevile, maswali mengine yapime uwezo wa wanafunzi katika kuonyesha mienendo mizuri ya mfanyakibashara kama vile kupokea na kushirikiana na wateja wake na kulipa ushuru. Vilevile, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuonyesha ujuzi wao wa kutafakari na kukuza stadi zao za utafiti kuhusu mienendo hiyo na aina tofauti za biashara zinazofanywa na kuleta faida. Aidha, sehemu hii ya tathmini ichunguze pia ujuzi wa wanafunzi kuhusu matumizi ya vivumishi vya idadi kwa kuuliza wanafunzi maswali kadhaa yenyе kiulizi *ngapi* ambapo wanafunzi wanajibu kwa kutumia majina pamoja na kivumishi cha idadi na hata kuijundia sentensi zao fupi fupi zenyе vivumishi hivyo vya idadi.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 165

1. Mama ya mugenzi anafanya biashara yake sokoni Nyamasheke.
2. Yeye hurudi nyumbani jioni.
3. Yeye huleta sambusa, mkate, machungwa, mapera, ndizi, nanasi na mapapai.
4. Mama huuza parachichi moja kwa faranga thelathini.
5. Nyumbani kuna vitanda vitano.
6. Vitanda vya wageni ni viwili.
7. Mama huleta mkate mmoja.
8. Mama huleta nanasi moja.
9. Katika fungu la vitunguu, mama huweka vitunguu vitano.
10. Mugenzi ana ndugu wawili.

Zoezi la I, ukurasa 165 - 167

I - e	2 - g	3 - h	4 - i	5 - f
6 - j	7 - k	8 - d	9 - b	10 - c 11 - a

Zoezi la I, ukurasa 167 - 168

1. Watoto hawa wanakula pamoja mapera mangapi?
2. Wanyarwanda wangapi wametoa mchango wao katika akiba ya kujiendeleza AGACIRO?
3. Mwanafunzi mbaya amepoteza vitabu vingapi?
4. Baba amepanda minanasi mingapi?
5. Nyumbani tuna wageni wangapi?

6. Darasa letu lina wanafunzi wangapi?
7. Mamangu amenunua nyumba ngapi?
8. Mkulima huyu ana faranga ngapi katika benki ya Kigali?
9. Mimi ninapeleka faranga zangu ngapi katika chama cha ushirika UMURENGE SACCO TWITEZIMBERE?
10. Wanaume wangapi wanaelewa umuhimu wa usawa wa kijinsia?

Zoezi la 2, ukurasa 168

Sentensi kumi zitungwe kwa kutumia **idadi** katika sentensi inayotangulia na neno **ngapi** katika sentensi inayoifuata kuulizia idadi iliyopo katika sentensi tangulizi.

Kwa mfano: S1: Wafanyabiashara wadogo wanalipa kodi ya faranga **elfu sitini** kwa mwaka.

S2: Wafanyabiashara wadogo wanalipa kodi ya faranga **ngapi** kwa mwaka?

Zoezi la 1, ukurasa 170

Uchunguzi wa sentensi unaweza kubainisha sifa zifuatazo za vifungu vilivypigiwa mstari:

Maneno: **mmoja, wawili, watatu, wanne, watano, sita, saba, wanane, tisa, kumi, kumi na mmoja, kumi na wawili, kimoja, viwili, vitatu, vinne, vitano, sita, saba, vinane, tisa, kumi, kumi na kimoja, kumi na viwili,** yanaelezea idadi ya watu na vitu vinavyotajwa.

Maneno hayo ni vivumishi vya idadi. Vivumishi sita, saba, tisa na kumi havichukui viambishi vya majina.

Zoezi la 2, ukurasa 170 - 171

Mwalimu atathmini usahihi wa sentensi za wanafunzi.

Zoezi la 3, ukurasa 171

Andika sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno katika idadi zilizowekwa.

Kwa mfano: Hospitalini kuna wagonjwa 123

Jibu: Hospitalini kuna wagonjwa **mia moja ishirini na mmoja**

1. Mugabo anaiza vitanda kumi na tisa.
2. Mama yangu ameuza mafungu thelathini na matatu ya nyanya.

3. Baba yangu ana magari mawili.
4. Wanafunzi elfu mbili mia tatu hamsini na mmoja wanajifunza Kiswahili.
5. Shule yangu ina majengo saba mazuri.
6. Watoto elfu sita mia tisa sabini na wanane wamefaulu mitihani yote.
7. Mkulima amepanda miti elfu moja mia tano thelathini na mmoja. Yeye anatunza vizuri miti yake.
8. Mfanyabiashara mzuri ameuza viatu elfu tatu mia sita sabini na vinane katika mwezi huu.
9. Nyumba ya baba yangu ina milango mitatu na madirisha manne.
10. Walimu watano wa darasa langu wanafundisha masomo kumi.

Zoezi la imla, ukurasa 171

Funga kitabu chako, kisha katika daftari lako, andika kwa usahihi sentensi utakazosomewa na mwalimu wako.

- a. *Dadangu Mukamusoni ananunua bidhaa nzuri na kuziuba sokoni.*
- b. *Dhima ya biashara ni kutajirisha watu kwa kuwatoa katika umaskini.*
- c. *Mwizi amekamatwa na polisi kwa kuwaibia wafanyabiashara na wateja wao katika soko la Nyamasheke.*
- d. *Usimdhara mtu kwa biashara ndogondogo anayoifanya.*
- e. *Fanya kazi yako kwa bidii ili uweze kutajirika na usimdhulumu mnyonge.*
- f. *Ni lazima kila mfanyabiashara aliye kodi kulingana na faida anayoipata.*
- g. *Kodi inadhamiria kuinua uchumi wa nchi na kuiendeleza.*
- h. *Biashara ya mamangu ina thamani kubwa.*
- i. *Mukamusoni anauza bidhaa nyngi sokoni Nyarugenge.*
- j. *Mhudumie mteja wako na usimdhara kamwe.*

MADA KUU: MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI

Mada Ndogo:

Matumizi ya msamiati kuhusu usafi wa mwili

Idadi ya Vipindi: 12

Ujuzi upatikanao katika mada hii:

- Kusikiliza
- Kusoma
- Kutamka na kuandika kwa kutumia kwa ufasaha msamiati kuhusu viungo vya mwili wa binadamu pamoja na vitendo fulani katika usafi wake.

Vifaa vya Kujifunza:

- Skeletoni
- Picha au michoro ya mwili wa binadamu
- Mwanafunzi fulani
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 174
- Vinasasauti

Kigezo cha Tathmini na Upimaji

- Uwezo wa kueleza mwili wa binadamu na kuweka majina ya viungo muhimu,
- Kueleza umuhimu ama kazi ya kila kiungo,
- Kuweza kutumia kwa usahihi, katika mawasiliano, umoja na wingi wa sehemu mbalimbali za mwili.

(a) Maelezo kwa mwalimu: Utangulizi wa mada

Mada hii inashughulikia msamiati na afya ya mwili wa binadamu katika mazingira ya mwili wa binadamu. Mwalimu atambue sehemu zote muhimu zinazohitaji usafi na umuhimu wa kufanya hivyo. Mwalimu atumie michoro au picha na skeletoni kuelekeza somo hili. Mwalimu afahamu kuwa somo hili linahusiana na somo la Bayolojia na ushirikiano na walimu husika na elimu ya somo hili ni muhimu katika kufanikisha malengo ya somo hili la Kiswahili.

Mwalimu pia atambue kwamba usafi, afya na magonjwa ni masomo mengine hasa kupitia elimu ya tiba na kinga za mwili pamoja na makala mengi yanayohusu afya na

tiba, kupitia hospitali na zahanati. Kwa hivyo, njia nyingine bora za kulikabili somo hili ni pamoja na:

- a) Kumwalika afisa wa afya kuzungumza na wanafunzi.
- b) Kumwalika mhudumu wa afya na tiba kama nesi ama daktari
- c) Kuwapeleka wanafunzi kuzuru ofisi za afya na hospitali ama zahanati
- d) Kuwaalika maafisa wa mazingira na huduma za kijamii
- e) Kutumia mifano dhahiri – kwa mfano; kuwahoji wanafunzi wenyewe kuhusu afya na usafi.
- f) Kumwalika mkuu wa dini kuzungumzia usafi wa mwili na utakatifu
- g) Kumwalika mshauri wa masuala ya jamii na mahusiano

Afyu mbaya ina madhara mengi kwa mhusika:

- Inaweza kusababisha kujitenga ama kutengwa
- Inaweza kusababisha kifo (vifo)
- Inaweza kusababisha uambukizaji wa maradhi zaidi
- Inaweza kuvunja uhusiano
- Inaweza kusababisha harufu mbaya
- Humzuia mtu kutekeleza majukumu mengine n.k.

Mwalimu asisitize kuwa bila usafi na afya ya mwili binadamu hawezi kushiriki barabara katika ujenzi wa jamii na taifa.

- Pesa nyingi zitaishia hospitali
- Uchumi utazorota kwa kukosa wafanyakazi wenyewe afya
- Tutakosa viongozi
- Majirani watatuepuka
- Itakuwa vigumu kupata mchumba na kuendeleza kizazi

TAZAMA: Kabla ya kufundisha kijisehemu chochote katika somo hili na yale mengine, maelezo ya utangulizi, ufanuzi wa mada na vipengele ni muhimu. Pale ambapo msisitizo unahitajika ifanywe hivyo kwa uangalifu na iwe sharti.

Mwalimu atumie somo hili kukuza ushirikiano mionganoni mwa wanafunzi, kueneza kampeni kuhusu mazingira bora na umuhimu wa kujikinga na maradhi ambukizi na yanayoletwa na mazingira mabovu kama: malaria, kipindupindu, kifua kikuu na homa ya matumbo . Mwalimu afafanue maradhi haya na yanavyoambukiza na kuathiri afya ya mwanadamu.

Mwalimu pia achukue fursa hii kueleza jinsi ambavyo tunaweza kuweka mikakati ya kulinda mazingira, kuishi vyema na majirani, kuzuia kelele, moshi wa magari na kuchoma vitu, maji na njia mpya za mawasiliano na afya kama;

- Simu na masikio
- Tarakilishi na macho
- Kelele za muziki, n.k.

Mwalimu aeleze kwamba, afya nzuri ya mwili inaweza kuokoa pesa na kusababisha ustawi na maendeleo. Pia itazuia dhuluma na kujidunisha mwenyewe ama jamii kuwa na unyanyasaji. Kwa mfano: kutokana na mtu wako kufa, hasa UKIMWI. Mwalimu aeleze suala la kiutu na kimaadili, ni kwa nini tunafanya vitendo kama kupiga mswaki, kupiga nguo pasi, kuepuka ulevi na ngono za kiholela, kufyeka nyasi ama kutofanya kazi ambazo zimepita uwezo wa ngvu za miili yetu.

Anaweza kutumia vifaa vingine kama; video, magazeti, kuzuru eneo la ujenzi baada ya kufanya matayarisho awali ili asije akahatarisha wanafunzi, n.k.

Muhimu zaidi kwa mwalimu ni kuwa, hili ni somo ambalo linasisimua kwa kuwa mwanafunzi mwenyewe anahusika na kwa hivyo udhibiti wa muda na maelezo ni muhimu. Pia, kutumia maswali ya dodosa itakuwa njia mwafaka kwake na kwa manufaa ya wanafunzi ambao hawana uwezo wa kujifunza haraka.

Wanafunzi wenyе taathira wasisahaulike; mwalimu ahuishe fahiwati zao zinginezo kama: kunusa (mfano sabuni), kushika n.k.

Hatua

1. Waelekeze wanafunzi katika kueleza na kuelewa michoro na maelezo.
2. Waulize maswali ya dodosa ili watoe maelezo zaidi.
3. Ibuu mbinu ya kuwashirikisha wanafunzi wanyonge na wenyе taathira.
4. Fafanua maneno magumu (dhana) na kuelezea maana yake;
 - Maelezo
 - Kutunga sentensi fupi
 - Kuelezea mifano mingine
5. Kila kipengele ni muhimu na kwa hivyo tilia maanani vyote

6. Ingawa kuna uhuru wa kujieleza wa mwanafunzi, dhibiti maelezo yao na kuzingatia;
 - Muda
 - Wenzao
 - Uadilifu

(b) **Masuala Mtambuka**

- Afya na maisha bora
- Usafi wa mwili na fikra
- Amani na maadili
- Mazingira bora ya mwili na hali inayotuzunguka
- Matumizi bora ya pesa
- Elimu kwa pamoja
- Usawa wa kijinsia
- Utamaduni wa kiusanifishaji
- Masomo ya jinsia na uzazi

(c) **Ujuzi wa jumla**

- Usuluhishaji wa matatizo
- Stadi za utafiti
- Ubunifu na ugunduzi
- Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha
- Ujifunzaji wa muda mrefu

Somo la I

Maana ya Usafi wa Mwili

Muda: Vipindi 3

a) Malengo ya somo

- Kusoma mazungumzo kwa usahihi na ufasaha kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi.
- Kutaja majina ya sehemu za mwili katika umoja na wingi.
- Kutaja viungo vya mwili na nafsi za Kiswahili katika umoja na wingi.

b) Vifaa vya kujifunza

- Skeletoni ya mwili wa binadamu
- Michoro au picha zinazoonyesha mwili wa binadamu
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 175
- Wanafunzi wenyewe
- Vinasasauti
- Mabango

c) Maandalizi ya somo

Hiki ni kipindi muhimu sana katika maisha ya mwanafunzi kwa sababu kinahusu mwili wake, mazingira na wale wanaomzunguka nyumbani na shulen. Mwalimu ahushe michoro na skeletoni kwa usahihi na hata kuwatumia wanafunzi wenyewe kutaja, kuonyesha na kueleza sehemu za mili yao wenyewe.

Mwalimu atumie mwili wake na viungo vya mwili wake wakati wa ufanuzi ili kurahisisha maelezo ya msamati na kufahamu viungo vinavyorejelewa. Ni vyema azingatie wakati unaofaa kutumia vifaa husika. Awashirikishe wanafunzi wote hata wenge upungufu ama taathira mbalimbali kwa kuwa afya ya mwili inawahusu wote kwa pamoja. Ni vizuri kugusa vifaa na kuvinusa ikiwezekana.

Mwalimu awagawe wanafunzi kwenye makundi kulingana na maelekezo na shughuli za kipindi hiki.

d) Utaratibu wa somo

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake. Awaulize maswali kuwakumbusha juu ya somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufasiri michoro pamoja na maelezo yaliyopo. Mwalimu awape maelezo ya kujibu kwa mfano:

Huu ni mkono.

Huu ni mdomo.

Hii ni pua.

Hizi ni nywele n.k

Pia mwalimu atumie nafsi za Kiswahili kujibu. Kwa mfano:

Mimi ni pua. Kazi yangu ni ipi?

Mimi ni mdomo. Kazi yangu ni ipi?

Yeye ni nywele. Kazi yake ni nini?

Hatua ya 2: Kusikiliza na kuzungumza

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuchambua michoro au picha. Awongoze kutazama vifaa kwa makini ili kuona sehemu mbalimbali za mwili wa binadamu. Mwalimu awapange wanafunzi kuigiza mazungumzo baina ya mwalimu na mwanafunzi. Mwalimu aeleze na kufafanua masuala magumu yanayoibuka ili wanafunzi waelewe barabara msamiati na sehemu za mwili zinazotajwa.

Mwalimu aulize maswali ya kufuatisha ili wanafunzi watoe maelezo ya kina kuhusu wanachokiona. Mwalimu asahihishe makosa ya matamshi ya wanafunzi ama usomaji na usemajji wa kusitasita.

Hatua ya 3: Msamiati

Mwalimu awongoze wanafunzi kutaja sehemu za miili yao kuanzia utosini hadi unyayoni bila utaratibu maalum. Mwalimu awapange kwenye vikundi.

Mmoja aonyeshe kiungo na wenzake wataje jina la sehemu iliyoonyeshwa na kazi yake.

Mfano:

Mdomo – kula, kupumua, kuzungumza, kuhifadhi meno na ulimi n.k.

Mwalimu awahimize kutunga sentensi rahisi fupifupi na maelezo mafupi. Ahimize kutamka kwa usahihi kulingana na sauti za Kiswahili.

Hatua ya 4: Ufahamu

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma kwa zamu na kwa sauti bila kusitasita. Mwalimu akosoe makosa ya matamshi ya silabi na maneno na pia kusoma kwa ufasaha. Kisha mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma kimya kimya na kwa kuzingatia yaliyomo. Mwalimu afafanue maneno yote magumu na kuyatolea maana yake. Mwalimu aulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu kinachohusu mwalimu na mwanafunzi. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu. Mwalimu akitosheka kuna uelewa wa kawaida, awaelekeze katika maswali ya ufahamu. Mwalimu asahihishe majibu ya wanafunzi.

Hatua ya 5: Sarufi

Hii ni sehemu muhimu sana. Mwalimu atumie sehemu hii kufundisha umoja na wingi wa sehemu za mwili. Kwa mfano:

Jino - Meno

Kifua - Vifua n.k.

Mwalimu atumie picha ama wanafunzi wenyewe. Mmoja aonyeshe kwa mfano mguu mmoja kisha atoe mguu wa pili. Kisha mmoja awaulize wenzake wanaona miguu mingapi? Wajibu; miwili. Wafanye hivyo kwa viungo vyote vingine.

Mwisho, mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu zoezi la sarufi. Mwalimu asahihishe kazi za wanafunzi na kuwapa mwongozo.

Hatua ya 6: Hijai na matamshi bora

Mwalimu atumie hatua hii kuhimiza utamkaji wa msamiati wa sehemu za mwili na kuyaendeleza kikamilifu. Mwalimu ahimize utamkaji wa silabi mojamoja.

Mifano:

M-ko-no

Ki-chwa

M-gu-u, n.k.

Mwalimu atumie imla kutathmini sehemu hii. Pia anaweza kutumia fumbo lenye msamiati wa viungo vya mwili au atumie chemshabongo. Mwalimu akosoe makosa ya matamshi na maendelezo mabaya ya msamiati.

Hatua ya 7: Hitimisho

Hi ni sehemu ya mwisho ya somo hili. Mwalimu aulize maswali ya kutathmini na wanafunzi wajibu kabla ya kuwapa maswali ya marudio ama zoezi la ziada. Mwalimu awaambie wanafunzi wataje sehemu zote za mwili walizosoma na pia kuzionyesha kwenye michoro na picha.

E. Zoezi la Ziada

Kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi wa kiwango cha chini, mwalimu atumie zoezi la ziada na mengine kuwaelekeza. Awaulize maswali nao wanafunzi wajibu. Wanafunzi wanaweza kunyoosha mikono na mwalimu kuwateua kwa zamu huku wakijibu.

Mfano wa zoezi la ziada

Eleza umuhimu wa sehemu zifuatazo za mwili:

1. Miguu
2. Kinywa
3. Mikono
4. Macho
5. Magoti

F. Tathmini

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali ya chemshabongo kuhusu msamiati waliojifunza. Pia anaweza kutumia imla kutathmini iwapo watakumbuka msamiati huo. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanatambua umuhimu wa kujifunza, wasiathiri viungo vya mili yao na vile vile kulinda afya zao kwa kuwa safi.

MAJIBU

Zoezi la 1, ukurasa 179

1. Mkono 2. Kichwani 3. Sabuni 4. Mswaki 5. Nywele

Zoezi la 2, ukurasa 179

1. Nywele 2. Mwili 3. Nywele 4. Kucha 5. Nguo

Zoezi la ufahrenu, ukurasa 181

1. Kusikia 2. Kutembea 3. Kuona 4. Kuzuia baridi
5. Kunusa/Kupimwa 6. Kukamata 7. Nywele 8. Vidole/Kiganja
9. Uso 10. Mguu

Zoezi la 1, ukurasa 182

1. Mikono 2. Vidole 3. Ndevu 4. Vinywa 5. Miguu

Zoezi la 2, ukurasa 182

1. Pua 2. Utosi 3. Unywele 4. Kifua 5. Mdomo

Zoezi la ubunifu, ukurasa 183

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

Zoezi la utafiti, ukurasa 183 - 184

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

Somo la pili

Msamiati wa Mwili na Mazingira

Muda: Vipindi 3

a) Malengo ya somo

- Kutaja na kusoma kwa usahihi herufi, maneno na sentensi.
- Kutaja sehemu za mwili zinazotakiwa kufanyiwa usafi.

b) Vifaa vya kujifunza

- Kiwiliwili cha binadamu
- Michoro au picha
- Kitabu cha mwanafunzi, ukurasa 185
- Wanafunzi wenyewe
- Vinasasauti
- Magazeti

c) Maandalizi ya somo

Kipindi kinahusu kutaja sehemu za mwili ambazo zinahitaji usafi wa hali ya juu. Kwa mfano:

- Kinywa (mdomo)
- Makwapa
- Sehemu nyeti
- Kichwa (nywele) n.k.

Mwalimu aeleze ni kwa nini kukosa kupiga mswaki kunaweza kuathiri uhusiano na wengine kutokana na uvundo n.k.

Mwalimu ahakikishe kuwa ameleta vifaa vyote vinavyohitajika ambavyo wanafunzi wanaweza kugusa na kuona. Mwalimu awapange wanafunzi katika vikundi ambavyo

vinawezesha kutumia vifaa kikamilifu.

Hatua ya 2: Kusikiliza na kuzungumza

Mwalimu awalekeze wanafunzi kutazama michoro na kisha maelezo yanayoambatana nayo. Mwalimu aulize maswali ya kutathmini ufasiri wa michoro na wanafunzi. Hatimaye, kifungu kinachohusu usafi wa mwili na pia sentensi. Mwalimu awalekeze wanafunzi kuandika mifano na maelezo muhimu kwenye madaftari yao. Mwalimu awaulize wanafunzi faida na hasara za kufanya usafi. Kwa mfano, kukata na kuchana nywele kuepuka kupata chawa, kuonekana vibaya na kupata maradhi.

Hatua ya 3: Msamiati

Mwalimu atoe maelekezo na maelezo kuhusu sehemu zinazohitaji usafi kama kinywa, makwapa na kueleza sehemu zinapopatikana na kazi yake. Wanafunzi wapangwe kwenye makundi ili wajadiliane na kutoa hoja zao kuhusu sehemu husika. Watamke na kuendeleza maneno husika kwa kutamka silabi kifasaha.

Mwalimu akosoe matamshi mabaya na uendelezaji mbaya. Hatimaye mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi la tahajia na matamshi bora.

Hatua ya 4: Ufahamu

Mwalimu awalekeze tena wanafunzi kwenye michoro na kifungu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote hata wenye upungufu wa viungo ili kuhakikisha kwamba wanafahamu yaliyomo. Mwalimu awaweke wanafunzi kwenye makundi ya kujadili vifungu pamoja na maswali ya ufahamu. Wanafunzi wajibu pamoja huku mwalimu akisahihisha kazi na majibu ya wanafunzi.

Hatua ya 5: Sarufi

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutaja viungo vya mwili kwa umoja na wingi hasa vile vinavyohitaji usafi sana kama; kichwa – vichwa, unywele – nywele, kwapa - makwapa n.k. Mwalimu awalekeze wanafunzi kutaja umoja na wingi wa viungo vya mwili. Pia atumie nafsi za Kiswahili kutaja na kuelezea umoja na wingi wa viungo na nafsi.

Tazama wimbo wa viungo (uk 180)

Hatimaye, mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya mazoezi ya sarufi. Mwalimu asahihishe majibu ya wanafunzi na kuwapa mwelekeo unaofaa.

Hatua ya 6: Hijai na matamshi bora

Mwalimu awalekeze wanafunzi wake kutaja kwa matamshi bora silabi na maneno kwa kuzingatia matamshi ya Kiswahili. Pia, mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika kwa hati nzuri. Atumie sehemu hii kuhimiza msamiati uliofundishwa barabara.

Hatua ya 7: Hitimisho

Hadi sasa, wanafunzi wameanza kumudu msamiati wa viungo vya mwili. Mwalimu aulize maswali ya tathmini kwa kutumia michoro na wanafunzi wajibu ikiwa wameelewa au la. Mwalimu atumie zoezi la ziada kwa wanafunzi wa kiwango cha chini na awape wanafunzi wa kiwango cha juu maswali ya marudio.

E. Mazoezi ya ziada

Mwalimu awashughulikie wanafunzi wa kiwango cha chini. Atumie zoezi la ziada kuwaongoza wanafunzi hao na awape wanafunzi wa kiwango cha juu kazi zaidi. Pia atumie maswali ya imla na chemshabongo kama njia ya kuchochea zaidi usomaji na uelewaji.

Mfano wa zoezi la ziada

Andika wingi wa maneno yafuatayo:

1. Kichwa
2. Malaria
3. Tumbo
4. Mguu
5. Jino

F. Tathmini

Mwalimu atumie imla, chemshabongo na maswali kutathmini uelewaji wa wanafunzi wake. Wanafunzi wanyooshe mikono na mwalimu atue mwanafunzi mmoja mmoja kwa kuzingatia jinsia zote na kila hulka ya mwanafunzi.

Zoezi la ufhamu, ukurasa 186 - 187

1. Tumbo 2. Maji safi 3. Mvua 4. Kuchemsha 5. Mdudu

Zoezi la mjadala, ukurasa 187

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

Zoezi la 1, ukurasa 188

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi

Zoezi la 2, ukurasa 188

Mwalimu akadilie majibu ya wanafunzi.

Zoezi la ziada, ukurasa 188

1. a) 2. Mbu 3. Maji 4. Nyasi 5. Mazingira

Zoezi la mjadala, ukurasa 189

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

Zoezi la 1, ukurasa 189

1. Mabega 2. Viuno 3. Ndevu 4. Vidole 5. Vichwa

Zoezi la 2, ukurasa 189

1. Jino 2. Paja 3. Kinywa 4. Pua 5. Udevu

Zoezi la ziada, ukurasa 190

- | | | |
|---|-------------------------|----------------|
| 1. Kutembea 2. Kukamatana | 3. Kuona 4. Kunusa | |
| a) Kuweka nguvu | | |
| b) Kubeba kichwa | c) Kukanyaga chini | d) Kusimamisha |
| c) kiwiliwili (Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi) | | |

Somo la 3

Usafi wa Mwili na Mazingira

Muda: Vipindi 3

a) Malengo ya Somo

- Kutaja magonjwa yanayotokana na kukosa usafi na mazingira machafu
- Kusoma kwa ufasaha, usahihi na kwa matamshi bora ya silabi, maneno na sentensi.

b) Vifaa vya Kujifunza

- Kiwiliwili cha mwili wa binadamu
- Vitabu vyenye michoro ya mwili wa binadamu
- Picha au michoro
- Kitabu cha mwanafunzi, ukurasa 191
- Wanafunzi wenyewe
- Vinasasauti

c) Maandalizi ya Somo

Kipindi hiki kinashughulikia maradhi mbalimbali yanayoathiri mwili wa binadamu. Kinahusu maradhi kama UKIMWI, kichocho, kipindupindu, homa ya matumbo n.k. Mwalimu atumie fursa hii kuwaliza wanafunzi kutaja aina ya magonjwa wayajuayo na kuyahusisha na uchafu wa mazingira ya miili yetu na mazingira kwa ujumla. Mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja athari za magonjwa.

Mfano:

- Kifo
- Ulemavu
- Afya mbaya
- Kutengwa n.k.

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake nao wamjibu. Kisha, awaulize maswali kuhusu somo lililopita. Pia atumie michoro ya ufunguzi katika kitabu cha mwanafunzi na hata kuwapanga ili waigize kifungu kinachohusu maradhi na afya ya mwili. Mwalimu akosoe matamshi na kusoma kwa kusitasita kwa wanafunzi. Mwalimu atoe fursa ya mjadala mionganoni mwa wanafunzi na kuwaongoza kuelewa na kuthamini miili na afya yao.

d) Utaratibu wa Somo

Hatua ya 1: Utangulizi

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwenye kifungu na michoro mwanzoni mwa somo hili. Mwalimu awaulize kutaja ugonjwa na namna unavyosababishwa. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua kwamba tabia pia inaweza kusababisha mwili kuathirika. Kwa mfano, uzinifu na uasherati unaweza kusababisha magonjwa ya zinaa na UKIMWI. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuandika mifano ya magonjwa na athari zake kwenye madaftari yao. Mwalimu akosoe makosa ya matamshi na kusoma kusiko kwa kumakinika.

Hatua ya 2: Kusikiliza na Kuzungumza

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma kifungu kwa makini, usahihi na ufasaha. Mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja magonjwa mbalimbali na athari zake kwa mwili wa binadamu. Mwalimu asahihishe maelezo yasiyo sahihi na matamshi mabaya na kusoma kusikofaa. Kama vile, kusoma kwa kusitasita. Mwalimu awapange kwenye makundi ili waigize mazungumzo kati ya daktari na mgonjwa. Mwalimu afafanue masuala magumu na hata magonjwa.

Mwalimu aruhusu kipindi cha maswali na majibu kama njia ya kuchochea uelewaji.

Hatua ya 3: Msamiati

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la msamiati. Atumie vifaa alivyo navyo kufafanua sehemu za mwili zinazoathirika, athari husika na matokeo ya kuathirika huko kijamii, kiuchumi, kitaaluma n.k.

Kijamii kwa mfano, kuwapoteza wapendwa wetu. Kiuchumi; kutumia gharama nyingi kwa matibabu, kupoteza wafanyakazi na pia kupoteza wasomi.

Mwalimu awahimize wanafunzi kuheshimu miili yao kwa kuepuka vitu kama sigara, pombe, magonjwa ya zinaa, miraa na dawa za kujidunga. Pia awatahadharishe kuhusu uhalifu. Awaongoze wanafunzi kutunga sentensi sahihi kwa kutumia majina ya maradhi na viungo vya mwili.

Hatua ya 4: Ufahamu

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma mazungumzo baina ya daktari na mgonjwa. Mwalimu afafanue masuala magumu na kutoa maelezo ya kuwafanya wanafunzi kuelewa somo barabara. Mwalimu vivyo hivyo awaelekeze wanafunzi kufasiri michoro na maelezo yanayoandamana nayo.

Mwalimu awapange wanafunzi kusoma kwa sauti na kwa zamu. Hatimaye, anaweza kutoa fursa ya kuigiza mazungumzo baina ya daktari na mgonjwa. Wanaweza kuwa katika vikundi vya wanafunzi watatu watatu ama watano watano kutegemea ukubwa wa darasa. Mwalimu awaongoze wanafunzi kuitia maswali ya ufahamu kwa ushirikiano. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wanashirikishwa hata wale wenye taathira ya kuona ama kusikia.

Hatua ya 5: Sarufi

Kufahamu sarufi ya lugha ni muhimu sana katika kupata umilisi wa lugha yoyote ile. Mwalimu atumie wimbo wa viungo vya mwili kutaja sehemu za mwili na maradhi katika umoja na wingi. Licha ya kutaja, mwalimu awaongoze wanafunzi kuelewa viambishi vya umoja na wingi.

Mfano:

Jicho huwa macho

Jino huwa meno

Kichwa huwa vichwa

Mkono huwa mikono

Kidari huwa vidari n.k.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kueleza kazi ya viungo wanavyovitaja. Pia watunge sentensi nyepesi katika umoja na wingi.

Mfano:

Umoja	Wingi
--------------	--------------

Huu ni mkono.	– Hii ni mikono.
---------------	------------------

Huu ni mguu.	– Hii ni miguu.
--------------	-----------------

Huu ni ulimi.	– Hizi ni ndimi.
---------------	------------------

Hatua ya 6: Tahajia na Matamshi Bora

Matamshi ni muhimu pamoja na hijai. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutamka barabara na pia kuendeleza msamiati aliopewa kwa njia bora. Mwalimu ahimize matamshi bora ya silabi na sentensi na pia kuandika kwa hati nzuri. Mwalimu atumie nafasi hii kusitiza mwandiko mzuri na usomaji wa kifasaha.

Hatua ya 7: Hitimisho

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuuliza maswali ya dodosa kuhusu mambo mbalimbali kuhusu sehemu za viungo vya mwili na maradhi kwa kutumia vifaa kama wanafunzi wenyewe na pia michoro na picha. Mwalimu atoe zoezi la ziada kwa wanafunzi wa kiwango cha chini na maswali ya marudio kwa wanafunzi wa kiwango cha juu.

E. Mazoezi ya Ziada

Ili kuwasaidia wanafunzi wa kiwango cha chini, mwalimu atumie mazoezi ya ziada yaliyopendekezwa kuwakumbusha waliyoyasoma na pia kuwasaidia waelewe somo barabara. Mwalimu asiwasahau wanafunzi werevu kwa kuwapa kazi zaidi na maswali ya marudio.

F. Tathmini

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali aina ya yale ya kufuatisha ndiposa kutathmini iwapo wamepata dhana ya somo hili. Pia mwalimu atumie mbinu ya imla na njia ya kuwachochaea wanafunzi kuuliza maswali na kujibu. Wanafunzi wahimizwe kutumia

umoja na wingi wa msamiati wa usafi wa mwili pamoja na maradhi. Pia watumie nafsi za Kiswahili. Hata hivyo, mwalimu atilie maanani umoja na wingi wa msamiati husika.

MAJIBU

Zoezi la mjadala, ukurasa 193

Mwalimu apime hoja za wanafunzi.

Zoezi la I, ukurasa 194

1. Vitu na hali 2. Wadudu 3. Magonjwa 4. Mdudu 5. (a)

Zoezi la 2, ukurasa 194

Mwalimu akadirie majibu ya wanafunzi.

Zoezi la ufahamu, ukurasa 195

1. 6 2. Mbu 3. Kwenye vumbi/mtu aliyeumwa (mwilini)
4. Kukohoa sana 5. Kipindupindu

Zoezi la mjadala, ukurasa 195

Mwalimu akadirie hoja za wanafunzi.

Zoezi la I, ukurasa 196

1. Ukimwi 2. Wadudu 3. Magonjwa 4. Funza 5. Usafi

Zoezi la 2, ukurasa 196 - 197

1. Kunywa maji safi.
2. Ua mdudu.
3. Badilisha tabia yako.
4. Fagia nyumba yako.
5. Osha chombo kichafu.

Zoezi la ziada, ukurasa 197

- | | | | |
|-----------|-----------|------------|-----------|
| 1. Uchafu | 2. Mwili | 3. Ugonjwa | 4. Wadudu |
| 5. Mkono | 6. Vichwa | 7. Miguu | 8. Kiuno |
| 9. Macho | 10. Pua | | |